Kikao cha Ishirini - Tarehe 11 Julai, 2013

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, taarifa ya Spika ambayo ninakusudia kuitoa hapa ni taarifa ya kawaida ambayo inatokana na shughuli mlizozifanya Waheshimiwa Wajumbe. Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa 12 wa Baraza la Nane la Wawakilishi ulianza tarehe 12/6/2013, Baraza lilipitisha Mswada mmoja wa sheria ambao ni kama ifuatavyo:-

Mswada wa Sheria ya kutoza kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za fedha na kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo, kama inavyotakiwa chini ya kifungu 90(3)3 cha kifungu hicho cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012, naomba Waheshimiwa Wajumbe kutoa taarifa kwamba mswada huo sasa umekuwa ni sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe, shukurani nyingi kwa kazi nzuri mliofanya na Mhe. Rais, ameshaikubali kazi hiyo.

Leo vile vile Waheshimiwa Wajumbe tunao wageni kama kawaida ambao na leo tuna wanafunzi, wageni wetu wa leo ni wanafunzi wa Skuli ya Ben-Bella, jumla ya ni wanafunzi 60 ambao wamefuatana na walimu wao wawili. Naomba nichukue nafasi hii wanafunzi hao pamoja na walimu wao sasa wasimame. Ndugu walimu pamoja na wanafunzi karibuni sana ili muone wazee wenu wanafanya kwa ajili yenu. Ahsante sana, karibuni Waheshimiwa Wajumbe ninakushukuruni.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hati ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka 2013/14.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/14 - Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto

(Majadiliano yanaendelea)

TAARIFA

Mhe. Spika: Mhe. Wajumbe ninataka muelewe kwamba shughuli zetu mara hii kwa kweli zimerefuka sana kutokana na haja na hoja zenu Waheshimiwa Wajumbe, kufuatana na hotuba mbali mbali za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara mbali mbali zilizotangulia kuchukua muda mkubwa zaidi kuliko vile ambavyo tulipanga katika ratiba. Tumejaribu kurekebisha ratiba hiyo ambayo tayari tumeshakuwa tuko nyuma kama kwa siku tano hadi sita hivi, na tukaweka ratibu nyengine ambayo nafikiri jana au juzi tuliigaiwa nayo pia sasa tushaanza kuwa nyuma kwa karibu siku moja. Sasa hilo jambo kwa kweli linatukwaza linatufikisha pahala pagumu kidogo kwa sababu huenda tukamalizia shughuli hizi bila ya kuwa na matumizi ambayo yamekuwa yamepangwa kwa ajili ya mkutano huu wa bajeti.

Hivyo Waheshimiwa Wajumbe ninawaomba tushirikiane kwa pamoja kama ilivyo kawaida yetu ili tuone shughuli zetu angalau basi zitakwenda kwa mujibu wa ratiba hii mpya ambayo imetolewa, nafikiri kila mmoja Waheshimiwa Wajumbe wameshapata ili tufikie ikaja ikawa tumeruka mno na bajeti ambayo imepagwa kwa ajili ya kuendesha mkutano huu wa bajeti. Kuna muelekeo ambayo haijawahi kutokea kwamba mara hii kasoro kidogo mkutano wa bajeti uwe unachukua miezi miwili, kwa kweli itakuwa ni muda mrefu sana zaidi kuliko ambavyo kwa kawaida huwa tunafanya shughuli zetu.

Implication yake ni kwamba tunafanya matumizi makubwa zaidi kuliko yale ambayo Waheshimiwa Wajumbe tulipitisha. Sasa hiyo kidogo inakuwa ni tatizo, pengine chombo hichi na si pengine ndio hasa kinatemewa kikawa mfano mzuri wa *discpline* ya matumizi, ili

Waheshimiwa Wajumbe mpate ile nguvu sasa ya kuhoji Wizara nyengine juu ya namna wanavyotumia kwa ufanisi, kwa sababu naamini kama kutakuwa na matumizi ya ziada basi Wajumbe sisi tutahoji vipi, lakini unahojije wakati wewe mwenyewe kumbe katika nyumba yako hujasafisha vizuri, itakuwa haielekei si vyema si utaratibu na itakuwa hata hizo Wizara hatuzitendei haki kuona kwamba tunawalaumu lakini kwamba kumbe ilikuwa tuanze kujilaumu sisi kwa kufanya matumizi kinyume na utaratibu.

Basi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tulione hilo na tushirikiane kuona kwamba tunakwenda kwa mujibu wa ratiba iliyowekwa tusikiuke yale matumizi ambayo sisi wenyewe tulijiidhinishia kwa ajili ya shughuli zetu. Kwa mujibu wa orodha niloyonayo sasa zamu ya Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo katika Wizara hii ya Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, mchango wangu mimi utakuwa ni mdogo tu lakini utajikita sana katika suala la udhalilishaji wa watoto na jinsia na hii ni kwa sababu Waheshimiwa Wawakilishi wengi walilizungumza suala hili.

Mhe. Spika, suala hili ni zito na ni gumu lakini si kwa hapa petu tu Zanzibar, kwa kweli katika nchi nyingi hasa zile za Maziwa Makuu nao wana matatizo kama haya. Mwaka juzi Marais wa Nchi hizi za Maziwa Makuu walikutana Uganda na suala moja katika mambo ambayo waliyazungumza ni suala hili la udhalilishaji wa watoto pamoja na wanawake. Kule Uganda lilitoka azimio kwamba Mawaziri wanaohusika na masuala ya watoto, pamoja na Waziri wa Sheria wakutane ili walijadili suala hili. Mhe. Spika, Mawaziri hao wa nchi zote hizo walikutana Kinshasa - Zaire na ajenda kubwa iliyokuwepo ni suala hili, lilijadiliwa kwa kina kabisa na ninapenda niseme tu kwamba nchi zote hizi zina mazingira tofauti katika maeneo. Kwa mfano ukichua Congo udhalilishaji wa wanawake na watoto umepita mpaka na hii ni kwa sababu hasa majeshi nao walikuwa ni moja katika watu waliokuwa wakisemwa sana katika suala zima la udhalilishaji, wale wenzetu kule kwa sababu tunajua kwamba wapo kwenye vita basi suala hili wanalichukua kwa juhudi kubwa sana.

Mhe. Spika, katika mkutano huo kuna mambo ambayo yalikubaliwa na kwamba mambo haya ni lazima nchi zinazohusika wayafuate. Naomba kwa ruhusa yako niyaseme kidogo haya mambo ambayo yalikubaliwa katika mkutano huo.

Kwanza kwa kwa nchi uanzishwaji wa Mahakama Maalum utaruhusu basi Mahakama hizo zianzishwe mara moja, lakini la pili kwa nchi nyengine basi wanaweza kuanzisha *session cases* na la tatu ni kwamba Mahakama ziliopo nchini zipewe madaraka zaidi kusikiliza kesi aina hiyo kwa haraka, lakini kwa nchi nyengine ambazo masuala haya ya ubakaji ni makubwa na hasa kwa maeneo ya machafuko na vita basi ianzishwe *mobile court* ili Mahakama ziweze kufika huko kwenye matukio. Kuwe na ugumu wa kesi hizi kupewa dhamana hata kama dhamana ni haki ya mtu, kesi aina hizi zichukue miezi sita tu kwa wingi, yaani isizidi miezi sita, kuanzia mtu anapofanyiwa uchunguzi hadi tarehe ya hukumu na jitihada maalumu zichukuliwe kwa kila nchi kutangaza ubaya wa suala hilo. Hayo ndio mambo muhimu ambayo yalikubaliwa katika mkutano huo na nchi wanachama ikiwemo Zanzibar tulitakiwa sote tu-*comply* na maagizo hayo.

Mhe. Spika, napenda niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba haya ndio tunayoyafanya kazi hivi sasa na kwa Zanzibar tulisema kwamba jambo zuri itakuwa ni kuanzisha *session cases*, yaani pale kesi ambapo mtu anakamatwa mpaka anatiwa hatiani basi kwanza isizidi kuliko miezi sita lakini kesi ile iwe haina kuahirishwa, inaanza leo tunakwenda moja kwa moja mpaka tunamaliza. Utaratibu huo ndio tunaouandaa hivi sasa na napenda nishukuru kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wameshatupitishia bajeti yetu kwa sababu tulikuwa tunasubiri hayo na bajeti ya Mhe. Zainab ili ipite tukae pamoja sasa tutizame utaratibu huo wa kuanzisha *session cases*. Kwa sababu tunaamini kwamba hii *session cases* tukijaaliwa tutaianzisha katika kipindi hiki ili ku-*comply* na maagizo hayo ya mkutano huo wa Kinshasa.

Mhe. Spika, pia tulitakiwa tuseme kwa mfano katika redio na televisheni tutoe matangazo na matangazo hayo yawe yana mambo chungu mzima ya kutoa kama indhari kwa watu na wale ambao wanashughulika na mambo haya. Kwa mfano kuwa na mabango, au kuwe na matangazo yanayolani vitendo hivi, kuwe na matangazo yanayowalaani wale wafanyaji na kuwauliza katika hayo matangazo kwa mfano, moja *specifically* ambalo limetolewa ni kwamba *TV* kwa mfano na redio na michezo ioneshe kwamba je kama wewe ni mbakaji na unabaka watoto na unabaka wanawake, sasa mama yako je, akibakwa au dada yako au ndugu yako. Sasa mambo kama haya wakishakupewa wale nafikiri kidogo itawagusa na itawaingia. Sasa hilo tumeshakutana na Wizara ya Habari ili kuandaa vipindi kama hivi kujaribu kuwatanabahisha wale watu ambao wana matatizo kama haya.

Mhe. Spika, mbali na haya ni kwamba katika masuala haya pia ilikubaliwa kwamba kweli kwa sababu hizi kesi ni *criminal case* na unajua kwamba *criminal case* zina utaratibu wake, utaratibu huu ulionekana kwamba ni mgumu na unaweza ukazorotesha haya malengo ambayo tunataka kuyafikia. Kwa hivyo katika kikao hicho ilikubaliwa vile vile kwamba nchi wanachama wajaribu kutizama sheria zao na sheria hizo zilenge mambo yafuatayo.

Mhe. Spika, katika mambo hayo ni kwamba kuna mambo matatu ambayo yalikubaliwa na lazima tuyafuate. Kwanza ni kwamba sheria tuzitizame na hasa katika lile suala la *criminal procedure* yaani ule utaratibu wa kesi kama hizi. Tunajua kwamba kesi kama hizi zina taratibu zake na taratibu hizi wakati mwengine ni ngumu. Kwa hivyo ikaonekana kwa mambo kama haya hivyo inaweza ikazorotesha kidogo. Hivyo agizo lililotoka ambalo na sisi tunalifanyia kazi ni kwamba ule utaratibu wote wa *criminal procedure* tuuondoe ya kwamba mdhalilishaji yule au mtuhumiwa asipate dhamana za wakati wote ule. La pili kwamba kesi hii isizidi miezi sita kuanzia kutizamwa yaani kuanzia pale ambapo ilipopokewa kesi mpaka kutolewa kwa hukumu na kwamba mbali na hayo hizi kezi zichukuwe kifungo cha miaka mingi. Kwa hiyo hayo ndio maagizo na kwamba yale mambo ya *procedures* katika *criminal* yaondolewe moja kwa moja.

Mhe. Spika, hivi sasa tuko katika utaratibu huu tumeshaangalia baadhi ya sheria zetu, tumeshaona wapi mwa kubadilisha lakini kuna utaratibu wake ambao tunaufuata hivi sasa. Tumeshazungumza kama nilivyosema na Wizara ya Habari katika suala la kutoa matangazo na katika suala la kutoa matangazo kwenye *TV* na kwenye *redio*, lakini zaidi ni kuwapa watu uhakika kwamba suala hili tunalitizama kama ilivyo. Sasa baada ya hayo Mhe. Spika, humu ndani yaani katika Zanzibar nchini mwetu baada ya kurudi tulipeleka ripoti hii katika Baraza la Mapinduzi na Baraza la Mapinduzi wakakubaliana na maamuzi haya na Baraza limetoa ushauri wake kwamba tuendelee na shughuli hii. Kuna Mawaziri watatu ambao waliteuliwa kushughulikia mimi nikiwemo, Mhe. Bi. Zainab na Mhe. Waziri wa Afya tulishughulikie pamoja na wajumbe wengine, tumeshakutana mara nyingi tu katika kulikamilisha suala hili. Kwa hivyo utakapokamilisha basi haya yote yataweza kufanyika.

Mhe. Spika, jengine ambalo tulilizungumza ni kwamba hivi sasa kuna suala zima la ushahidi wa watoto, wewe mwenyewe unajua kwamba ushahidi wa watoto ni mgumu kidogo lakini katika mkutano huu uliona

tatizo hilo la ushahidi wa watoto na ikasemwa kwamba katika marekebisho ya sheria basi tujitahidi kwamba ushahidi wa watoto tuweke njia ambayo inaweza ikakubalika. Kwa hivyo ndio maana hatua ya mwanzo ambayo tumeifanya ni kwamba ile Mahakama ya Watoto, unapotoa ushahidi pale yule mtoto hata pengine hatoonekana kwa sababu pengine akimuona yule mtu aliyemfanyia vitendo vile yule mtoto anaweza akaogopa, anaweza akatishwa. Kwa hivyo tutakuwa na masuala ambayo pengine hutomuona yule mtoto anaulizwa anajibu. Pia hiyo inaweza ikasaidia na kwamba katika kisheria ushahidi wa mtoto lazima uwe-*collaborated*, yaani lazima uwekewe mwega au kusaidia na ushahidi mwengine, unatizama njia ya kufanya, yaani ushahidi huu wa kitoto uwe unakubalika moja kwa moja kutokana na maagizo hayo.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema suala hili tunalijua, Serikali inajua na tumejitahidi kufanya hayo ili kuweza kulipatia ufumbuzi. Naomba niseme tu haya yote kama hatutoshirikiana na wazee na jamii basi utaratibu wote huu unaweza ukaharibika, namna gani kwa sababu hivi sasa tuna matatizo, kuna kesi nyingi ambazo mtu akikamatwa basi ama wazee wa mtoto watakwenda polisi au atakuja kwetu kusema kwamba kesi hii wanaomba ifutwe isiende Mahakamani, watasema huyu aliyefanya ni mtoto wa Mjomba wangu au mtoto wa jirani, kwa hivyo mtaani pale patakuwa hapana uelewano mzuri, kwa hivyo tumeshakubaliana sisi tunaomba tuifute. Sasa tukifanya hayo hatutafika mbali, vitendo vitaendelea na makosa haya yataendelea kwa kasi, kwa sababu mtu atajua kwamba hana kitu ambacho atakipata, hana adhabu ambayo atatiwa, hii inatokana na wazee wenyewe na jamii kwamba wanachukulia kesi hizi kama ni kesi rahisi kabisa.

Mhe. Spika, ombi langu ni kwamba kesi kama hizi zinapotokea tunaomba sana wananchi na jamii kwamba wakubali kukaa mashahidi ili kesi hizi ziweze kuendelea, kwa sababu tatizo kubwa hapa ni kwamba ukimwambia aje akae ushahidi sasa hapo hataki, hata ukimwita haji na mwisho atakwambia bora ifutwe tumeshakubaliana. Kwa hivyo itakuwa hatufanikiwi kwa sababu lazima tupate ushahidi, lazima watu waje Mahakamani na wao hawataki lakini marekebisho haya yanaweza yakasaidia kwamba ushahidi ule tunaweza tukautoa baada ya kupata baadhi ya mambo ambayo tunayategemea na hasa kuna suala jengine la *DNA* ambalo tulikuwa na matatizo ya *DNA* kama alivyosema Waziri wa Afya kuwa *DNA* baadhi ya sehemu zimepatikana lakini hata katika hii sheria tunatizama sana tutafanya namna gani, ili hata hili suala la DNA liwe kidogo si lazima sana. Maana yake hivi sasa kila mtu anakwambia lazima achekiwe *DNA* na *DNA* hakuna inaweza

ikakaa kesi mwaka mzima. Hilo nalo ni tatizo lakini pia katika sheria hii ambayo tunaijaribu kuitizama nalo litazingatiwa.

Mhe. Spika, mimi naomba niseme tu kwamba hivi sasa tunayo hiyo Kamati ambayo inasimamiwa na Mawaziri watatu na watu kutoka *DPP* na watu wengine, Mashekhe ili tuweze kutizama ni kitu gani. Suala hili pia liliingia katika suala zima la vyuo, ni bahati mbaya kwamba baadhi ya wanaoitwa Maustadhi sio watu wazuri, sio watu wazuri kwa sababu wanachukua fursa hii kuwaharibu watoto. Hili pia Serikali limeliona na katika Wizara yangu hivi sasa tumeanzisha kuorodhesha vyuo vyote na vyuo vile hatutoviorodhesha mpaka tufanye utafiti ni mwalimu gani atakayesomesha, watoto wangapi na mwalimu huyo tupate historia yake, tukiona historia yake ni mbaya chuo kile hatutokikubali. Tumeshafanya hivyo kwa baadhi ya sehemu kuna maeneo ambayo tumeyataja. Wako watu watasema kidogo kwa nini tunawakatalia na nini, lakini tukifanya hivyo ndio tutawanusuru hawa watoto wetu.

Pia katika suala hili la Maustadhi hawa pia naombaWaheshimiwa Wawakilishi wajue tu kwamba Serikali tumeshaanza kuchukuwa hatua, tumeorodhesha hivi sasa kuna vyuo karibu 2000 lakini vyengine tunavipitia kwa kutizama hayo na pale ambapo mwalimu hana sifa zile tunazozitaka, kwa hivyo mwalimu huyo hatumpi leseni ya kusomesha.

Mhe. Spika, hatua tunazichukua ni kama hizo ambazo tunazichukuwa na naamini mashirikiano ya Waheshimiwa Wawakilishi, wazee, jamii basi suala hili tunaweza tukalipunguza kwa kiasi kikubwa sana. Hilo ndilo lengo na ndilo ambapo hivi sasa Kamati hiyo iliyoteuliwa na Baraza la Mapinduzi tunalifanyia kazi.

Mhe. Spika, baada ya kumaliza hayo yote pengine baadae tutakuja na sheria ambayo itarekebisha mambo haya. Lakini kwa hivi sasa tumeshaanza kukutana na hivi sasa tumeshakutana kiasi mara mbili tatu ili kujadili hii *session case* zitafanywa namna gani, hasa kwa sababu ukifanya *session case* lazima upate Hakimu anayekwenda moja kwa moja na nashukuru Baraza limetupitishia bajeti kidogo. Kwa hivyo tutajitahidi ili kesi hizi kama ilivyotoka agizo katika mkutano huo wa Kinshasa kwamba ikianza leo basi isizidi miezi sita na hukumu kubwa itakuwa imeshatoka.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Wanawake na Watoto, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu hoja za Wajumbe kama zilivyozungumzwa.

Lakini pia Mhe. Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wote waliochangia bajeti hii ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Bajeti hii Mhe. Spika, imeungwa mkono na Wajumbe wote waliosimama kuichangia bajeti hii isipokuwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Lakini kwa bahati nzuri Mhe. Jaku kwanza alitupongeza kwa sababu yeye alikuwa ni Mjumbe wetu wa Kamati katika kipindi kilichopita aliona namna ya utendaji wa Wizara hii ya Ustawi wa Jamii. Baadae tena akatumia nafasi yake ya kunishtua kidogo hilo si tatizo kwangu.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wizara ya Ustawi wa Jamii napenda kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliochangia ambao walikuwa wajumbe 24 na walioleta kwa maandishi walikuwa wajumbe 5. Waliochangia hotuba ya bajeti ya wizara yangu moja kwa moja au kwa maandishi, michango yao kwa njia moja au nyengine itaweza kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara. Miongoni mwa wajumbe waliochangia katika hotuba hii ya bajeti ya wizara hii ni pamoja na:-

1. Mhe. Mahmoud Mohamed Mahmoud
2. Mhe. Mohamed Haji Khalid
3. Mhe. Ali Salum Haji
4. Mhe. Farida Amour Mohamed
5. Mhe. Fatma Mbarouk Said
6. Mhe. Marina Joel Thomas
7. Mhe. Asha Bakari Makame
8. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
9. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
10. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
11. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
12. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
13. Mhe. Asha Abdu Haji
14. Mhe. Hija Hassan Hija
15. Mhe. Abdi Mossi Kombo
16. Mhe. Salma Mussa Bilali
17. Mhe. Kazija Khamis Kona

18. Mhe. Salma Mohamed Ali
19. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
20. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
21. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
22. Mhe. Panya Ali Abdalla
23. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
24. Mhe. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria

Waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
2. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
3. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
4. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
5. Mhe. Hamad Masoud Hamad

Mhe. Spika, kwanza kabisa tunaishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa ushauri na miongozo yao mizuri. Pia tunamshukuru Makamo Mwenyekiti kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa na kuipongeza wizara kwa kazi nzuri tunayoifanya. Pongezi hizi zimetokana na michango yao waliyoitoa katika kipindi hiki kifupi ili kufanikisha shughuli na majukumu ya wizara, shughuli hizo ni pamoja na kukamilika kwa rasimu ya sera ya hifadhi ya jamii, kupambana na kutokomeza vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, kukamilika kwa rasimu ya sheria ya Mahkama ya Kazi, kutafuta mbinu za kumaliza deni la fidia linaloikabili wizara.

Mhe. Spika, Mhe. Hassan Mohamed Omar akijumuika na Mhe. Farida Amour Mohamed, Mhe. Asha Bakari Makame na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa walitaka kujua ni jinsi gani wizara itaweka mikakati ya kupambana na suala la omba omba ambalo linatia aibu katika nchi yetu na hapo zamani lilikuwa halipo. Lakini mimi nasema tangu utoto nakumbuka kwamba suala hili lilikuwepo lakini halikuja juu sana, sasa hivi ndio limenawiri zaidi.

Wizara itazingatia suala la omba omba katika sera na programu za hifadhi ya jamii. Pia tutachukua ushauri wao wa kuanzisha *program* tofauti ili kupambana na tatizo hili.

Mhe. Spika, kwa nasaha za Mhe. Asha Bakari Makame naomba niseme kabisa yeye alitaka wanawake tukae kwa pamoja tuzingatie na tulizungumzie sana suala la ubakaji. Suala hilo nakubaliana naye na

tutashirikiana na wanawake wote wa Baraza hili nitawashirikisha kikamilifu ili tulizungumze tuliwekee mikakati zaidi.

Mhe. Spika, nikiendelea na kamati na Mhe. Farida Amour kuhusu sehemu za kufanyia kazi Mabaraza ya Watoto. Wizara kwa kushirikiana na Masheha tunaangalia uwezekano wa kupata maeneo muafaka ili Mabaraza ya Watoto yaweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kuhusu kasma maalum kwa mabaraza hayo kuweza kufanya kazi zao. Wizara itatumia bajeti yake iliyopangiwa kuweza kusaidia kuendesha shughuli za Mabaraza hayo ili watoto waachane kabisa na kuchangia katika mifuko yao kuwachangia watoto wenzao. Suala hili litafanyiwa kazi kwa uadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, napenda kuijibu kamati na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa kuhusu suala la fidia. Wizara inafanya mashirikiano na Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo juu ya namna ya kulipunguza deni la fidia. Kwa mwaka huu jumla ya shilingi 50 milioni zimetengwa kwa ajili ya fidia, yaani 30 tulipe Unguja na 20 tulipe Pemba. Mhe. Spika, si hatua ndogo hiyo, tunadaiwa sana lakini tumejikaza.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mohamed Haji Khalid, Mhe. Suleiman Hemed na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kuhusu suala lao la kuwalinda watoto katika mazingira ya elimu dhidi ya udhalilishaji. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inashirikiana sana na Wizara ya Ustawi wa Jamii kwa kuwandaa sera ya kumlinda mtoto katika mazingira ya taaluma. Wizara pia imeandaa mkakati wa mawasiliano juu ya kuelimisha jamii kwa kutumia vyombo vya habari, athari za udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa jamii. Aidha, tuna mpango wa kutumia viongozi wa dini ambao wamekubali na wamekula kiapo kwamba wao suala hili hawatalifanya hata siku moja na kamati za kupinga udhalilishaji wa kijinsia za shehia katika kuelimisha jamii juu ya mapambano hayo.

Mhe. Spika, napenda kuijibu kamati kuhusu ushirikishwaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Ofisi Kuu Pemba, kwamba wizara inashirikiana vizuri katika kutekeleza miradi yake yote ya maendeleo, shughuli zote zinazotekelezwa Makao Makuu pia huwa zinatekelezwa Ofisi Kuu Pemba. Pia shughuli zote za miradi zinazotekelezwa na idara Unguja pia zinatekelezwa Ofisi Kuu Pemba. Pia Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa kusema kwamba nampongeza sana Afisa Mdhamini aliyeko Pemba kwa jitihada na kazi nzuri anayoifanya. Kwa kweli nimeridhika naye.

Kwa niaba ya wizara napenda kuishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa michango yao na tunaahidi kwamba tutatekeleza yale yote ambayo wametushauri kwa ajili ya kukuza ufanisi wa shughuli zetu na tutashirikiana na kamati bega kwa bega kama tulivyokuwa tumeshirikiana na kamati iliyopita na hii iliyopo sasa hivi tutashirikiana nayo.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mahmoud Mohamed kuhusu suala la majukumu ya Idara ya Vijana yanajirejea rejea kila mwaka kwa nini? Idara hii Mhe. Spika, ina jukumu la kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana na masuala haya ni endelevu yanayohitaji kusimamiwa na kutekelezwa mwaka hadi mwaka hadi tumalize kipindi chetu hiki cha miaka mitano. Yako malengo ambayo hayawezi kumalizika kwa mwaka mmoja yanahitaji kuendelezwa na ndio maana ikawa tunayaleta hapa kila mara. Lakini mwisho naomba nimwambie Mhe. Mahmoud kama tulivyokubaliana kwamba tukimaliza bajeti yetu hii tukutane katika jimbo lake, niko tayari sina wasi wasi wowote tutafanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Spika, kuhusu fungu 220401 limeongezeka kutokana na mahitaji ya Baraza la Vijana kwa nini? Sekretarieti ya Baraza itatumia fungu hili baada ya kuanzishwa. Aidha, kilimo cha *Rossela* Tunguu tumetakiwa kuwapatia gari na mafuta ya jenereta na kuratibu shughuli za ufuatiliaji katika maeneo yote litatumika fungu hili na ndio maana likawa kubwa.

Kuhusu suala la kesi za ubakaji kwamba mwanzo zinatajwa lakini baadae hazijulikani zinaishia wapi. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa maelezo aliyoyatoa. Mchango wake nadhani umenisaidia sana, kesi hizi huwa zinapelekwa katika vyombo vya sheria ili ziweze kupewa hukumu zinazostahiki. Zikishapelekwa katika vyombo vya sheria wizara inasikitishwa sana kuona kesi hizi hazihukumiwi. Lakini nadhani kutokana na utaratibu ambao tumeuanzisha sasa hivi tukishirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Afya kama alivyoeleza Waziri wa Katiba na Sheria huenda tukafanikiwa *Inshaallah.*

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mamoud kwamba ni kweli wake wa viongozi wanatoa misaada mbali mbali kwa vikundi vya wanawake. Hivyo napenda kumshukuru Mama Mwanamwema Shein, Mama Awena na Mama Asha Balozi kwa jitihada zao wanazozifanya katika kusaidia maendeleo ya wanawake. Lakini vikundi tulivyovitaja Mhe. Spika, katika hotuba ya bajeti ni vile tu vilivyosaidiwa kutokana na juhudi za wizara, ndio maana ikawa haya mengine hatukuyataja. Hizi ni

jitihada zao hawa akinamama na naomba tuungane tuwapongeze sana na tuwape hongera nyingi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Mhe. Ali Salum la uanzishwaji wa Mahkama maalum za kushughulikia kesi za udhalilishaji wa kijinsia, hili ni azimio lililotolewa katika mkutano wa nchi za Maziwa Makuu ambapo wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba kama alivyozungumza mwenzangu ipo katika hatua ya kuanzishwa mahkama hizo ili kuweza kuharakisha utoaji wa hukumu wa kesi za udhalilishaji. Inavyotakiwa baada ya miezi sita kesi ziwe zimeshamalizika.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Ali Salum, Mhe. Mohamed Mbwana na Mhe. Mohamed Haji Khalid waliotaka kujua wizara ina mkakati gani wa kuwasaidia wazee mbali na kuwapa milo mitatu kama tunavyowapa sasa hivi. Wizara kupitia sera ya hifadhi ya jamii inakusudia kuweka utaratibu wa kuwasaidia wazee wote na kuanzishwa mpango wa pencheni jamii kwa wazee. Hivi sasa wizara inaendelea na kufanya zoezi la kuwatambua wazee wote na kujua mahitaji yao.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Ali Salum aliyetaka kujua ikiwa mikopo inayotolewa inawasaidia vijana wetu na kinachotolewa kinatosha kuanzisha miradi. Wizara inafuatilia wale wote waliyoomba mikopo na kuangalia mahitaji ya maombi na uwezekano wa marejesho.

Mhe. Spika, viko vikundi ambavyo mahitaji yao ni madogo. Hata hivyo, wizara imefanya tathmini ya vikundi vya uzalishaji kujua mahitaji yao halisi ili vile ambavyo mahitaji yao yataweza kusaidiwa na Mfuko wa Vijana vihudumiwe na Mfuko huo, na ambapo mahitaji yao ni makubwa wataelekezwa katika Mfuko wa Uwezeshaji. Hakuna kikundi cha watu 30 waliopewa shilingi milioni mbili, utaratibu wa Mfuko wa Vijana ni vikundi vya watu watano watano.

Mhe. Spika, nataka pia niseme kwamba, nakumbuka msemo wa Marehemu Mzee Karume aliosema, “Ni afadhali tuwe na kitu kidogo lakini tugawane kidogo kidogo, kuliko kuwa na kitu kingi tukaanza kukigombea”. Sasa hawa vijana wetu haidhuru tuna kitu kidogo lakini na wao wapate wengi, kwa sababu tukiwapa kidogo wengine watavunjika moyo, kwa hivyo tunatoa kwa kadri ya uwezo wetu.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Marina Joel juu ya mikakati inayotumika kwa urejeshaji wa fedha za mikopo. Naomba kumuarifu Mhe. Marina pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwamba Mfuko wa Vijana unaendelea vizuri na marejesho ya mikopo

yanaendelea vizuri, vijana wanalipa hawana wasi wasi wowote na sisi tunawafuatilia nyendo zao na kuona kazi zao.

Vile vile napenda kumjibu Mhe. Ali Salum na Mhe. Haji Khalid kwamba wizara inafahamu tatizo la ajira linalowakabili vijana, hivyo inajipangia kuhamasisha vijana kubadili mtazamo wao juu ya dhana ya ajira na kuelekeza katika kujiajiri wenyewe. Aidha, kuna mpango mkubwa ambao umeanzishwa na serikali wa kutatua tatizo la ajira kwa vijana maana sisi hatuna uwezo wa kuajiri vijana, unaoratibiwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Makame Mshimba alipokuwa akichangia Mhe. Spika, alisema haya mambo ya ajira, pesa za zakka na nini zote tupewe sisi wanawake na watoto, lakini sasa sidhani kama mwenzetu atakubali angalau tunaomba atugaiye fungu tu kidogo.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mohamed Haji Khalid na Mhe. Wanu Hafidh Ameir waliotaka kujua mikakati inayofanywa ili kupambana na mporomoko wa maadili unayoikumba Zanzibar.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tusibabaike, tutaifanyia *editing* maana kuna majina mengine sina wajumbe hao humu. Kwa hiyo tutaifanyia *editing* baadae kuthibitisha yale majina iwe yanakwenda kila mmoja kwa mujibu wa majina niliyonayo ndani ya ukumbi huu. Kwa hivyo, tumuwie radhi kidogo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunisaidia. Hili ni jukumu la kila mmoja wetu kuhakikisha malezi bora kwa watoto wetu, tuwe karibu na watoto wetu, tuwapende watoto, tuwatunze vizuri lakini pia wizara imepokea ushauri wake na hivi sasa imejipanga kutoa elimu ya *study* za maisha kwa vijana ili waweze kujitambua na kuwa na tabia njema.

Kuhusu kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji katika mpango mkuu wa ajira kwa vijana wizara imeshafanya vikao mbali mbali vya mashirikiano kuhusu mpango huo. Pia tumeshirikiana katika uanzishwaji wa soko la Jumapili Pemba na tunaendelea kuratibu kwa pamoja uendelezwaji wa soko hilo. Nawapongeza sana wanawake wa Pemba kwa namna wanavyolitumia soko lao la Jumapili. Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Farida Amour kwamba suala hili tunaendelea kulifanyia kazi kwa hali na mali na kwa uzito unaostahiki.

Mhe. Spika, Mhe. Rais alishughulikia suala la udhalilishaji nchini, mbali ya jitihada zinazochukuliwa na wizara, Mhe. Rais analifuatilia kwa kina suala hili. Mhe. Rais aliunda kamati maalum ya mawaziri kama alivyozungumza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria; kuangalia ukubwa wa tatizo hili kwa kuangalia tafiti zake zilizofanywa. Kamati hii ilipendekeza kufanyika utafiti wa kuangalia ukubwa wa tatizo na hatua zinazochukuliwa katika kupambana na udhalilishaji. Wizara hivi sasa ipo katika hatua ya mwisho ya kukamilisha utafiti wa mambo ya udhalilishaji.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Farida Amour kuhusu lini jengo la ofisi Pemba litakuwa tayari ili kupunguza kulipa fedha nyingi kwa ajili ya kukodi ofisi. Suala hili Mhe. Spika, tunalisimamia lakini hasa Waziri wa Fedha. Hali itakapokuwa nzuri Mhe. Spika, tutajenga ofisi lakini kwa hivi sasa siwadanganyi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi bado pesa hatujapata za kujengea ofisi ile na wenzetu wanakuwa na mikakati kule ya kuongeza ongeza bei kwa sababu washajua kwamba hatuna pa kwenda. Kwa hivyo, itabidi hili tulivumilie na mimi naomba mkubaliane na mimi.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Fatma Mbarouk Said suala lake kuhusu uchimbaji wa kisima chengine katika makao ya Wazee Sebleni. Mhe. Fatma nakuomba ukiwa na tatizo lolote kuhusu wizara hii mimi ndio mwenzio usiende ukahangaika kwa watu wa kati kati, lakini tumeshakubaliana mimi na wewe kwamba tukishapitisha mambo yetu ya bajeti tuje tukae mimi na wewe tulizungumze. Mhe. Salmin Awadh pia kakubaliana na mimi kwamba tutakaa kwa pamoja tulipange jambo hili ili watu wote wapate maji. Rais mwenyewe anavyotaka hasa kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji sasa kwa nini sisi twende hivi hivi tu, lazima mambo haya tuyashughulikie kwa kina kwa hivyo usiwe na wasi wasi ndugu yangu tutakuwa pamoja na hili *Inshaallah* kwa sababu ni jambo la kheri Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru Mhe. Fatma pia kwa kuishukuru na kuipongeza wizara kwa juhudi zake za kutayarisha Sera ya Hifadhi ya Jamii, lakini pia napenda kutoa ufafanuzi kuhusu umri wa kutoa pencheni jamii kwa wazee wote. Wizara itakaa na wadau husika ili kukubaliana umri wa kutoa pencheni hiyo, kwani wazee kupewa hifadhi ni haki yao ya msingi.

Mhe. Spika, napenda kujibu tena suala la mhe. Marina Joel kuhusu utoaji wa mafunzo kwa Mabaraza yote ya Shehia ya Watoto. Mpango wa mafunzo kwa Mabaraza ya Watoto ni endelevu na kwamba hata

mwaka huu wa fedha mafunzo kwa Mabaraza ya Watoto yataendelea kama yalivyopangwa kulingana na uwezo wa fedha tulizonazo.

Mhe. Spika, napenda kumjibu suala Mhe. Asha Bakari, Mhe. Panya Ali na Marina Joel kuhusu udhalilishaji. Nashukuru sana kwa maelekezo waliyoyatoa na *Inshaallah* nimeshasema tangu mapema kwamba tutashirikiana ili jambo hili tulishughulikie. Aidha, wizara yangu inaendelea na jitihada za kuandaa mikakati na mipango mahsusi ya kulishughulikia tatizo la udhalilishaji wa watoto kwa kuwapatia haki zao za msingi. Aidha, wizara imeandaa kamati maalum ya Makatibu Wakuu inayokutana kila baada ya miezi mitatu na Kamati ya Mawaziri inayokutana kila baada ya miezi sita kulishughulikia suala hili na kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wa Katiba ameeleza vizuri sana.

Mhe. Spika, naomba kumjibu tena Mhe. Marina suala lake juu ya uundwaji wa Mabaraza ya Watoto. Wizara inaendelea na kazi ya uhamasishaji na ushajihishaji wa uundwaji wa Mabaraza ya Watoto ya Shehia. Hatujapumzika Mhe. Spika, tunaendelea na mabaraza yataendelea kuundwa hadi kufikia ngazi za wilaya na mikoa.

Kuhusu suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mhe. Viwe Khamis Abdalla na Mhe. Wanu Hafidh kuhusu suala la Baraza la Vijana litamalizika lini, na lini litaletwa Barazani. Wizara kwa heshima na taadhima nataka niseme tumehangaika sana na sasa hivi tuko katika hatua ya mwisho, Mswada wa Sheria tunategemea mwezi wa Oktoba tutausoma hapa kwa mara ya kwanza ili muujadili na baadae vijana ikikubalika na ikishapita watapata nafasi ya kuunda Baraza lao la Vijana. Tusiwe na haraka mambo mazuri jamani hayataki haraka.

Nilikuwa namsikia jamaa mmoja hapa akizungumza mambo ya Bara wenzetu mambo ya benki wanatushinda na nini. Lakini kwa taarifa yenu na sisi kuna mambao ambayo tunayafanya wale hawajayafanya, kwa hivyo tusijidharau tujipongeze na sisi.

Mhe. Spika, nikiendelea na Mhe. Jussa suala la kulea watoto kwa mujibu wa utaratibu wa Kiislamu. Ushauri wake mheshimiwa tunauchukua, tunaukubali na tutaufanyia kazi na kuangalia namna ya kuandaa kanuni katika eneo hili la sheria kama alivyopendekeza. Namshukuru alinipongeza sana watu wengine wakasema hee!, kampa zawadi gani. Sijampa zawadi yoyote anaona utendaji wetu.

Kuhusu suala la kutunga kanuni kwa kufuata mila na desturi zetu bila ya kufuata shindikizo la washirika wa maendeleo, hili linazingatiwa kwani baada ya wataalamu kukamilisha zoezi lao, wizara pia kupitia Kamati ya Uongozi hukaa pamoja kupitia na kuangalia kama kanuni zinaendelea kwa kufuata mila na desturi za nchi yetu,

Mhe. Spika, napenda kumjibu tena Mhe. Jussa suala la kuwa na idadi kubwa ya ajira za watoto. Wizara inashirikiana na Wizara ya Kazi ili kusimamia suala hili. Kwa upande wa wizara suala hili linaingia katika masuala ya hifadhi ya watoto na watoto wenye mazingira magumu.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Wanu Hafidh, Mhe. Bi Panya tena, Mhe. Mwanaidi Kassim, Mhe. Ali Salum, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Amin Iddi, Mhe. Kazija Khamis Kona na Mhe. Bikame Yussuf kuhusu suala la kuanzishwa Benki ya Wanawake. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inaendelea na hatua za kuanzisha benki hiyo. Aidha, Rais mwenyewe alitwambia mkiwa tayari wakati wowote jengo kwa ajili ya benki hiyo litakuwa lipo tayari, tatizo linalotukabili ni pesa hatuna shilingi milioni mia sita sijui na ngapi huko utaona wewe ni jambo dogo lakini si dogo, kwa sababu tuna mambo ya kuwahudumia watu. Kwa hivyo, tatizo letu hili la fedha likimalizika tukipata bilioni 5 basi uanzishwaji wa benki hii utakuwa tayari. Lakini hatutaki tuwaite watu kule kutoka Bara kuja huku kutuanzishia benki. Benki tutanzisha sisi wenyewe hapa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Bikame Yussuf Hamad suala lake alitaka kujua kamati za kupinga udhalilishaji wa kijinsia katika Sheria zinaundwa na watu wa namna gani. Kamati za udhalilishaji wa kijinsia zinaundwa kwa kuwajumuisha Masheha, mratibu wa wanawake na watoto, mwalimu, daktari, polisi jamii, watu wa dini na watu wengine wote ambao watasaidia katika jamii. Aidha kamati inajumuisha wanawake na wanaume ili kurahisha utekelezaji wa majukumu ya kamati.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Fatma Mbarouk ambaye anasema wizara inasikitishwa sana na ongezeko la vitendo vya udhalilishaji hasa kwa watoto wa kike na wa kiume. Wizara inaendelea kuchukua jitihada mbali mbali ikiwa ni pamoja na kushirikiana na wadau wakiwemo polisi, mahakama, afya, elimu na wengine. Hata hivyo wizara haina mamlaka ya kutoa hukumu lakini ingelikuwa kama sisi tuna mamlaka ya kutoa hukumu mngeona kazi yetu.

Mhe. Spika, pia nawaomba wananchi kuwacha tabia ya kufumbia macho vitendo hivyo na baada yake kuviripoti katika taasisi husika kwa wakati ili tusipoteze ushahidi. Aidha jamii iache tabia ya kumalizia kesi hizi wenyewe kwa wenyewe majumbani, utaona mtu anasema muoe yatamalizika, aah! basi chukua shilingi laki tano, kwa kweli hili ni tatizo. Vile vile naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kutuunga mkono kupitia majimbo yao katika harakati za kukomesha vitendo hivi, tukifikia kwenye majimbo yetu tuwaambie watu tusikae kimya.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir kwamba ushauri wake wa kuanzisha *Green house* tumeupokea na tutaufanyia kazi. Aidha, kuhusu soko la Rossela lipo. Vile vile suala la maendeleo ya vijana ni la jamii na si la wizara peke yake, nawaomba Waheshimiwa washirikiane na wizara kuleta michango yao ya kuwaendeleza vijana.

Mhe. Spika, naomba pia nimjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alishukuru sana kuhusu suala la Skauti kwa namna tulivyomsaidia. Lakini kwa bahati mbaya mpaka leo hajapata majibu kutoka Wizara ya Elimu. Sasa mimi namuhakikishia Mhe. Makame Mshimba tukimaliza bajeti yetu hii tutakwenda zetu Wizara ya Elimu tukafuatilie na Mhe. Waziri wa Elimu ni mwenzetu hana wasi wasi wowote ili tuone kwamba jambo hili linakubalika.

Lakini pia akasema tufuatane twende wapi huko kwenye mahoteli. Mimi niko tayari kwa sababu yeye mwenyewe Mhe. Makame Mshimba alivyonambia twende Kitope kwa matatizo ya kilimo mimi nilikwenda Kitope muda wa siku tatu tukawa tunafuatana mimi na yeye kushughulikia suala la kilimo hasa kwa wanawake.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub tulikuwa naye katika kamati yetu kipindi kilichopita yeye ni hodari wa kazi, nashukuru Mwenyezi Mungu *alhamdulillah* alitusaidia sana. Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliuliza suala lake kwamba katika utafiti wa udhalilishaji ni maeneo gani yameonekana kwamba kuna udhalilishaji mkubwa. Wizara ipo katika hatua ya kuzifanyia uchunguzi takwimu na kupata matokeo. Namuahidi kwamba pale matokeo yatakapokuwa tayari nitampa taarifa hii ni Wilaya gani inayoongoza kwa vitendo vya udhalilishaji. Lakini kwa ufupi vitendo hivi vimeenea katika wilaya zote, leo utasikia Wilaya gani mtoto kabakwa, hata hivyo taarifa nitampatia rasmi Mhe. Jaku Hashim Ayoub na pamoja na Waheshimiwa wote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, napenda kumjibu tena Mhe. Makame Mshimba kuhusu suala la Mkimbiza Mwenge halina ubaguzi, wizara inatangaza katika vyombo vya habari kuwataka wenye sifa waombe na waliotimiza masharti wanafanyiwa usaili na wanaofaulu wanachukuliwa kwa shughuli za kukimbiza mwenge. Hatuna ubaguzi wowote anayefeli ndio kafeli, mwenye riski yake anapata.

Mhe. Spika, naomba kumjibu tena Mhe. Bikame Yussuf Hamad kwa kuwa kuna mrundikano mkubwa wa vikundi vya vijana na je, vikundi hivyo vinapata mafanikio. Suala la vijana kujiunga pamoja ni la msingi kwani linarahisisha ufikwaji wa vijana wengi kwa muda mfupi, vikundi vinafanikiwa kupata maelekezo ya mafunzo kwa kuendeleza na kuunganishwa na fursa mbali mbali zikiwemo za mikopo. Kwa hivyo matokeo yake ni mazuri.

Mhe. Spika, napenda kumjibu tena Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Jaku Hashim walioiuliza kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Wizara imetenga fedha maalum za mradi wa maendelo kwa ajili ya kuanza kutoa misaada kwa hao wanaotambuliwa pamoja na familia zao.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Asha Abdu Haji swali lake la uzio katika makao ya wazee Welezo. Wizara imeliingiza suala la uzio kwa makao haya katika bajeti hii tunayoijadili hapa jumla la shilingi milioni 300 zimetengwa kukamilisha suala hili la kujenga uzio Welezo.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Salma Bilal swali lake kuhusu kuwahudumia wazee. Wizara inakuhakikishia kwamba inashughulikia wazee wote wa mijini na vijijini kwa sababu wazee walioko Sebleni ni wazee wa Wilaya zote za Unguja na Pemba. Lakini inategemea uwezo wa wizara katika kuwahudumia wazee. Hapa ninachotaka kusema Waheshimiwa nawaomba tuwaambie watu wetu vijijini waliotuchangua kuwashughulikia na kuwapenda na kuwasaidia wazee wetu, sisi tumezaliwa tukanyonyoshwa, tukawekwa vizuri mpaka tukawa watu wazima, wazee walipata shida sana. Kwa hivyo, tuwalee tusiisubiri Serikali tu, Serikali ina sehemu yake lakini na sisi tuliozaliwa tuna sehemu yetu. Sasa kwa wale waliokuwa hawana watoto kabisa hao ndio tunachukua jitihada za kuwaweka pahala wakatulia kama wale walioko Welezo, Sembleni, Limbani na kadhalika.

Napenda sasa kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija aliyetaka kujua kwa nini mara hii hatukuleta kitabu hapa cha Mtoto wa Muafrika. Mhe. Hija

Hassan Hija pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine ni kweli mara hii hatukuleta hichi kitabu kwa sababu kulitokea matatizo ambayo kwa vyovyote mimi mwenyewe kama ni Mwakilishi mwenzenu nikaona kwamba tukiileta taarifa vile ilivyo, kwa kweli itakuwa sisi si watu wa kawaida. Lakini kwa bahati nzuri sasa suala lile bado tunalishughulikia na ikiwa tayari tutalileta hapa hapa Mhe. Hija Hassa Hija.

Pia napenda kumjibu vile vile Mhe. Hija Hassan Hija suala lake alitaka kujua madawati ya kijinsia yako chini ya dhamana ya nani. Ni kweli kuwa wizara ilichangia katika uanzishwaji wa madawati ya kijinsia katika wizara mbali mbali na maafisa wanaoshughulikia masuala ya jinsia wapo. Jukumu lao kubwa ni kuhakikisha kuwa taasisi zao zinazingatia masuala ya kujinsia hususan mahitaji na changamoto zinazowakabili wanawake na wanaume zinafanyiwa kazi katika sera na mipango na taasisi zao. Madawati haya yako chini ya Wizara husika na maafisa jinsia wanaozifanyia kazi wizara zao. Hivyo jukumu la kuwezesha madawati hayo linakuwa chini ya Wizara au taasisi husika sio Wizara ya Ustawi wa Jamii tu.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Salma Mohamed Ali kuhusu suala lake la vipindi vya kuelimisha wanawake juu ya haki zao. Wizara inaendelea kuwaelimisha wanawake juu ya haki zao kupitia *television*, *radio*, magazeti na hata mikutano tukipata nafasi sisi tunakwenda tunawambia wanawake wajikaze ili wajue haki zao wasikae tu hivi hivi wakadanganywa wakaona basi ndio tumefikia muafaka. Lazima wajue haki zao tunawaelimisha kwa hilo.

Mhe. Spika, napenda tena kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija kuhusu suala la kwa nini nafasi tupu za ajira zilikuwa 16 na zimeajiriwa 12 tu. Wizara imeomba kuajiri nafasi zote 12 lakini kwa bahati mbaya tumefanikiwa kuruhuruhisiwa kuajiri nafasi 10, naomba upokee hizo tulizozipata.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Asha Abdu Haji kuhusu suala la vespa zimegaiwa vipi baina ya Pemba na Unguja ambazo hizi zilikuwa ni vespa 4. Naomba nikwambie kwamba hizi baada ya sisi kumaliza bajeti yetu kila mmoja huwa anawekewa fungu lake. Kwa hivyo, idara mbali mbali zilikubali wenyewe ili wawapatie nafasi watendaji wao wapate vyombo vya kufuatilia mambo. Kwa hivyo, idara mbali mbali zikanunua tuseme mfano Idara ya Wanawake na Watoto, Idara ya Ustawi wa Jamii, mfano ndio huo na nyengine mpaka zikatimia nne, na kule Pemba wakapanga na wao wakanunue vespa yao moja. Kwa hivyo huo ndio utaratibu sio kama tulinunua vespa nne halafu ikesha, vespa

nne zile labda zigaiwe Unguja 2 Pemba 2 sio hivyo nadhani umenielewa.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Salma Mohamed Ali suala lake la kwa nini wafanyakazi waliokwenda likizo ni wengi 138 ukilinganishwa na waliolipwa posho la likizo ni 56. Mhe. Spika, naomba niseme wizara inalipa posho la likizo kulingana na bajeti iliyopewa kwa mwaka. Lakini kila mfanyakazi anapewa pesa za likizo akichukua likizo mwaka huu akae miaka 3 ndio aje kulipwa tena sio kama kila akaenda likizo apate, maana ingekuwa tena ni mchezo watu wote saa zote wako likizo wanasubiri zile pesa zao za likizo. Kwa hivyo, ndio ukaona waliolipwa ni 56 tu, aidha kila mfanyakazi anastahili kulipwa pesa za likizo baada ya miaka 3 kamili.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Salma Mohamed Ali suala lake la kutaka kujua ni vikundi vingapi vya *SACCOS* Pemba zilivyopatiwa msaada ya shilingi milioni 1. Mhe. Spika, ni kikundi kimoja tu ndio kilichopatiwa msaada wa milioni 1 nacho ni kikundi cha Jondeni *SACCOS* na hii milioni 1 kwa taarifa yako niliitoa mimi mfukoni mwangu nikaipeleka Jondeni.

Mhe. Spika, napenda kumjibu tena Mhe. Jaku Hashim suala lake kuhusu watoto wa Micheweni ambao wanajishughulisha na ajira za kubanja kokoto linashughulikiwa vipi. Wizara ikishirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika wanashughulikia suala la kupambana na ajira za watoto ambapo Michweni ikiwa ni moja ya eneo linalofanyiwa kazi. Lakini nakuhakikishieni kwamba kazi hii tuliifanyia kazi tena tukishirikiana na Mhe. Bihindi Hamad Khamis huyo hapo ambaye ni Mwakilishi wa Viti Maalum huko huko Micheweni, kwa hivyo Mhe. Bihindi Hamad Khamis anajua habari hizi. Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mohammed Mbwana Hamad suala lake kuhusu kiwango kikubwa cha malalamiko ya udhalilishaji mengi zaidi katika Wilaya ya Chake-Chake ukilinganisha na Wilaya nyengine Pemba, kwa nini. Kwanza kwa sababu kituo pale kilikuwa ni kimoja. Kwa hivyo na watu wamehamasika walipopata taarifa zile wakawatarifu kutoka Wete, Micheweni, Mkoani, Chake- Chake zote zinarundikana pale. Lakini kwa taarifa yenu Waheshimiwa sasa hivi tunamalizia kutengeneza kituo kilioko Wete na tumeshapata eneo kwa ajili ya kituo cha Micheweni, kwa hivyo kule Pemba tutakuwa tumebakiwa na eneo moja tu la Mkoani bado tunalishughulikia.

Mhe. Spika, naomba pia kumjibu Mhe. Hamad Masoud Hamad wa Jimbo la Ole ambaye ametaka kujua Sheha wa Ole ambaye

alimwagiwa Tindi kali hadi leo hajalipwa fidia yake kwa nini watu wanamuhangaisha. Hatumuhangaishi hatujapata pesa tukipata tu atalipwa lakini suala hili tunalichukua na tutakwenda kulifanyia kazi Mhe. Hamad Masoud Hamad, usione kama tunalipuuza

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mohammed Mbwana suala lake linalosema ni lini Ofisa Jinsia wa Wizara Pemba atajiriwa. Ofisa wa Jinsi wa wizara yupo lakini kwa hivi sasa yuko masomoni Tanzania Bara yaani tumekwenda kumsuka zaidi ili akirudi afanye kazi zake vizuri.

Kwanza Mhe. Spika, napenda niseme kwamba nimejitahidi kujibu lakini kwa yeyote kama ikiwa sikumjibu, naomba radhi sana sikuweza kumaliza yote. Hata hivyo naomba tu wanivumilie na *inshaallah* kama yeyote sikumjibu tukutane tuambiane ili tufanye kazi kwa pamoja.

Hitimisho

Kwa niaba ya Wizara na watendaji wake wote napenda kukushukuru Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Spika, nyote pamoja na watendaji wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano mazuri wanayonipa kwa kipindi chote cha kuwasilisha hotuba yangu.

Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana na Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Aidha napenda kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia hotuba yangu kwa njia tofauti michango yao naithamini naipenda na nitaifanyia kazi. Nayo ilikuwa ni mizuri watu wote wameunga mkono hoja.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba ba Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spka: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikoni, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kufikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 28 - WIZARA YA USTAWI WA JAMII MAENDELEO YA VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu 0301 - Ofisi kuu Pemba 347,617,000/=
Kifungu 0401- Idara ya Mipango na Utafiti

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nataka kumtoa wasi wasi Waziri mwenye wizara hii kuwa sina mashaka naye. Lakini mtu hata akikukosa jua anakutakia mema na mtu hata akikusifu mia juu ya mia uko safi basi huko safi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia mwaka jana kuna kesi 127 zilizofunguliwa na kesi 66 tu zilizosikilizwa na kati ya hizo 3 ndio zilizopata hukumu. Je, wizara imechukua hatua gani kwa sababu hili suala linazidi kuendelea na litazidia kuendelea kama wizara haiko *serious*.

Mhe. Waziri wa Katiba ba Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kesi za mwaka jana ni nyingi. Lakini kama nilivyosema mwanzo hapa kwamba hizi sasa zote ziko chini ya *criminal case* na *criminal case* zina utaratibu wake sote tunajua na yote hii ni msururu wa kushughulikia kesi yaani kesi zinachukua muda.

Kutokana na haya ndio kile kikao nilichokitaja cha Maziwa Makuu nilisema lazima kuwe na utaratibu ambao ushahidi utakuwa umepungua watu siku zote watawekwa ndani, hakuna mtu kutolewa ndani, kutakuwa na kesi kuanzia mwanzo inapokamatwa kesi mpaka kutolewa hukumu isizidi miezi sita, na huo utaratibu huu ambao tunafanya tumeshakaa vikao vingi tu vya kutizama utaratibu huo na tujaribu sasa kutayarisha sheria ambayo inaweza ikapunguza haya.

Kwa hivyo, ni kweli alivyosema Mhe. Jaku Hashim kwamba kesi ziko nyingi na naamini tukimaliza haya basi kesi hizi zote zitapungua sana kutokana na utaribu mpya ambao tumekubaliana, si hapa Zanzibar tu lakini kwa nchi zote za Maziwa Makuu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa bahati mbaya Mhe. Jaku Hashim wakati wa majuisho haya ulipokuwa ukiyatoa hayupo na ndio maana akauliza suala hili na kama alikuwepo naamini asingeuliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kauli ya mkubwa inakuwa haipingwi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kufahamu hivi sasa wanasheria walioajiriwa kwa wizara hii kwa Unguja ni wangapi na Pemba wangapi.

Mhe. Waziri wa Katiba ba Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ninavyojua mimi kila wizara inakuwa na wanasheria wake. Lakini tutakumbuka sote kwamba hivi karibuni tulipitisha sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.
Kwa hivyo, wanasheria wote wa Serikali watakuwa chini ya utaratibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hata kama wizara haina wanasheria basi bado Mwanasheria Mkuu atawajibika na wizara hiyo. Kwa hivyo, tunao wanasheria wengi tu wa kufanya shughuli.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi nataka anieleze tu Unguja ni wangapi na Pemba ni wangapi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hili suala hebu tuliwache. Tuendelee
Kifungu 0401- Idara ya Mipango na Utafiti

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na mimi pia sina tatizo sana na Mhe. Waziri. Lakini nilihoji suala la kutoletwa Ripoti ya Mtoto mwaka huu. Mhe. Waziri alikiri kwamba haikuletwa kwamba kuna matatizo fulani na sisi ndio Wawakilishi ambao tunataka kumsaidia yeye kama tatizo lilimkwanza na likasababisha Ripoti ya Mtoto isiletwe labda atwambie ili tupate kumkwamua kwa sababu tulizoea Ripoti ya Mtoto tunajadiliana tunampa baraka.

Mhe. Mwenyekiti: Labda hili nisaidie na mimi kwa sababu hii taarifa ililetwa na ikawa ni juu yetu kuiwekea utaratibu na ikaweza kuwasilishwa. Pamoja na yale Mhe. Waziri aliyasema kwamba kuna mambo yamejitokeza lakini kimsingi taarifa hii ililetwa na tuipangie muda. Shida na tatizo inakuja ratiba yetu namna jinsi inavyovurugika, sasa kupanga muda ule inakuwa kidogo ni jambo gumu. Ni juu yetu sisi. Kwa kweli ni jukumu langu kutafuta muda ambao muafaka jambo hili tuliweke.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa ufafanuzi huo na kwa sababu ni matatizo ya kiufundi naomba tuendelee kwa nia safi.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia Ofisi ya Pemba mfanyakazi mmoja wa wazee hana usafiri na katika kuchangia niuliza suala hili lakini katika majibu yake sijayasikia. Zilitolewa vespa na vespa zile nilifikiria labda atanambia kwamba moja kapewa yeye na naona kwamba hakunijibu. Sasa nauliza mfanyakazi yule je, atapata usafiri na ikiwa hajapa atapata lini.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niendelee kutoa maelezo kwamba inawezekana Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii hakupanga kwa wakati ule kununua vespa. Sasa waliopanga kununua vespa kwa ajili ya wafanyakazi wao ndio zikanunuliwa vespa hizi.

Sasa ikifika wakati Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii akiona sasa tayari kununua vespa atanunua na tutampa yule mfanyakazi wake pale anayeshughulikia wazee, sidhani kama hilo litakuwa suala kubwa. Hata hivyo lakini kwa sasa hivi kweli walikuwa hawajanunua.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, namuuliza katika hilo fungu vespa hiyo ya mfanyakazi haimo. Kwa sababu nilipokuwa katika kamati tulikuwa kila tukienda sehemu ile anatusitikia kuhusu usafiri.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, vespa hiyo ndani ya Idara hii ya Ustawi wa Jamii ilikuwa haimo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Abdu Haji kwenye fungu hilo hamkuwa na suala la vespa.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, sasa namuuliza Mhe. Waziri atamfanyia maarifa ili kumpatia usafiri mfanyakazi yule.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, tukipata pesa tu tutamfanyia utaratibu na yeye apate vespa ili kumpunguzia matatizo.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Lakini pesa ndio tunapitisha na yeye hayumo katika bajeti sijui vipi tena. Lakini tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hapo wacha nisaidie. Unajua wakati mwengine wizara huwa ina maarifa, inapotokezea kwamba kuna jambo

muhimu sana litekelezwe, wanayo maarifa ya utaratibu hata kufanya *re-allocation*, kwa sababu ya uzito wa lile jambo. Kwa hivyo, kweli kwenye bajeti halimo, jibu lake kwa urahisi lingehusu labda lizingatiwe mwakani, lakini kwa maneno yake aliyosema Mhe. Waziri pale, maana yake wanaweza kutafuta maarifa ili jambo hili kuweza kulizingatia. Nadhani tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 318,446,000

Kifungu 0501 Idara ya Wanawake na Watoto

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Mhe. Mwenyekiti, nilivyochangia kuhusu Mahakama ya Watoto na nilimsikiliza vizuri Mhe. Abubakar Khamis Bakary wakati akitoa ufafanuzi, akizungumzia kuhusu ile *system* ya kumsikiliza mtoto wakati anatoa ushahidi katika vyumba viwili tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara ya mwisho Kamati ya Katiba na Sheria ilipokwenda pale, ile *system* ilikuwa haifanyikazi kwa sababu kulikuwa kuna kifaa kimoja cha sauti ambacho ingewezesha kusikilizana kilikuwa hakipo. Lakini Mhe. Abubakar Khamis alipokuwa anatoa ufafanuzi, alisema kuwa ile *system* tayari inafanyakazi. Sasa nilikuwa nataka anihakikishie kwamba inafanyakazi au bado serikali inasuasua kutafuta hiki kifaa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hii Mahakama ya Watoto tulishamaliza na vitu vyote tayari, isipokuwa ile *system* ya sauti ndio bado haipo. Hivi sasa tumeshakuwa tayari kila kitu na tumeshaagizia wakati wowote inaweza kufika, kwa hivyo itakapofika tu Mahakama ya Watoto itaanza kazi rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, tumefanya majaribio na majaribio yote yanakwenda vizuri. Sasa tatizo liliopo ni hii sauti, kwa sababu haiwezi kwenda kule aliko mtoto lakini tumeshaona matatizo hayo na tumeshaagizia. Kwa hivyo wakati wowote kuanzia kipindi hiki hiki tutaipata. Kwa maana hiyo tuna hakika tukijaaliwa tutaanza kazi katika kipindi hiki.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Salma Moh'd Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilimueleza Mhe. Waziri kuwa kuna baadhi ya wazazi, kwa itikadi zao za kidini wanawazuwia watoto wanawake kuwapeleka maskuli na

nilimuomba anieleze atajitahidi vipi kuwasaidia watoto hawa kupata haki yao ya elimu. Mhe. Mwenyekiti, sikupata jawabu.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyokumbuka nilisema kwamba tutashirikiana na Waziri wa Elimu ili jambo hili tulishughulikie. Hata hivyo, namuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba tutapita tukiwaelimisha wazazi wa watoto juu ya umuhimu wa elimu ili watoto wapelekwe skuli wasifanyishwe kazi ngumu kuliko kiasi chao. Nadhani Mhe. Mwenyekiti, hili litawezekana tukishirikiana sote kwa pamoja.

Mhe. Salma Moh'd Ali: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hapa aliponijibu Mhe. Waziri nilikuwepo. Niliuliza maeneo yaliyoathirika zaidi kuhusu ubakaji wa watoto, akaniambia utaratibu wakati wowote atakuja kunijulisha kuwa amelifanyia kazi suala hili. Nafikiri ni sawa sawa Mhe. Mwenyekiti, narudia tena wakati wowote inaweza kuwa kesho au keshokutwa au mwakani au mwaka ujao.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tunapiga kelele jana kuhusu suala la madaktari. Hivi sasa kaangalie magazeti yanazungumza nini kuhusu madaktari kutaka kuelekea Ikulu kumuona Mhe. Rais. Kwa hivyo aniambia tu Mhe. Waziri ni lini atakuja kutujibu.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli thawabu, sehemu zote zimeathirika. Maana yake ubakaji umeenea Pemba na Unguja watoto wanabakwa. Lakini sasa nilichomuomba mimi ili nizunguke nitafute hasa ni nani na nani kwa kupitia vituo vyetu vya *One Stop Centre* na sehemu nyengine kwa Masheha, kwa sababu tunao maafisa wetu katika mawilaya, maafisa wa wanawake na watoto. Kwa hivyo, mule nitakamozunguka ndimo nitakapopata kumwambia kwamba sehemu hii imeathirika zaidi, ndio nikasema nitamletea kwa maandishi Mhe. Jaku Hashim, naomba akubali hilo mzee wangu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mtu anayeombwa katika mwezi mtukufu wa Ramadhani hatakiwi kukataa. Tuendelee.

Kifungu 0501 Idara ya Wanawake na Watoto 220,568,000

Kifungu 0701 Idara ya Maendeleo ya Vijana 272,557,000

Kifungu 1101 Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Naomba Mhe. Waziri asishangae sana akiona tunapiga buti ajue yale mafunzo yake yanafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia nilizungumzia kuhusu suala la Benki ya Wanawake na nimesimama katika Idara ya Ustawi wa Jamii kwa sababu kuleta maendeleo kama haya ni kustawisha jamii. Wakati nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba kwa sababu inaonekana serikali haina fedha ya kuanzisha Benki ya Wanawake kama yetu wanawake kwa Zanzibar. Basi nilimuomba Mhe. Waziri afanye mazungumzo na Mhe. Waziri mwenzake ambaye pia ni mwanamke kama yeye, kuona kwamba wanafungua tawi la benki ile ambayo inatoa huduma kule Tanzania Bara ili iwasaidie wanawake wa huku Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nilimsikiliza Mhe. Waziri wakati anatoa maelekezo yake alisema kwamba hataki kuwaita watu wa Bara kuja kutuanzishia benki huku. Lakini Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ndio ulivyo, *NBC* iko kule lakini huku wana tawi, *CRDB*, *Exim*, *Barcleys* na benki nyengine. Sasa Mhe. Mwenyekiti, aidha tubaki na umaskini wetu na jeuri yetu, ama Mhe. Waziri akubali akafanye mazungumzo na Mhe.Waziri mwenzake mwanamke ili waone kwamba wanawasaidia wanawake wa Kizanzibari kwa kuanzisha tawi la benki kama hili hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye kabisa Mhe. Wanu Hafidh. Kwanza waziri aliyekuwa Bara mimi na yeye damu damu tuko pamoja, tunafanyakazi zetu pamoja, tunasafiri pamoja. Kwa hivyo, mimi nitazungumza naye na *Inshaallah* atanisaidia kunipa ushauri na pengine ikiwezekana anaweza akaja huku akanisaidia. Kwa hivyo, naomba avumilie kidogo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa waziri amekiri kwamba yeye na Mhe.Waziri mwenzake wa Bara ni mambo damu damu. Kwa hivyo, na sisi tunakaa mkao wa kula wanawake ili kuona hii benki inafunguliwa. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 1101 Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja 687,825,000

Kifungu 1102 Idara ya Ustawi wa Jamii Pemba 105,000,000

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Nilipokuwa nikichangia hotuba hii Mhe. Mwenyekiti, niliunga mkono jinsi wizara inavyojitahidi kuondosha udhalilishaji wa jumla wa Wazanzibari. Lakini nilimkumbusha kwamba wizara hii pamoja na kwamba inaongozwa na mwanamke, lakini sio ya wanawake peke yao inahisi jamii kwa jumla, kwa maana ya wanaume na vijana. Sasa tumekuwa tukizoea kuona kwamba wizara hii inaleta kesi za wanawake kudhalilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atuambie ni lini atafanya juhudi maalum ya kuwatafuta wanaume wanaodhalilishwa majumbani na wanawake ili kuwa na takwimu sahihi. Kwa sababu utafiti unaonesha kuwa kuna wanaume wanateswa sana majumbani, wanapigwa, wanakataliwa na talaka zinatoka nje ya utaratibu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atafanya nini ili kuweza kusaidia takwimu kuwagundua wale kina ngalawa wa Kiwani kuwatafuta na kuwajua ili kuwasaidia angalau kwa ushauri nasaha.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mimi Mhe. Mwenyekiti, nikiwa nimemfahamu vizuri Mhe. Mjumbe nataka nimwambie hivi, tusibaguane kiasi hicho. Kwa vyovyote penye mwanamke na mwanamme tupo tunashirikiana nao wenzetu. Inategemea na elimu Mhe. Mwenyekiti, pengine inawezekana wapo wanawake ambao hawakusoma zaidi kuliko wale wanaume, kwa hivyo tunakwenda nao.

Mimi nakumbuka ilivyoanzishwa wizara hii kulikuwa na Katibu Mkuu mwanamme, alikuwa akisema kwa niaba ya wanawake wenzangu, maana yake na yeye yumo katika kundi la wanawake. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nakuomba tutakwenda kwa utaratibu mwisho pengine tutachukua asilimia kubwa iwe ni wanawake, kama nimemfahamu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo na idadi ya wafanyakazi kuwa ni wanawake. Hofu yangu ni kwamba kuna wanaume wengi sana wanateswa sana na wanawake, kuna wanaume wengi sana katika vijiji vyetu wanateswa na kupigwa sana na kuumizwa.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki niseme jambo, lakini humu ndani kuna wanaume wameteswa sana na wanawake, kwa sababu sisi ni viongozi

hatusemi kwa sababu itakuwa ni aibu. Lakini wizara hii ndio itusaidie sasa kuwadhibiti wanawake wanaowatesa waume zao ili ile haki ya mke na mume ipatikane.

Mhe. Mwenyekiti: Je, Mhe. Waziri utatoa taaluma gani kwa wanawake wanaowatesa wanaume?

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, sio aghalabu wanawake kuwatesa wanaume. Lakini inatokea wakati mwengine wanawake hujitetea nao, mambo yanakuwa makubwa, inabidi mwanamke ajitetee anachukua chuma anampiga mwanamme angalau alegee kidogo. *(Makofi/Vichoko).*

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya wanaume wakishapata kisago hawaripoti wao, wanaoripoti ni wanawake. Kwa hivyo, nawaambia sasa wanaume nao wakipata tabu waje wizara ya ustawi wa jamii. *(Makofi/Vicheko)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri anasemaje, tusiwe tunagugumia, tunaumia umia twende wizara ya ustawi wa jamii.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri ametoa ujumbe kitaalamu. Kwa hivyo, nishauri tu kwamba wale wanaume wanaoteswa waende huko wizarani ili wapate ushauri nasaha wa wizara. Ahsante, tuendelee.

Kifungu 1201	Idara ya Utumishi na Utawala	588,977,000
	Jumla ya Fungu	**2,541,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 28 - WIZARA YA USTAWI WA JAMII NA MAENDELEO YA VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	401,200,000
Kifungu 0501	Idara ya Wanawake na Watoto	958,800,000
Kifungu 1101	Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja	520,000,000
	Jumla ya Fungu	**1,880,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko yoyote. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo, ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio hayo ya Wizara hii ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, sasa wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa liingie katika Kamati ya Matumizi ili niweze kutoa maelezo kuhusu malengo yaliyomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, hotuba yangu itakwenda kwa mujibu wa kifungu cha 96(2), yaani sitosoma hii hotuba yote iliomo kwenye kitabu badala yake nitatoa taarifa kwa muhutasari. Kwa hivyo, nadhani wajumbe watafuatilia kile kitabu na waweze kujua wapi nimeparuka na wapi pako.

Mhe. Spika, pia naomba hotuba yangu kitabu ichapishwe kwenye Hansard, iwemo katika Hansard kitabu chote vile vile.

Mhe. Spika, kabla ya hapo naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia afya njema na uzima na kwa

kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu, kuwasilisha hotuba ya Wizara hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara ninayoiongoza, napenda kuchukua nafasi hii adhimu, kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dokta Ali Mohamed Shein na washauri wake wakuu, yaani Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa ufuatiliaji makini wa utendaji wa Serikali anayoiongoza, uliopelekea kufanya mabadilikokwa safu za watendaji wakuu wa mawizara na taasisi mbali mbali. Ni imani yangu kuwa amefanya hivyo kwa lengo la kutafuta ufanisi zaidi katika kuwapatia wananchi wa Zanzibar huduma bora katika kipindi husika.

Mhe. Spika, wizara yangu ni moja wapo kati ya wizara zilizofanyiwa mabadiliko hayo, naomba nimuahidi tena Mhesimiwa Rais na kuliahidi Baraza Lako tukufu kuwa nitashirikiana nao kadri ya uwezo wangu katika kukabiliana na changamoto zilizopo ndani ya wizara hii na kuhakikisha kuwa Dira na Malengo ya Wizara hii na Serikali kwa ujumla wake yanafikiwa kwa ufanisi. *Inshalla* Mwenyezi Mungu anisaidie, pamoja na watendaji wote wa Wizara yangu (AMIN).

Mhe. Spika, napenda vile vile kutumia nafasi hii kuwapongeza wenyeviti wapya wa kamati za kudumu za Baraza hili na wajumbe wao, ni imani yetu kuwa tutakuwa na mashirikiano mazuri na watazishauri wizara ipasavyo kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi katika kuwahudumia wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, Wizara yangu imeundwa na Idara nane (8), Mamlaka mbili (2), Shirika moja (1), Mahakama (1), Afisi ya Mrajisi (1), Bodi nne (4) na Afisi Kuu Pemba. Asasi hizo ni kama zifuatazo:-

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
ii. Idara ya Utumishi na Uendeshaji,
iii. Idara ya Ardhi na Usajili,
iv. Idara ya Mipango Miji na Vijiji,
v. Idara ya Upimaji na Ramani,
vi. Idara ya ujenzi,
vii. Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi,
viii. Idara ya Nishati na Madini,
ix. Mamlaka ya Mji Mkongwe,
x. Mamlaka ya Maji,
xi. Shirika la Umeme,
xii. Mahakama ya Ardhi,

xiii. Afisi ya Mrajis wa Ardhi,
xiv. Bodi ya Kusajili Wasanifu, Wahandisina Wakadiriaji Majengo,
xv. Bodi ya kusajili Wakandarasi,
xvi. Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba,
xvii. Bodi ya Uhaulishaji Ardhi na
xviii. Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, katika upangaji na utekelezaji wa malengo, kazi na shughuli za wizara, msisitizo umewekwa kwa kuangalia Sera na Mipango Mikuu ya Taifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, MKUZA II, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2010 - 2015 pamoja na Sera za kisekta na Mpango Mkakati wa Wizara.

Mapato na Matumizi

Mhe. Spika, suala la ukusanyaji wa mapato ni kigezo muhimu sana katika kupima mafanikio ya utekelezaji. Wizara yangu katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 4,092,000,000 kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato ya taasisi zake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2013 jumla ya **Tsh** 1,979,365,755 zimekusanywa**.** Kiwango hiki ni sawa na asilimia 48.37ya Makadirio**.** Kwa ufafanuzi zaidi angalia Kiambatanisho **"A"**

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya Mwaka wa Fedha 2012/2013, Bajeti ya Wizara yangu ilikuwa ni Tsh 80,082,728,000. Kazi za kawaida zilipangiwa Tsh 6,708,000,000 na kazi za maendeleo zilipangiwa Tsh 73,374,728,000 ambapoTsh 5,301,928,000 mchango wa Serikali na Tsh 68,072,800,000 mchango wa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2013 Wizara yangu ilikwishapatiwa Tsh 4,411,468,563 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 65.76 na Tsh 106,102,067,000 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 144, ambapo kwa upande wa mchango wa serikali tumepatiwa Tsh 2,866,611,000 sawa na asilimia 54 na mchango wa wahisani ni Tsh 103,235,456,000 sawa na asilimia 151.65. Hivyo kufanya jumla ya Fedha zote zilizoingizwa kuwa ni Tsh 110,513,535,563 sawa na asilimia 137.99 ya makisio yote
Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho "B1, B2 na B3"

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2012/2013 NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, baada ya kukamilisha muhtasari huu wa mapato na matumizi ya wizara yangu, sasa naomba uniruhusu kuelezea kwa kina utekelezaji wa kazi za kawaida na za maendeleo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2012/2013 na malengo ya Mwaka wa Fedha 2013/2014 kupitia kila taasisi zilizomo ndani ya Wizara hii.

IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, Idara hii inawajibika kusimamia na kuratibu kazi zote za kawaida na za maendeleo za Wizara. Kazi za maendeleo zinajumuisha ufuatiliaji na tathmini (*Monitoring and Evaluation*) ya Miradi ya Wizara, ambapo miradi iliyosimamiwa na Idara hii ni pamoja na hii ifuatayo:

i. Usambazaji Maji Vijijini
ii. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
iii. Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)
iv. Maji na Usafi wa Mazingira. (AFDB)
v. Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharabi na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (ADF12)
vi. Uimarishaji wa Mji wa Zanzibar (ZUSP)
vii. Usambazaji Umeme Vijijini.
viii. Kuweka Njia ya Pili ya Umeme Ubungo hadi Mtoni (MCC)
ix. Kufunga Mita 50, 000 za TUKUZA Unguja na Pemba
x. Uhuishaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme kwa Unguja (JICA)
xi. Utekelezaji wa Sera ya Nishati.
xii. Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira (SMOLE II)
xiii. Utafiti wa Nishati Mbadala
xiv. Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Mpapa
xv. Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari Mizingani

xvi. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

Mhe. Spika, Idara imeratibu na kuendesha vikao 12 vya Kamati Tendaji na vikao 4 vya Kamati ya Uongozi ya Wizara kwa mujibu wa Kanuni. Aidha, Idara kwa kushirikiana na Kamati ya wataalam inayoshughulikia maombi ya eneo la nyongeza ya Bahari iliratibu vikao vya mawasilisho ya taarifa ya maombi ya Tanzania ambayo iliwasilishwa kwa Wajumbe wa Baraza La Mapinduzi na Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Idara imesimamia kikamilifu utayarishaji wa Sera ya Ardhi pamoja na marekebisho ya Sheria ya Ardhi na kusimamia utekelezaji wa Sera nyengine za Wizara (Maji, Nyumba na Nishati). Rasimu ya awali ya Sera ya ardhi tayari imetayarishwa na hivi sasa inaendelea kujadiliwa na wadau. Aidha, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ardhi *Land Tenure Act* yametayarishwa kwa kuzingatia vipengele vya umiliki na ulipaji fidia pamoja na kutayarisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya utambuzi.

Mhe. Spika, kwa upande wa shughuli za utafiti Idara imeanza kwa kukusanya tafiti zilizowahi kufanywa na kubainisha maeneo ya kuendeleza utafiti ndani ya sekta za wizara. Kiambatanisho "C" kinafafanua zaidi

MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inakusudia kusimamia utekelezaji wa kazi zifuatazo:

1. Kuimarisha Mfumo wa utoaji wa taarifa za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/14
2. Kusimamia Utekelezaji wa Kazi za Wizara kwa Ufuatiliaji na Kutathmini Miradi 10 ya Maendeleo ambayo ni:-
   i. Usambazaji wa maji na Usafi wa Mazingira
   ii. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (ADF 12).
   iii. Uhuishaji na Upanuzi wa shughuli za Maji Mijini
   iv. Usambazaji wa Maji Vijijini
   v. Usambazaji Umeme Vijijini
   vi. Uimarishaji wa Miundo Mbinu ya Umeme Unguja na Pemba
   vii. Ufungaji wa Mita 20,000 za TUKUZA
   viii. Utekelezaji wa Sera ya Nishati
   ix. Utafiti wa Nishati Mbadala

x. Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira

3. Kukuza na Kuimarisha Uhusiano baina ya wizara na wizara 3 za SMT pamoja na Washirika wa Maendeleo
4. Kuratibu matayarisho ya Sera ya Mipango Miji na kukamilisha mapitio ya Sera ya Ardhi na Sheria mbalimbali za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/14
5. Kuimarisha Mazingira ya Uendelezaji wa Tafiti kwa Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuratibu shughuli za uendelezaji wa tafiti ndani ya sekta za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/14
6. Kuandaa Mipango ya Maendeleo na Bajeti ya wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/15

Mhe. Spika, Ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh.2,384,377,000 kwa kazi za kawaida na Tsh. 59,571,530,000 kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, Idara hii imeendelea na jukumu la kusimamia Rasilimali watu pamoja na uendeshaji wa kazi za kila siku za wizara. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 Wizara yangu kupitia Idara yahii imeendelea kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kuendelea kufanya marekebisho ya mishahara ya wafanyakazi na kuhakiki wafanyakazi waliopangwa katika miundo ya Utumishi.

xxxx

4. Kukusanya shilingi 325,000,000/= kutokana na ukodishaji wa Nyumba za Serikali.
5. Kuhakikisha Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba inafanya vikao vyake kwa kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri yanayowasilishwa.

Mhe. Spika, ili Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 251,818,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida za

MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ina jukumu la kuhakikisha kwamba urithi wa kihistoria wa majengo, utamaduni wa asili, mandhari na vivutio vyengine vya Mji Mkongwe vinabakia katika hali yake ya asili kwa faida ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo pamoja na kudumisha hadhi ya urithi ya mji wetu duniani.

Mhe. Spika, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 Mamlaka ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

Kusimamia Miradi ya Uhifadhi wa Majengo

Mhe. Spika, Mamlaka imefanya kazi za usimamizi na ukarabati wa majengo mbali mbali kama inavyoonekana katoka Kiambatanisho "F".

Kuielimisha Jamii juu ya Uendelezaji wa Mradi wa Mambo Msiige

Mhe. Spika, Mamlaka imetoa elimu kwa wadau juu ya uendelezaji wa Mradi wa Mambo Msiige pamoja na uimarishaji wa eneo la wazi.Vile vile Mamlaka imewasilisha ripoti ya kumbukumbu za kikao hicho huko *UNESCO*. Aidha Mamlaka imetoa elimu kwa wamiliki wa makampuni ya ujenzi pamoja na mafundi kwa lengo la kujua changamoto wanazokabilianazo katika kazi zao za ujenzi ndani ya Mji Mkongwe, ili kuzitathmini kwa pamoja na kuzipatia ufumbuzi .

Ukaguzi wa Nyumba Zilizomo Ndani ya Eneo la Mji Mkongwe

Mhe. Spika, ukaguzi unaonesha kwamba katika eneo la Mji Mkongwe zipo nyumba zilizo katika hali mbaya 52. Kati ya hizo, Nyumba 34 zipo katika hali mbaya sana. Jadueli nambari 3 linafafanua zaidi.

Jadueli nambari 3

NYUMBA ZILIZOPO KATIKA HALI MBAYA NDANI YA MJI MKONGWE

MMILIKI	IDADI YA NYUMBA MBOVU	IDADI YA NYUMBA MBOVU SANA
SERIKALI	**13**	**7**
KAMISHENI YA WAKFU	**6**	**2**
WATU BINAFSI	**33**	**25**
JUMLA	**52**	**34**

Chanzo: Ripoti ya (2012/2013) nyumba zilizo katika hali mbaya ya Mamlaka

Aidha Mikakati mbali mbali inatekelezwa na Mamlaka ili kuzinusuru nyumba zilizo katika hali mbaya ikiwemo:-

i. Kuyaorodhesha majengo yenye hali mbaya na kushauri nini kifanyike katika kuyanusuru majengo hayo.
ii. Kushirikiana na kitengo cha Maafa cha Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika kutathmini njia bora za kukabiliana na tatizo la maafa ndani ya Mji Mkongwe.
iii. Mashirikiano na wamiliki kwa kuyahami majengo yao kabla ya kupata gharama kubwa za ukarabati.
iv. Kuwaelimisha wahusika juu ya hali halisi ya ubovu ilivyo na jinsi ilivyo hatari kwa maisha yao, jitihada gani wanahitajika kuzifanya pamoja na kufanya ukarabati wa majengo yao kabla ya kufikia hali mbaya.
v. Kutafuta njia na mbinu mbali mbali za kuomba fedha kupitia Mashirika ya Kimataifa.

Matengenezo ya Sehemu ya Nyuma Iliyoanguka ya Jengo la Beit-Aljaib

Mhe. Spika, baada ya kutokezea hitilafu katika sehemu ya nyuma ya jengo hili mwanzoni mwa mwezi wa Januari, Mamlaka imeshaanza kufanya ukarabati kwa kurudisha hali ya mandhari ya asili katika ghorofa ya kwanza ya jengo hili na inaendelea na matengenezo katika ghorofa nyengine, ili kurudisha kwa haraka matumizi ya jengo hili ambapo yataliongezea serikali mapato.

Kudhibiti Ujenzi Katika Eneo la Mji Mkongwe

Mhe. Spika, Mamlaka katika kuulinda na kuuhifadhi Mji Mkongwe, ili ubaki katika hadhi yake ya urithi wa asili, imekuwa ikitoa vibali kwa kufanya matengenezo makubwa na madogo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaoenda kinyume na taratibu zilizowekwa, kwa ufafanuzi zaidi naomba muangalie kiambatanisho "G".

Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari ya Mizingani

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa chini ya Uimarishaji wa huduma za Mji wa Zanzibar *Zanzibar Urban Services Project* (*ZUSP*), ambapo hatua iliofikiwa ni vikao vya makubaliano ya gharama za Mshauri Elekezi atakaesimamia kazi za Ujenzi.

Kuendeleza Mashirikiano na Vyuo Pamoja na Taasisi za Nje ya Nchi

Mhe. Spika, Mamlaka imepokea wanafunzi 22 kutoka Chuo Kikuu cha "*Chalmers University of Technology*" wakiongozwa na walimu wao 3 waliofika kwa ajili ya kufanya mafunzo ya utafiti katika fani za uhandisi, usanifu na mipango miji, ambapo Mamlaka ilitoa mashirikiano katika kufanikisha kazi yao hiyo.

MALENGO YA MWAKA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendeleza kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia miradi ya Uhifadhi wa majengo.
2. Kuyahami majengo 34 yaliyo katika hatari ya kuanguka pamoja na kumalizia ukarabati wa sehemu ya nyuma ilioanguka Kusini Mashariki ya Jengo la *Beit-el-Ajab*.

3. Kutoa elimu kwa waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza kuhusiana na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.
4. Kuandaa maadhimisho ya siku mashuhuri za kimataifa kama vile siku ya urithi wa Duniani 18 April na 9 Septemba siku ya Mshikamano kwa Miji ya Urithi wa Kimataifa.
5. Kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa *UNESCO* kwa Miji ya Urithi wa Dunia.
6. Kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa ukuta wa ukingo wa bahari ya Mizingani.
7. Kufanya ukaguzi ili kupunguza ujenzi unaofanyika kinyume na utaratibu.
8. Kurejesha majina ya zamani ya mitaa katika eneo la Mji Mkongwe
9. Kuimarisha maeneo ya wazi kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Mhe. Spika, ili Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 299,996,000/= kwa kazi za kawaida.

MAMLAKA YA MAJI

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, maji ni rasilimali muhimu sana katika maisha ya viumbe vyote hapa duniani. Bila maji hakuna maisha, na bila maji safi hakuna afya. Aidha, wizara inatambua kwamba idadi ya watu inazidi kuongezeka siku hadi siku na hivyo kufanya mahitaji ya maji nayo kuongezeka kwa kasi kubwa. Ili kwenda sambamba na ukuaji wa miji na ongezeko la idadi ya watu, wizara imeweka mikakati ya kuyalinda na kuyaendeleza maeneo yote yaliyotengwa kwa shughuli za maji pamoja na matumizi bora ya maji katika shughuli zetu za kila siku.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013 wizara yangu ilitekeleza programu mbili na miradi ya maendeleo ifuatayo:-

i. Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini
ii. Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

iii. Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)
iv. Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*AfDB*)
v. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka kifedha (*ADF* 12)

Usambazaji wa Maji Vijijini

Mhe. Spika, *program* hii ambayo ni endelevu na inahusisha usambazaji wa maji katika maeneo ya vijiji ambavyo huduma hiyo haipatikani vizuri. Pia kukamilisha miradi midogo midogo ya vijijini ambayo haikukamilika katika mwaka wa fedha uliopita kwa kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 programu hii ilitekeleza kazi kama zinavyojionyesha katika jaduweli namba 4 na *paragraph* ya 101.

Jaduweli nambari 4

MAENEO YALIOPATIWA HUDUMA YA USAMBAZAJI WA MAJI VIJIJINI

S/NO	KAZI ZILIZOFANYIKA	ENEO	UTEKELEZAJI
1.	Uchimbaji wa visima	Pete, Kilombero, Miwani, Bambi-Mpapa, (Unguja) Kilindi na Kokota (Pemba)	Kazi imekamilika
		Ziwani na Kiwani (Pemba)	Kazi inaendelea
2.	Ulazaji wa mabomba	Nungwi, Mkwajuni, Miwani, Chwaka (Unguja) Kojani, na Michenzani (Pemba)	Kazi imekamilika
		Matemwe (Unguja), Konde, Kilindi na Kisiwapanza (Pemba).	Kazi inaendelea
3	Uwekaji wa pampu mpya	Chwaka, Kitogani, Paje, Kiashange-1, Kiashange2, Pangeni, Kilindi, Kigongoni, Bwejuu ,Kizimkazi Kongwe na Miwani (Unguja) na Konde, Chokocho, Michenzani, Wesha, Ukutini, Daya, Kangani,	`

		Chokocho-2 na Ole Skuli (Pemba)	
4	Ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu	Jendele-Chwaka, Miwani, (Unguja). Kojani na Michenzani, Chokocho, Kojani na Konde (Pemba).	Kazi imekamilika
		Kilombero (Unguja)	Kazi inaendelea
5	Upelekaji wa umeme	Jendele-Chwaka, Miwani, Kiashange (Unguja) Konde na Kojani(Pemba)	Kazi imekamilika
6	Ujenzi wa matangi	Ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji Nungwi na Kojani	Kazi imekamilika
7	Ujenzi wa vituo vya huduma na malipo ya maji	Chwaka	Kazi imekamilika

Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji 2012/2013 ZAWA

Mhe. Spika, miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa ambayo haikuweza kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ni pamoja na Mtende, Muyuni, Tumbatu, Kinduni, Cheju, kibuteni – Makunduchi, Kidoti, Mfenesini Bumbwini, Chaani Bandamaji Matuleni, Muambe, Shumba viamboni, Wingwi Mtemani, Wingwi Mjananza, na Mtambwe Kaskazini

Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

Mhe. Spika, wizara yangu katika program hii imeweza kuchimba visima, kulaza mabomba mapya, kununua pampu na mota, ufungaji wa mita na ujenzi wa uzio katika maeneo mbali mbali kama inavyoonekanaa katika jaduweli nambari 5.

Jaduweli nambari 5

KAZI ZILIZOFANYIKA KATIKA UHUISHAJI WA MAJI MIJINI

S/NO	KAZI ZILIZOFANYIKA	ENEO	UTEKELEZAJI
1	Ufungaji wa Mita za maji	**Wateja wa Majumbani** Mwanakwerekwe na Melinne Taveta. **Wateja wa Biashara**	Kazi ya ufungaji mita ni endelevu

		Malindi, Bwawani, kilimani, Migombani, Mpendae, forodhani, Amani, Mtoni, Hakuna matata, Michungwa miwili, Dole, Welezo, Kiembesamaki na Mombasa **Wateja wa Taasisi** Benki Kuu, *ZSTC*, *TRA*, *ZSSF*, Ultimate Security Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*), *ZSTC*, *TRA*, *ZSSF*, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Ultimate Security, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Chuo cha Usimamizi wa Fedha.	
2	Uchimbaji wa visima	Chumbuni visima vitatu, Saateni viwili, na kimoja Sebleni -1.	Kazi imekamilika
3	Uwekaji wa pampu mpya	Kijito Upele- Kwarara, Dimani, Chukwani-Hali ya hewa, Chumbuni 1, Chumbuni 2, N7, N8, N9-2, Mwembe Mchomeke U050, Chunga-U008, Chunga-U026, Saateni Pumping Station, Kiembesamaki-Al Youseif, Kaburi Kikombe, Migombani, Mbweni *TRW*, Mbweni- BLW na kisima kipya cha Sebleni.	kazi hii ni endelevu
4	Ulazaji wa mabomba	Mtopepo- Saateni, Chumbuni, Dimani, Kijichi na Kaburi Kikombe.	kazi hii ni endelevu
5	Ujenzi wa Uzio	Amani (Semuso), Mwembe Madema na Kaburi Kikombe.	kazi imekamilika
		Chemchem ya Mwanyanya	Kazi inaendelea
6	Ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu	Chumbuni na Dimani.	Kazi imekamilika

Chanzo: taarifa ya Utekelezaji 2012/2013 ZAWA

Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)

Mhe. Spika, mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Misaada la *JICA*, uliendelea na kazi ya kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji kwa utowaji mafunzo mbali mbali ndani na nje ya nchi, jumla ya wafanyakazi12 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini Japani, na wafanyakazi 9 wamepatiwa mafunzo ya ndani ya nchi. Maelezo zaidi ya utekelezaji wa mradi huu yameelezwa katika *paragraph* ya 104 na 105.

Mhe. Spika, mbali na mafunzo hayo pia timu ya wataalam wa *JICA* kwa kushirikiana na wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji, pamoja na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeendeleza uhakiki (*Customer Survey*) kwa wateja wa majumbani pamoja uchukuaji wa taarifa za mita za wateja wa majumbani katika maeneo ya Bububu kwa kutumia *GPS(Global Positioning System)*.

Mhe. Spika, kupitia mradi huu kazi ya ufungaji mita kwa wateja wa majumbani imefanyika ambapo jumla ya mita 800 zimefungwa kwa wateja wa majumbani katika maeneo ya Bububu, Kijichi, na Taveta.

Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*AfDB*)

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2013, Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) na ruzuku ya Shirika la Makaazi Duniani (*UN- HABITANT*) umetekeleza kazi za ujenzi wa miundombinu ya maji ambapo tayari wakandarasi wameshaanza kazi za usafishaji wa maeneo, uchimbaji wa misingi kwa ajili ya ulazaji mabomba, ujenzi wa matangi, na uchimbaji wa visima, kwa upande wa miji mitatu ya Pemba na vijijini Unguja na Pemba sambamba na ujenzi wa matangi matano ya majaribio ya uvunaji wa maji ya mvua maskulini. (Maelezo ya mradi huu yanapatikana kwenye *paragraph* ya 107)

Aidha Mradi huu unahusisha kazi za usimamizi wa rasilimali maji ambapo Mamlaka ilitangaza tenda, ilifanya tathmini na hatimae kumpata Mshauri Mwelekezi, Mkataba kwa ajili ya kazi hiyo ya uhifadhi rasilimali maji (*Intergrated Water Resources Management*) umeshasainiwa. Vile vile, kazi ya ujenzi wa vyoo maskulini na ujenzi wa matangi ya majaribio ya uvunaji wa maji ya mvua imekamilika.

Mhe. Spika, mradi pia umeendesha mafunzo ya vitendo na Mshauri Mwelekezi wa Kampuni ya *NIRAS* kwa kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji juu ya ongezeko la huduma ya maji na udhibiti wa upotevu wa

Maji (*Water Loss Control*) sambamba na mafunzo ya uendeshaji na shughuli za kiufundi.

Vile vile, Mamlaka imeendelea na kazi ya kufanya tathmini ya mazao na majengo katika maeneo ya mradi kwa ajili ya kulipa fidia kwa walioathirika na mradi huo.

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (*ADF* 12)

Mhe. Spika, mradi huu wenye madhumuni ya kubadilisha mabomba makongwe na kuweka mapya katika Mkoa wa Mjini/Magharibi umeshaanza utekelezaji wake baada ya matayarisho ya mchanganuo wa kazi na gharama za mradi (*Project Appraisal*) pamoja na kutiliana saini na benki kwa mkataba wa utekelezaji. Hatua za kutangaza zabuni na kufanya tathmini ya kumpata mtaalamu wa manunuzi (*Technical Assistant*) imekamilika.

Aidha, utaratibu wa awali wa kuandaa taarifa na nyaraka za kumpata Mshauri Mwelekezi (*Consultant*) kwa ajili ya kazi za kuandaa michoro na usimamizi wa mradi zimekamilika na hatua iliyobakia ni kutangaza zabuni na kufanya tathmini ya kumpata Mshauri huyo.

Sambamba na utekelezaji wa mradi huu, serikali imeendeleza juhudi za kuimarisha huduma ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi kupitia mradi wa uchimbaji wa visima tisa ambapo hadi hivi sasa visima vitano vimeshachimbwa katika maeneo ya Saateni na Chumbuni. Juhudi hii inalengo la kuongeza uzallishaji wa maji, illi kukabiliana na upungufu mkubwa wa uzalishaji katika Chemchem za Mwanyanya na Mtoni. Kufuatia kukamilika kwa visima hivi, wananchi wa maeneo ya Michenzani, Shangani, Malindi, Forodhani, Mkunazini, Michenzani, Miembeni, Makadara, Kijangwani tayari wanafaidika na huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

KAZI ZA KAWAIDA

Mafunzo ya Wafanyakazi

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imewapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi wake katika fani tofauti ndani na nje ya nchi. Jumla ya wafanyakazi 2 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi katika kiwango cha Shahada ya Pili na wafanyakazi 11

wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na 13 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi na wafanyakazi 31 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi katika kuwajengea uwezo wafanyakazi hao na kumudu majukumu yao ya kazi za kila siku. Hali hiyo inafanya jumla ya wafanyakazi wanawake 16 wanaume 42 waliopatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Matengenezo ya Miundombinu

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji katika kuimarisha huduma ya maji safi na salama kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 imefanya kazi za kubadilisha mabomba ya *asbestos* na kuweka mengine mapya katika maeneo mbalimbali kama inavyoonekana katika kiambatanisho "H"

Elimu Kwa Watumiaji wa Maji

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imeedelea kufanya kazi ya kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi bora ya maji sambamba na kuwashajiisha wananchi katika kuchangia huduma ya maji safi na salama kupitia vyombo mbali mbali vya habari vya redio televisheni na magazeti. Kiambatanisho "I" kinafanunua zaidi.

Ukusanyanyaji wa Mapato

Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ilijipangia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 3.8 kutokana na mauzo ya maji na mauzo mengineyo. Hivyo hadi kufikia Machi 31, jumla ya shilingi bilioni 1.1 zimekusanywa sawa na asilimia 35 ya makadirio.

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia mamlaka haikuweza kufikia lengo ililojipangia kutokana na wananchi walio wengi bado hawajaitikia vizuri wito wa kuchangia huduma hii muhimu na adhimu hata kwa yale maeneo ambayo huduma hii inapatikana vizuri.

Hivyo kupitia Baraza lako hili tukufu ninawaomba waheshimiwa Wawakilishi kuwa msatri wa mbele katika kushajiisha dhana ya uchangiaji wa huduma ya maji, sambamba na kutoa wito kwa wananchi wote wanaopata huduma ya maji kuchangia kiasi cha fedha kilichowekwa, ili hatimae fedha hizo ziweze kutumika kuimarisha huduma hii kwa yale maeneo ambayo huduma haipatikani vizuri au haipatikani kabisa.

MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 wizara yangu imepanga kutekeleza programu mbili na miradi ya maendeleo pamoja na kukamilisha miradi ambayo haikuweza kukamilika katika mwaka wa fedha 2012/2013 kama ifuatavyo:-

i. Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini
ii. Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
iii. Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)
iv. Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*AfDB*)
v. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi na Kuijengea Uwezo Mamlaka kifedha (*ADF* 12).
vi. Kulinda na kuhifadhi vianzio vya maji

Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini

Mhe. Spika, wizara yangu inatarajia kutekeleza Mradi wa uchimbaji wa visima unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambao ulikuwa utekelezwe katika Mwaka wa Fedha uliopita, lakini Mradi huo haukuweza kutekekelezwa kutokana na kutokamilika kwa taratibu za Ubalozi wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, kama ilivyokadiriwa hapo awali.

Kwa sasa mradi huo utachimba visima 30 katika visiwa vya Unguja na Pemba, ulazaji wa mabomba ya inchi 6 na 4, ujenzi wa matangi na utiaji wa pampu katika visima vyote vitakavyochimbwa. Katika kutekeleza mradi huo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China itachangia jumla ya dola za Kimarekani milioni 1.5.

Miradi mingine ambayo imepangwa kutekelezwa kupitia program hii ni Mtende, Muyuni, Tumbatu, Kinduni, Cheju, Kibuteni – Makunduchi, Kidoti, Bumbwini-Maji Mekundu, Moga-Mwembe Mkali, Chaani Bandamaji, Matuleni, Muambe, Uroa, Ndijani, Bambi, Shumbaviamboni, Wingwi Mtemani, Wingwi Mjananza, Mgogoni, Masipa, Mtambile,Kilindi, Kiwani na Mtambwe Kaskazini. *(Makofi)*

Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

Mhe. Spika, Programu ya Uhuishaji na upanuzi wa shughuli za Maji Mijini inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imepanga kubadilisha mabomba machakavu na uwekaji wa mabomba mapya katika meneo ya Mijini Unguja na Pemba, uchimbaji wa visima, ununuzi wa pampu, mota na vidhibiti umeme, ujenzi wa uzio pamoja na ununuzi wa mita.

Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)

Mhe. Spika, mradi huu ambao unafadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Misaada la *JICA*, utaendelea na kazi ya ufungaji mita kwa wateja wetu mbali mbali, kufanya mafunzo ya ndani na nje kwa lengo la kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji.

Vile vile kuendelea kufanya uhakiki (*survey*) wa wateja katika wilaya nyengine zilizobakia, ili kuwajua wateja wanaopata na wasiopata huduma ya maji kwa kutumia *GPS* sambamba na kupata michoro inayoonesha maeneo yaliofungwa mita. Aidha kazi kama hiyo imepangwa kufanyika katika maeneo yote yenye vianzio vya maji.

Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*AfDB*)

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imepanga kukamilisha Mradi huu kwa kukamilisha ujenzi wa matangi yaliyopangwa kujengwa mijini na vijijini. Aidha mradi utakamilisha ujenzi wa visima, usambazaji wa mabomba, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea visima pamoja kukamilisha kulipa fidia kwa wale wote walioathirika na kuharibiwa mali zao. Pia mradi utakamilisha ujenzi wa vyoo katika skuli 81 zilizochaguliwa Unguja na Pemba (Unguja skuli 47 na Pemba skuli 34), ili kuongeza hali ya usafi mashuleni.

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (*ADF* 12)

Mhe. Spika, mradi huu ambao unahusisha zaidi uimarishaji wa miundo mbinu ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi na kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji kifedha, unatarajia kubadilisha mabomba machakavu na kuweka mabomba mapya katika eneo la Mji Mkongwe, uchimbaji wa visima 10, kwa ajili ya kuongeza kiwango cha uzalishaji wa maji, ufungaji wa mita za kupima uzalishaji na matumizi ya maji ili kuijengea uwezo Mamlaka ya maji kifedha.

Mradi wa Uchimbaji wa Visima

Mhe. Spika, mradi wa uchimbaji wa visima 50 unaofadhiliwa na Mtawala wa *Ras-AL–Kheimah* unatarajia kuchimba visima hivyo vitakavyowanufaisha wakaazi wapatao zaidi ya 224,000 katika Wilaya zote za Unguja na Pemba, ambapo hadi sasa Mkandarasi kutoka katika Kampuni ya Chimba ya Tanzania alieteuliwa na Muhisani yupo nchini kwa ajili ya kuanza kazi hiyo. Maeneo yatakayonufaika na Mradi huu ni kama yanavyoonekana katika Kiambatanisho"J"

Kuvilinda na Kuviwekea Uzio Vianzio Vya Maji

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha Mamlaka ya maji inatarajia kuendelea na ulinzi na uhifadhi wa vianzio vya maji kwa upandaji wa miti, Ujenzi wa uzio na upimaji wa maeneo kwa lengo la kuyatafutia hati miliki baadhi ya maeneo yenye vianzio vya maji ili kuepusha wimbi kubwa la uvamizi wa maeneo hayo kwa shughuli mbali mbali za kijamii.

KAZI ZA KAWAIDA

Matengenezo ya Miundombinu

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji itaendelea kufanya matengenezo ya miundombinu yake kila yanapotokea maharibiko, ili kuongeza wingi wa maji katika maeneo ya mijini na vijijini pamoja na kupunguza upotevu wa maji yanayovuja katika mabomba yaliyopasuka kwa kuyabadilisha mabomba hayo na kuweka mengine mapya, kubadilisha pampu na mota zilizoungua na kuweka nyengine mpya.

Mafunzo ya Wafanyakazi

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inategemea kuendelea na kuwapatia wafanyakazi wake mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu. Katika hali hiyo Mamlaka inategemea kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake wapatao 20 kwa mafunzo ya muda muda mrefu na 72 kwa mafunzo ya muda mfupi.

Elimu Kwa Watumiaji wa Maji

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji itaendelea kushajiisha jamii juu ya umuhimu wa kuchangia huduma ya maji kwa maeneo yote ya mijini na vijijini kwa yale maeneo ambayo elimu hiyo bado haijawafikia wananchi.

Ukusanyanyaji wa Mapato

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 inategemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni 3.6. Aidha ili kuongeza makusanyo ya fedha Mamlaka imejipanga kuongeza vituo vya mauzo ya maji mijini na vijijini kwa lengo la kuimarisha huduma hiyo pamoja na kuwapunguzia wananchi masafa marefu ya kufuata huduma zetu.

IDARA YA NISHATI NA MADINI

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, Idara ya Nishati na Madini ni taasisi yenye jukumu la kusimamia Sekta ya Nishati na Madini hapa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha wa 2012-2013 Idara ya Nishati na Madini ilisimamia na kutekeleza mambo yafuatayo:-

Kuandaa Mpangokazi wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Zanzibar

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012-2013, Idara imeweza kutayarisha Mpango Kazi kama ilivyopangwa kwa mashirikiano makubwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais chini ya Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira (*Strengthening Environment and Climate Changes Governance for Zanzibar*). Mpangokazi wa Sera ya Nishati utasaidia sana utekelezaji wa Sera hio.

Kuendelea na Juhudi za Kuwapatia Wananchi wa Zanzibar Elimu Juu ya Matumizi ya Nishati Mbadala kama vile Umeme wa Jua na Upepo

Mhe. Spika, juhudi za kuwapatia wananchi wa Zanzibar uwelewa juu ya matumizi ya nishati mbadala kama vile umeme wa jua na upepo zimeanza kutekelezwa kwa mashirikiano na Taasisi za Elimu (Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume) kwa upande wa Serikali na

jumuiya zisizo za kiserikali kama vile *ZASEA*. Hii ni sehemu muhimu ya hatua ya utekelezaji wa juhudi za kuwapatia wananchi elimu juu ya matumizi ya nishati mbadala kwa mashirikiano na taasisi kama hizo ambazo zinaweza kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi.

Kushiriki katika Masuala yote ya Nishati ya Kitaifa, Kikanda, na Kimataifa.

Mhe. Spika, idara inaendelea kushiriki katika masuala ya nishati ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa madhumuni ya kuongeza uwezo na uelewa.

Idara imeweza kushiriki katika vikao vya Kamati Tendaji (*Steering Commitee*) ya Mikutano Mikuu ya Mafuta ya Afrika ya Mashariki (*EAPCE'13*) iliyofanyika katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambao ni matayarisho ya Mkutano Mkuu wa Mafuta wa Afrika Mashariki uliofanyika Arusha tarehe 6-8 Februari, 2013.

Vile vile Idara imeshiriki katika mkutano wa kutayarisha mikataba ya utafutaji na uzalishaji wa Mafuta (*PSA Negotiations*) ambao ulifanyika Nairobi na kushiriki katika mafunzo mafupi kuhusu Nishati Mbadala nchini China kwa kuwahusisha mwanasheria wa Idara na Wataalamu wengine.

Kuendelea Kusimamia Upatikanaji wa Mafuta Zanzibar (Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa).

Mhe. Spika, nishati ya mafuta kwa ujumla imeendelea kupatikana kwa mwaka wa fedha 2012-2013. Changamoto inayoikabili sekta hii ni kupanda na kushuka kwa bei ya mafuta kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo katika soko la kimataifa na viwango hafifu vya mafuta kwa baadhi ya bidhaa hizo zinazoingizwa nchini. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imekuwa ikilipatia ufumbuzi suala hili kwa njia ya mazungumzo na makampuni yanayoingiza mafuta nchini.

Mhe. Spika, changamoto hizi zinatazamiwa kudhibitiwa kwa kiasi kikubwa na Taasisi inayotazamiwa kuundwa baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Kuanzisha Udhibiti wa Maji na Nishati (*ZURA*) na Baraza la Wawakilishi mwezi wa Aprili 2013.

Idara inaendelea kufuatilia takwimu za mafuta yanayoingizwa nchini katika "Depot" za Mtoni ili kuhakikisha nishati inapatikana bila ya

matatizo. Takwimu ya bidhaa hiyo ni kama inavyopatikana katika kiambatanisho ”K”

Kukamilisha Sheria ya Kusimamia Usambazaji wa Mafuta na ile ya Mdhibiti wa Nishati.

Mhe. Spika, Sheria ya kuanzisha kwa Mdhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (*Zanzibar Utilities Regulatory Authority – ZURA*) tayari imeshapitishwa na Baraza lako Tukufu katika kikao cha Mwezi wa Aprili 2013 na kwa sasa inasubiri kuwekewa saini kwa hatua nyenginezo.

Aidha, matayarisho ya Sheria ya Usambazaji wa Mafuta na Gesi *(Petroleum Supply Act)* yamefikia katika hatua ya Kamati ya Makatibu Wakuu na Idara inatarajia kuiwasilisha katika vikao vya juu zaidi katika Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika Kuimarisha na Kutekeleza Programu ya Mafunzo ya Mafuta na Gesi Asilia.

Mhe. Spika, idara inaendelea kufanya juhudi ya kuwapatia Mafunzo wafanyakazi wa Idara hii ili kuweza kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa fani ya nishati ikiwemo ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar.

Hata hivyo Kampuni ya *Ras-el-Khaimah Tanzania Ltd*. yenye Makao yake Makuu nchini *UAE* inaendelea kugharamia mafunzo kwa Wazanzibar wenye sifa na kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ambapo mfanyakazi mmoja (1) wa Idara ya Nishati na Madini amewezeshwa kupata masomo katika fani ya mafuta *(Petroleum Engineering)* nchini Uingereza na kufanya idadi ya waliopata ufadhili kupitia kwa Kampuni hiyo kufikia watatu(3). Mhe. Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa programu ya mafunzo na mafuta na gesi asilia yanaendelea katika *paragraph* ya 134.

Mhe. Spika, idara imewasilisha maombi ya ajira katika fani za Sayansi na Ufundi kwa kiwango cha Digrii ya Kwanza na ina tarajia kupata nafasi mbili ambazo zimekusudiwa kutumiwa kwa kuwapeleka nje kwa masomo ya Mafuta na Gesi ngazi ya Digirii ya Pili. Utaratibu huu utaweza kuzalisha kwa haraka wataalamu wa fani hio kwa vile mafunzo yao yanakuwa kwa muda mfupi ukilinganisha na kuwapeleka waliomaliza kidato cha sita.

Aidha, Idara imefanya mazungumzo na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar ili kuandaa mikakati maalum ya kushajiisha wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita wanaojiunga na masomo ya juu ya muda mrefu kuchukuwa fani za Mafuta na Gesi Asili kwa matayarisho ya siku za mbele.

Kwa kuanzia, taasisi hizi mbilli zimekubaliana kuanza Mkakati Rasmi kwa Wanafunzi waliomaliza Mwaka 2012/13 ambapo jumla ya Wanafunzi sita wamejiunga na vyuo vya hapa Nchini kwa ufadhili wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar. Vile vile Idara kupitia Wizara Aradhi, Makaazi, Maji na Nishati imewasilisha maombi ya mafunzo katika fani za mafuta na gesi asilia kupitia Serikali ya Oman.

Kushirikiana na Serikali ya Norway katika Utekelezaji wa Kazi ya Tathmini ya Mazingira ya Zanzibar (*Strategic Environmental Impact Assesment*)

Mhe. Spika, suala hili bado halijatekelezwa kutokana na kutokukamilika kwa mipango ya utekelezaji wa suala. Hata hivyo, idara inafanya mazungumzo na Idara ya Mazingira katika kujijengea uwezo wa ndani kabla ya kutekelezwa kwa hatua ya kazi ya tathmini ya mazingira ya Zanzibar (*Strategic Environmental Impact Assesment*).

Hili limeonekana ni muhimu kwa vile taasisi hizi mbili na hasa Idara ya Mazingira ndiyo itakayokuwa msimamizi mkuu wa suala hili. Idara hizi mbilizinaendelea kuwasiliana na taasisi nyenginezo ambazo zitawezesha kufanikisha ujengaji wa uwezo uliokusudiwa.

Kuanzisha Mikakati ya Kujiimarisha na Utafiti na Matumizi ya Teknolojia za Nishati Mbadala

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, idara imefanya mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi kuhusiana na suala hili. Umoja wa Ulaya (*EU*) ulifanya tathmini ya nishati mbadala kwa Zanzibar (*Renewable Energy Assessment for Zanzibar*) na tathmini hiyo iliwasilishwa rasmi Serikalini kwa kuzingatiwa. Baada ya Serikali kuu kuzingatia tathmini hiyo imeamuliwa kufanyike kwa utafiti yakinifu (*feasibility study*) katika masuala ya nishati mbadala. Kazi hiyo ya utafiti yakinifu inatarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha ujao baada ya kupatikana msaada wa *EURO* 3,000,000 kutoka *EU*. Vile vile idara kwa upande wake imefanya utambuzi wa maeneo manane (8) ya Unguja(4) na Pemba(4), ili kujitayarisha na kazi hio ya utafiti wa kina kwa kuwekewa vifaa vya ukusanyaji wa takwimu muhimu za upepo ili

kuangalia uwezekano wa kuzalisha umeme wa upepo. Mhe. Spika, maelezo ya kutekeleza mikakati ya utafiti wa nishati mbadala yanaendelea kwenye *paragraph* ya 137.

Mhe. Spika, kwa upande wa taasisi za ndani ya nchi, idara imefanya makubaliano (*MoU*) na taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume na Jumuiya ya *ZASEA* kwa madhumuni ya kuendeleza utafiti na matumizi ya nishati mbadala. Idara ya Nishati na Madini imeweza kuipatia Taasisi ya Karume vifaa mbalimbali vya kufundishia somo la nishati mbadala baada ya kuwasiliana na Taasisi ya kijerumani (*GSW*) na kwa sasa Idara inawasiliana na Kampuni kadhaa kwa malengo hayo

MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, Idara ya Nishati na Madini katika mwaka wa fedha 2013/2014 imepanga kutekeleza yafuatayo:

1. Utekelezaji wa Mradi wa Sera ya Nishati Awamu ya Pili *(Second Phase)* chini ya mashirikiano ya pamoja na Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* na Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango kazi wa Sera hio.
2. Utekelezaji wa Mradi wa Nishati Mbadala kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*
3. Kuvipatia vijiji 12 vya Unguja na Pemba uelewa wa teknolojia ya elimu ya matumizi ya Nishati Mbadala kama vile Umeme wa Jua na Upepo.
4. Kushiriki katika masuala yote ya nishati ya kitaifa, kikanda na kimataifa.
5. Kuendelea kusimamia upatikanaji wa mafuta Zanzibar (Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa).
6. Kukamilisha utayarishaji wa Sheria ya Kusimamia Usambazaji wa Mafuta.
7. Kuendelea Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuimarisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya Mafuta na Gesi Asilia.
8. Kujiimarisha na utafiti na matumizi ya teknolojia za Nishati mbadala kwa kushirikiana Washirika wa Maendeleo na taasisi mbali mbali za nje na ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na kujenga mashirikiano katika kutimiza lengo la upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa visiwa vya Zanzibar*(Energy Security).*

9. Kuimarisha Ofisi na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara kwa Mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, ili Idara ya Nishati na Madini iweze kutekeleza malengo yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 735,868,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 6,870,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

SHIRIKA LA UMEME:

Mhe. Spika, katika kuendeleza juhudi za kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma bora ya Umeme na iliyo ya uhakika hapa Zanzibar. Shirika la Umeme kwa mwaka wa fedha 2012/2013 limefanikiwa kutekeleza Miradi mbali mbali kama vile Ujenzi wa Njia ya Pili ya Umeme Unguja, Ujenzi wa Vituo Vipya Vitatu vya Umeme Unguja na Usambazaji wa Umeme Vijijini Unguja na Pemba.

Kutekelezwa kwa miradi hii pamoja na shughuli nyengine inategemewa kuleta changamoto kubwa za kimaendeleo hapa nchini kwa kuondosha mgao wa umeme katika maeneo yote ya Unguja, kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo, kuongeza wawekezaji wa ndani na nje kwenye sekta za Utalii, Viwanda, Kilimo nakadhalika, kuongeza ajira binafsi na hatimaye kusaidia kukuza kiwango cha pato la taifa.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio makubwa tuliyoyafikia, ukatikaji wa umeme bado upo kwenye baadhi ya maeneo. Matatizo haya yanatokana na sababu kubwa zifuatazo ambapo shirika linapambana nazo:-

i. Uchakavu wa miundo mbinu ya usambazaji na ugawaji Umeme.
ii. Uharibifu wa Mazingira kwenye njia na miundo mbinu ya kusambaza Umeme, kunako fanywa na Wananchi wasio waaminifu.
iii. Wimbi la Wizi wa waya wa Shaba kwenye maeneo mbali mbali.

MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Shirika lilikadiria kukusanya shilingi 55,425,794,240.00/= kutokana na biashara ya kuuza

umeme na huduma zinazotolewa kwa wananchi. Hadi kufikia 31 Machi, 2013 shirika limekusanya jumla ya sh 36,618,471,782.00/= sawa na asilimia 66% ya makadirio.

.

Nam707

IMESAHIHISHWA

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (anaendelea)

Hadi kufikia 31 Machi, 2013 Shirika limekusanya jumla ya Tsh 36,618,471,782.00 sawa na asilimia 66% ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilikadiria kutumia Tsh 59,461,571,289.00 kwa matumizi kama inavyoonekana katika jaduweli ifuatayo:-

Jaduweli nambari 6

MAELEZO	**GHARAMA ZA MATUMIZI (Tsh)**
Ununuzi wa umeme na mafuta ya kuzalisha umeme	41,519,577,144.00
Gharama za Uendeshaji wa kazi za Shirika	17,,815,814,708.00
Jumla ndogo	42,335,391,869.00
Kazi za Maendeleo	17,126,179,420.00
Jumla	59,461,571,289.00

Mhe. Spika, hadi kufika Machi 2013, Shirika limetumia Tsh 47,803,746,919.00 sawa na asilimia 80 ya makadirio kama inavyoonekana katika Jaduweli ifuatayo:-

Jaduweli nambari 7

MAELEZO	TSH
Malipo ya ununuzi wa umeme TANESCO	33,463,412,834
Kazi za Kawaida	7,496,233,138
Kazi za Maendeleo	6,844,100,947
Jumla	47,803,746,919

Utekelezaji wa Kazi za Kawaida:

Kukuza Ubora wa Huduma ya Umeme kwenye maeneo

Mhe. Spika, Shirika limeimarisha miundombinu ya kusafirishia na kusambaza umeme Unguja na Pemba kwa kupima (kukaguwa) transforma 115, kubadilisha transfoma 12, Nguzo 156 pamoja na kubadilisha Mita 17,754 za waya chakavu Unguja na Pemba

Miradi ya Maendeleo:

Mhe. Spika, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, Shirika lilijipanga kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Pili ya Umeme Unguja
ii. Uimarishaji wa Njia na Ujenzi wa Vituo Vipya Vitatu vya Umeme Unguja.
iii. Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini.
iv. Mradi wa Ufungaji Mita 50,000 za TUKUZA

Utekelezaji wa miradi:

Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Pili ya Umeme Unguja.

Mhe. Spika, Mradi wa Njia ya Pili ya Umeme Unguja ambao ulianza mwaka 2008 kwa sasa umekamilika na ulizinduliwa rasmi tarehe 10 Aprili, 2013 na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Muhamed Shein. Mradi huu uligharimu Dola za Kimarekani 64.4 Milioni sawa na Tsh Bilioni 97.6. Kati ya fedha hizo, Dola za Kimarekeni 62.3 Milioni ambazo ni sawa na Tsh Bilioni 93.4 Bilioni zilichangiwa na Serikali ya Marekani na Dola za Marekani 2,100,000 ambazo ni sawa na Tsh Bilioni 3.2 ni mchango wa

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Shirika la Umeme limechangia shilingi bilioni 1.

Mradi huu ulihusisha kazi za ujenzi wa vituo (*Substations*), ujenzi wa njia ya Umeme wa Nchi kavu *(Overhead line*) pamoja na ulazaji wa waya baharini.

Uimarishaji wa Njia na Ujenzi wa Vituo Vipya Vitatu vya Umeme Unguja

Mhe. Spika, mradi huu ambao ulianza mwaka 2010 umefadhiliwa na Serikali ya Japani na umegharimu Yeni za Kijapani bilioni 3 sawa na Tsh Bilioni 55. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechangia Tsh Bilioni 2.7 na Shirika la Umeme limechangia Tsh Milioni 800 hadi kukamilika kwa kazi za mradi.

Mhe. Spika, mradi huu ulihusisha kazi za ujenzi wa vituo vipya vitatu (Mwanya, Mtoni na Welezo) pamoja na Ujenzi wa laini ya Umeme ya Kusini (Mtoni – Tunguu), Kaskazini (Mahonda – Mtoni). kazi za mradi huu zimekamilika sambamba na za mradi wa njia ya pili ya umeme Unguja.

Mhe. Spika, napewa taarifa tu kwamba mtaalam wa JEC ambaye anaeshughulikia suala hili yupo pale kwenye Jukwaa anasikiliza bajeti hii.

Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini

Mhe. Spika, Shirika lilipanga kutumia shilingi bilioni 1.2 kwa kazi za kusambaza Umeme Mijini na Vijijini. Kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni 775 kutoka mfuko wa Shirika la Umeme na shilingi milioni 425 ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hadi kufikia Machi 2013, jumla ya Tsh 1,547,282,281.00 zimetumika kwa ununuzi wa Nguzo, Waya, Transfoma, na vifaa vya umeme kwa kazi za kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba kama invyoonekana katika kiambatanisho “L”

Mhe. Spika, Shirika linaendelea na kazi za ujenzi wa laini za kusambaza umeme kwenye vijiji cha Mtwango – Pongwe, Kibonde Maji na Kitundu – Mkanyageni.

Mradi wa Ufungaji Mita 50,000 za TUKUZA

Mhe. Spika, Mradi huu umehusisha uondoaji wa mita za kawaida ambazo bado zinatumika kwa Wananchi. Hadi kufikia Machi, Shirika limenunua mita 20,000 za Tukuza zilizogharimu Tsh Bilioni 1.5 ambazo zinaendelea kufungwa kwenye maeneo ya mijini na vijijini. Mita 5,455 tayari zimeshafungwa kwa wateja wapya na mita 6,045 zimebadilishwa kwa mita kongwe katika maeneo mbalimbali

MALENGO YA MWAKA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Shirika limejipanga kutekeleza miradi ya maendeleo ifuatayo:-

1. Mradi wa uimarishaji wa miundo mbinu ya umeme kwa msaada wa Norway.
2. Mradi wa usambazaji umeme vijijini**.**
3. Ufungaji wa Mita 20,000 za TUKUZA

Mapato na Matumizi

Mhe. Spika, Shirika linakadiria kukusanya shilingi Tsh.84, 287,637,412 Kati ya Fedha hizo, Tsh.74, 474,860,000 ni mauzo ya umeme na Tsh. 9,812,774,412 zitakusanywa kutokana na mapato mengineyo.

Aidha, Shirika linategemea kutumia jumla ya Tsh.80, 546,365,942 kwa kazi za Kawaida na za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Tsh.36,917,456,792 kwa ununuzi na uzalishaji umeme. Tsh. 19,866,898,650 kwa kazi za Kawaida na Tsh. 23,762,010,500 kwa kazi za Maendeleo.

AFISI KUU PEMBA

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba inajukumu la kusimamia shughuli zote za Wizara na kutekeleza Malengo yaliopangwa na Taasisi zetu kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa majukumu ya Afisi Kuu Pemba kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 tayari umeainishwa katika utekelezaji wa Taasisi zetu. Miongoni mwa kazi zilizoratibiwa na kusimamiwa na Ofisi Kuu Pemba ni pamoja na Upimaji wa viwanja kwa ajili ya shughuli mbalimbali, utayarishaji na utoaji wa Hati Miliki, uthamini na uhaulishaji, kupokea na kutolea maamuzi kesi zinazohusiana na ardhi,

kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi na kufanya matengenezo ya Nyumba za Serikali.

MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, Kwa Mwaka wa Fedha 2013/ 2014 Afisi kuu Pemba imekusudia kuendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi na kuwalipia wanaoendelea na mafunzo.
ii. Kupima viwanja kwa ajili ya makaazi, biashara, taasisi, vitega uchumi, mashamba na mengineo.
iii. Kutayarisha ramani kwa ajili ya utoaji wa hati miliki.
iv. Utayarishaji wa hati miliki za matumizi ya ardhi.
v. Kufanya mapitio katika sehemu zilizopangwa kwa ajili ya utalii Pemba.
vi. Kusimamia Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika baadhi ya vijiji vya Pemba.
vii. Kutayarisha miongozo ya maendeleo ya majengo katika miji ya Pemba.
viii. Kupunguza migogoro inayohusiana na ardhi.
ix. Kuzifanyia matengenezo nyumba za Serikali
x. Kuyafanyia matengenezo majengo ya Ofisi
xi. Kushajihisha masuala ya Jinsia na Ukimwi kwa Wafanyakazi

Mhe. Spika, Ili Ofisi Kuu Pemba iweze kusimamia na kutekeleza malengo ya Wizara kwa upande wa Pemba kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 1,123,007,000.00 kwa kazi za kawaida.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuwatumikia Wananchi wenzangu kupitia Wizara hii, ambayo inawagusa wananchi wenyewe ama mmoja mmoja au kwa ujumla wao.

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba katika utekelezaji wa Wizara yangu ndani ya Mwaka uliomalizika kulijitokeza changamoto kadhaa kama

ilivyoelezwa. Hata hivyo, Wizara yangu ilijitahidi kuzikabili kadri ilivyoweza, na naamini wananchi wameona matunda ya juhudi zetu hususan katika suala la Umeme wa Mgao. Ninawashukuru sana wananchi kwa uelewa wao, sambamba na ushirikiano wao katika kupata huduma bora zaidi kutoka katika Wizara hii.

Mhe. Spika, kwa Mwaka ujao wa Fedha 2013/2014, wananchi wategemee ongezeko kubwa la ubora wa huduma na ufanisi wa utendaji kutoka Wizarani kwangu. Mradi wa Maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi utaanza kutekelezwa, usajili wa Ardhi na huduma nyenginezo zitazidi kushika kasiza kiutekelezaji.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara yangu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mashirika ya Kimataifa na yasiyo ya Kimataifa, Sekta binafsi, NGO‟s, CBO‟s na wananchi kwa jumla kwa mashirikiano makubwa waliyoyaonesha kwa Wizara yangu kwa misaada yao ya hali na mali waliyoitoa na wanayoendelea kutoa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara yangu. Washirika hao ni pamoja na JAPAN, NORWAY, SWEDEN, MAREKANI, CHINA, EGYPT, FINLAND, UNICEF, UNESCO, UNDP, DFID, JICA, Sida, UN HABITAT, AFDB, TASAF, ZATI, IFA, NORAD, RED CROSS, ACRA, BENKI YA DUNIA, IVO DE CARNERI FOUNDATION, UBELGIJI, RAK GAS TANZANIA, EU, PETRAD, MCC ya Marekani, RAS-AL-KHEIMAH pamoja na wale wote ambao kwa bahati mbaya hatukuweza kuwataja . Tumepata faraja kubwa sana kwa michango yao kwa maendeleo ya nchi yetu, tunaahidi kuienzi na kuiendeleza na kuithamini michango hiyo.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe Mhe. Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini wa hali ya juu.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, kwa imani yake kwangu na kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuitumikia nchi yangu. Aidha namshukuru Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais kwa misaada na maelekezo yao kwangu wote ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu uadilifu zaidi katika kazi zao, afya njema na maisha marefu pamoja na familia zao.

Vilevile, tunawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilizotembelea na kufanya vikao na Wizara yangu. Maoni, ushauri na maelekezo yao kwetu yamesaidia sana sio tu katika utekelezaji wa kazi bali pia katika uandikaji wa hotuba hii. Shukurani maalum kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa msaada wao mkubwa kwetu.

Mhe. Spika, naomba pia kumshukuru sana Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Wafanyakazi wenzake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuwezesha vitabu vya Bajeti za Wizara zote kupatikana kwa wakati.

Mhe. Spika, shukurani maalum ziwaendee wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa msaada wao mkubwa kwangu Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu bila ya msaada na mashirikiano yao bajeti hii isingeweza kuwasilishwa. Mhe. Spika, ninashukuru kwamba wafanyakazi wa Wizara hii siku hizi wameanza kunielewa vizuri na tunakwenda vizuri sana. Walipata tabu nilipoanza.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapokee, wayajadili kwa kina, watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe Makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza kazi, majukumu na malengo niliyoyaeleza, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh 7,519,000,000 kwa kazi za kawaida na Tsh 69,721,030,000 kwa kazi za Maendeleo. Kati ya Fedha hizo Tsh 4,890,000,000 ni mchango wa Serikali na Tsh 64,831,030,000 ni mchango wa wahisani kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, sasa naliomba Baraza lako Tukufu likubali matumizi ya Wizara yangu jumla ya Tsh 77,240,030,000 na pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Tsh 4,039,700,000 kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Kwa ufafanuzi zaidi ninaomba muangalie Kiambatanisho “M1 na M2”

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KIAMBATANISHO "A"

MUHTASARI WA MAKUSANYO YA FEDHA ZA MAPATO JULAI 2012 - MACHI 2012

KIFUNGU	MAELEZO	MAKISIO 2012 - 2013	WASTANI WA MAKUSANYO	MA HA JU MA 2
03	AFISI KUU PEMBA	156,000,000	70,350,000	62,71
05	IDARA YA UJENZI	7,000,000	6,310,000	2,242
07	MAMLAKA YA MJI MKONGWE	24,000,000	21,650,000	15,98
09	IDARA YA ARDHI NA USAJILI	3,505,000,000	2,053,625,000	1,767 38
10	IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI	250,000,000	175,752,665	36,75

11	IDARA YA NYUMBA NA MAKAAZI	150,000,000	112,500,000	93,6
	JUMLA	**4,092,000,000**	**2,440,187,665**	**1,97 55**

KIAMBATANISHO "B1".

MUHTASARI WA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA MAENDELEO JULAI 2012- MACHI 2013 - MCHANGO WA SERIKALI (SMZ)

KIFUNGU	MAELEZO	MAKISIO 2012 - 2013	WASTANI WA MATUMIZI JULAI - MACHI 2013	FE ZI AT A J MA 201
04	MRADI WA USAMBAZAJI WA MAJI SAFI NA MAZINGIRA	2,600,000,000	2,263,000,000	963 00
	USAMBAZAJI MAJI VIJIJINI	600,000,000	450,000,000	370 00
	UHUISHAJI NA UPANUZI WA MAJI MIJINI	700,000,000	525,000,000	474 00

	UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA MAJI MJINI MAGHARIBI	-	-	-
	SECOND INTERCONECTOR SUB-MARINE CABLE	75,000,000	75,000,000	75 0
	KUIMARISHA USAMBAZAJI UMEME UNGUJA	431,928,000	431,928,000	43 00
	KUJENGA UWEZO NA MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU YA UMEME ZANZIBAR			
	USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI	425,000,000	425,000,000	33 00

05	UJENZI WA NYUMBA ZA MICHENZANI /MPAPA	100,000,000	100,000,000	83,0
08	SERA YA NISHATI	150,000,000	112,500,000	45,0
	UTAFITI WA NISHATI MBADALA	50,000,000	37,500,000	26,0
10	USIMAMIZI ENDELEVU WA A/MAZINGIRA (SMOLE)	170,000,000	127,500,000	64,0
	JUMLA	**5,301,928,000**	**4,547,428,000**	**2,860**

KIAMBATANISHO "B2".

MUHTASARI WA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA MAENDELEO
JULAI 2012- MACHI 2013 - MCHANGO WA WAHISANI

KIFUNGU	MAELEZO	MAKISIO 2012 - 2013	F ZIL KAN MA
04	MRADI WA USAMBAZAJI WA MAJI SAFI NA MAZINGIRA	27,000,000,000	9,5
	USAMBAZAJI MAJI VIJIJINI	-	
	UHUISHAJI NA UPANUZI WA MAJI MIJINI	-	
	UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA MAJI MJINI MAGHARIBI	-	
	SECOND INTERCONECTOR SUB-MARINE CABLE	30,608,000,000	58,9
	KUIMARISHA USAMBAZAJI UMEME UNGUJA	-	30,3

	MATUMIZI BORA YA NISHATI KWA KUPUNGUZA GESI, MKAA NA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI	1,254,400,000	
	KUJENGA UWEZO NA MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU YA UMEME ZANZIBAR		
	USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI		
05	UJENZI WA NYUMBA ZA MICHENZANI /MPAPA		
08	SERA YA NISHATI	-	
	UTAFITI WA NISHATI MBADALA	-	
10	USIMAMIZI ENDELEVU WA A/MAZINGIRA (SMOLE)	9,210,400,000	4,40
	JUMLA		

		68,072,800,000	**103,**

KIAMBATANISHO "B3".

MUHTASARI WA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA KAWAIDA JULAI 2012 - MACHI 2013

KIFUNGU	MAELEZO	MAKISIO 2012 - 2013	WASTANI WA MATUMIZI JULAI - MACHI 2013	
03	AFISI KUU PEMBA	1,002,000,000	717,424,313	5 4
04	IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI	2,174,000,000	1,628,759,000	1 3
05	IDARA YA UJENZI	622,000,000	442,701,750	3 0

07	MAMLAKA YA MJI MKONGWE	330,000,000	236,225,000	19 3
08	IDARA YA NISHATI	216,000,000	153,268,000	1 0
09	IDARA YA ARDHI NA USAJILI	359,000,000	253,522,000	2 0
10	IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI	358,000,000	230,661,800	2 0
11	IDARA YA NYUMBA NA MAKAAZI	269,000,000	185,881,525	1 0
12	MAHKAMA YA ARDHI	194,000,000	125,052,500	1
13	IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI	738,000,000	538,556,675	5 1
14	MRAJIS WA ARDHI	153,000,000	93,731,000	8
15	IDARA YA MIPANGO MIJI	293,000,000	212,336,200	1 0

	NA VIJIJI			
	JUMLA	**6,708,000,000**	**4,818,119,763**	**4**

KIAMBATANISHO “C”.

MAENEO YALIOFANYIWA UTAFITI NA TAFITI ZILIZOPANGWA KUENEDELEZWA ZAIDI

TAFITI ZILIZOFANYWA

1. Zanzibar Stone Town Ng’ambo Buffer Zone Precinct Framework cording
2. Frictions, Fractures and Culture resilience of Swahili Coast town
3. Swahili House
4. Applicability of Volunteered Geographic Information in Assessing Subjective quality of life case of Zanzibar
5. Integrating Community Participation for Urban Development Planning in Zanzibar.
6. Feasibility study for Urban Water supply Network Rehabilitation in Unguja
7. Hydrological Map of Zanzibar
8. Water equity in Tourism

9. Land and gender studies in Zanzibar
10. Land Market study in Zanzibar
11. Land Disputes Study in Zanzibar
12. An assessment of rain water harvesting potential in Zanzibar.
13. Zanzibar renewable energy assessment

MAENEO YALIOBAINISHWA KWA AJILI YA KUFANYIWA TAFITI ZAIDI

1. Alternative source of Energy
2. Alternative energy source for water sources.
3. Study on water demand management.
4. Land related Taxation
5. Social Housing
6. The study on the development of water Resources in Zanzibar

KIAMBATANISHO "D1"

WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA KIPINDI CHA JULAI 2012 – MACHI 2013

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NCH
1	**IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI**	1		1	MALEY
2		1		1	TANZA
3			1	1	NETHE ND
4		1		1	TANZA ZANZIB
5		1		1	TANZA

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NC
6		1		1	TANZ/ ZANZI
7	**MRAJIS WA ARDHI**	1		1	TANZ/ ZANZI
8			1	1	TANZ/ ZANZI
9	**MAMLAKA YA MJI MKONGWE**		1	1	TANZ/ ZANZI
10		**1**		1	TANZ/ ZANZI
11	**MIPANGO MIJI NA**	**1**		1	TANZ/

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NCH
	VIJIJI				
12	**NYUMBA NA MAKAAZI**	**1**		1	TANZA
13		**1**		1	TANZA ZANZIB
14	**UJENZI**		1	1	CHINA
15			1	1	TANZA ZANZIB

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NC
16			1	1	TANZA ZANZI
17			1	1	TANZA ZANZI
18			1	1	TANZA ZANZI
19			1	1	TANZA ZANZI
20		**1**		1	TANZA ZANZI
21	**NISHATI NA MADINI**	**1**		1	UINGE A

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NCH
22			2	2	TANZA ZANZII
23	**SHIRIKALA UMEME**	**1**		1	TANZA ZANZII
24		**1**		1	TANZA ZANZII
25		**1**		1	TANZA ZANZII
26		**1**		1	

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NC
27			1	1	TANZA ZANZI
28		**1**		1	
29		**1**		1	TANZA ZANZI
30		**1**		1	TANZA ZANZI
31	**MAMLAKA YA MAJI**	**2**	1	3	TANZA ZANZI

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NCH
38		**2**	1	3	TANZA ZANZII
32		**2**	1	3	TANZA ZANZII
33		**1**		1	TANZA ZANZII
34			1	1	TANZA ZANZII
35		**1**		1	TANZA BARA
36		**1**		1	TANZA BARA

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NC
37			1	1	TURKI
38		**1**		1	INDIA
39	**MAHKAMA YA ARDHI**	**1**		1	TANZA ZANZI
40		**1**		1	TANZA ZANZI
41			1	1	TANZA ZANZI

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NCI
42	**AFISI KUU PEMBA**	**1**		1	TANZIA
43		**1**		1	TANZIA
44		**1**		1	TANZIA
45			1	1	TANZIA
46		**1**		1	TANZIA
47		**1**		1	TANZIA

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NC
48		**1**		1	TANIA
49		**1**		1	TANIA
50			1	1	TANIA
51		**1**		1	TANIA
52			1	1	TANIA

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NCI
53			1	1	TANZIA
54			1	1	TANZIA
55		**1**		1	TANZIA
56			1	1	TANZIA

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NO
57		**1**		1	TANIA ZANAR
58		**1**		1	TANIA
59			1	1	TANIA
60		**1**	1	2	TANIA
61		**1**		1	TANIA

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NCI
62		**1**		1	TANZIA
63		**1**		1	TANZIA
64		**1**		1	TANZIA
65		**1**		1	TANZIA
66		**1**		1	TANZIA

S/NO	TAASISI	W/UME	W/WAKE	JUMLA	NO
JUMLA		**49**	**26**	**75**	

KIAMBATANISHO "D2"

WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MUDA MFUPI KWA KIPINDI CHA JULAI 2012 – MACHI 2013

S/NO	TAASISI	AINA YA MAFUNZO
1	IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI	DRIVING
3	IDARA YA NISHATI NA MADINI	RENEWABLE RURAL ENVIROMENT AND HYGIEN OFFICIALS FROM DEVELOP COUNTRIES
4	IDARA YA UJENZI	EMPLOYMENT LAW
5		ELETRIFICATION ON RURA AREA IN DEVELOPING COU
6	MAMLAKA YA MJI MKONGWE	KUPUNGUZA UMASIKINI V
7		RASILIMALI WATU
8	MAMLAKA YA MAJI	ZIARA YA MAFUNZO YA RASILIMALI YA MAADINI
9		ARUTI

10		UTUNZAJI WA KUMBU KU
11		STUDY TOUR
12		ADV.SOFTWARE
13		ZAWA CAPACITY BUILDIN
14		ZAWA CAPACITY BUILDIN
15		LIKAGE DETECTION
16		PUMP & OPERATION
17		WATER METER READING

S/NO	TAASISI	AINA YA MAFUNZO
18	**SHIRIKA LA UMEME**	ELECTRICAL ARTISANS C
19		CLEAN ENERGY APPLICAT TECHNOLOGY
20		EFFICIENT ENERGY USE A PLANNING
21		WIND POWER DEVELOPM USE
22		PLANNING AND MANAGE POWER TRASMISSION AN DISTRIBUTION SYSTEM
23		MONITORING AND EVALU DEVELOPMENT PROJECT
24		MICROSOFT INFORMATIO TECHNOLOGY PROFFESSI
25		SECRETARIAL SKILLS
26		ADVANCED DRIVERS GRA
27		NJIA BORA ZA KUFANIKIS ZA UKATAJI UMEME KWA WENYE MADENI (ON JOB TRAINING)
	JUMLA KUU	

KIAMBATANISHO “D3”

TAARIFA ZA WAFANYAKAZI
WALIOSTAAFU KAZI 2012/2013

TAASISI	WALIOSTAAFU KWA KUFIKIA UMRI WA MIAKA SITINI (60)	
IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI		
IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI	2	-
IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI	-	-
IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI	1	-
IDARA YA ARDHI NA USAJILI	2	-
IDARA YA NYUMBA NA MAKAAZI	1	1
MSAJILI WA ARDHI	-	-
MAMLAKA YA MJI MKONGWE	2	-
IDARA YA NISHATI NA MADINI	-	-
IDARA YA UJENZI	14	2
SHIRIKA LA UMEME	20	2
MAMLAKA YA MAJI	15	-
PEMBA	9	1

JUMLA	**66**	

KIAMBATANISHO "E"

MAENEO YALIOPIMWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2012 – MACHI 2013

PEMBA

MAKAAZI			**HUDUMA/MAKAA**	
PAHALA	**WILAYA**	**IDADI**	PAHALA	**WILA**
Wara	ChakeChake	5	Madungu	ChakeC
Michakaini	ChakeChake	2	Kilindi	ChakeC
Mkungu Malofa	ChakeChake	1	Kwale	ChakeC
Madungu	ChakeChake	8	Chambani	Mkoan
Kwale	ChakeChake	10	Mkoani Mjini	Mkoan
Chonga	ChakeChake	3	Mkanyageni	Mkoan
Tibirinzi	ChakeChake	1	Kangani	Mkoan
Chanjaani	ChakeChake	1	Makangale	Michev
N'gambwa	ChakeChake	3	Konde	Michev
Mguye	ChakeChake	2	Machomane	ChakeC
Ndagoni	ChakeChake	1	Kengeja	Mkoan

Macho mane	ChakeChake	8	Kiwani	Mkoa
Msingini	ChakeChake	3	Shengejuu	Wete
Mkoroshoni	ChakeChake	1	Konde	Miche
Wawi	ChakeChake	10	Micheweni	Miche
Mkanjuni	ChakeChake	1		
Gongomawe	ChakeChake	1		
Kichungwani	ChakeChake	1		
	ChakeChake	3		
Uweleni	Mkoani	1		
Mzingani	Mkoani	3		
Mkoani Mjini	Mkoani	15		
Kengeja	Mkoani	2		
Mbuguani	Mkoani	1		
	Mkoani	8		
	Micheweni	92		
	Wete	58		
JUMLA		**245**		

UNGUJA

MAKAAZI			**HUDUMA/MAKAAZ**		
PAHALA	**WILAYA**	**IDADI**	**PAHALA**	**WILAYA**	
Amani	Mjini	1	Amani	Mjini	

Bwejuu	Kusini	2	Chukwani	Magharibi	
Fukuchani	Kusini	1	Chwaka	Kati	
Fuoni	Magharibi	1	Jumbi	Kati	
Jambiani	Kusini	1	Mazizini	Mjini	
Kama	Magharibi	1	Masingini	Magharibi	
Kiwengwa	Kaskazini B	1	Tunguu	Kati	
Kiwengwa	Kaskazini B	4	Kiwengwa	Kaskazini B	
Marumbi	Kati	1	Kibweni	Magharibi	
Dimani	Magharibi	1	Mitondooni	Magharibi	
Fuoni	Magharibi	2	Nungwi	Kaskazini A	
Jambiani	Kusini	2	Jozani	Kusini	
Kendwa	Kaskazini A	1	Kibele	Kati	
Kibele	Kati	2	Mkele	Magharibi	
Kisauni	Magharibi	1	Tunguu	Kati	
Kiwengwa	Kaskazini B	2			
Kizimkazi	Kusini	1			
Maungani	Magharibi	2			
Mbunzini	Magharibi	1			

Mbweni	Magharibi	1			
Michamvi	Kusini	1			
Mkanyageni	Magharibi	1			
Mto wa Pwani	Kaskazini B	1			
Mtoni	Magharibi	1			
Mtufaani	Magharibi	6			
M/makumbi	Mjini	1			
M/tanga	Mjini	1			
Nungwi	Kaskazini A	2			
Shakani	Magharibi	2			
Tazari	Kaskazini A	4			
Tunguu	Kati	44			
Uroa	Kati	3			

JUMLA		**96**			1

KIAMBATANISHO "F"

USIMAMIZI NA UKARABATI WA MAJENGO NDANI YA MJI MKONGWE KWA KIPINDI CHA JULAI 2012 – MACHI 2013

UKARABATI WA JENGO	**FEDHA KUTOKA MWEZI WA JUNE (Opening Balance)**	**FE ILIOP EV**
IKULU	31,269,770	0
BARAZA LA MAPINDUZI	38,266,332	197,74
JENGO LA IDARA ZA ARDHI	4,788,600	19,457,
JENGO LA "SULTANI PALACE" LILIOPO FORODHANI	0	14,033,
BEIT-EL-ALJAIB	0	30,000,

KUSIMAMIA UJENZI WA UKUTA (FENCE) WA CHUO CHA MAFUNZO HANYEGWA.	2,000,000	20,000
KUSIMAMIA UJENZI WA CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TUNGUU	0	13,950
TUMEKUJA, FORODHANI NA HAMAMNI	0	0
UKARABATI WA NYUMBA NAMABARI 2351-2353 SOKOMUHOGO.	0	0
KUIHAMI NYUMBA NAMBARI 1220 KOKONI.	0	0
JUMLA	**76,324,702**	**295,18**

KIAMBATANISHO "G"

TAKWIMU ZA UJENZI KATIKA ENEO LA MJI MKONGWE

ENEO	MATENGENEZO MADOGO	MATENGENEZO MAKUBWA	UJENZI MPYA	MAOYALI TALI
Malindi	7	4	6	2
Mkunazini	5	2	-	-
Forodhani	2	2	1	-
Kiponda	5	3	2	-
Shangani	6	15	3	-
Vuga	1	3	-	-
Sokomuhogo	5	1	1	-
Kajifichen i	2	1	-	-
Darajani	3	1	-	-

Jumla	**36**	**32**	**13**	**2**

KIAMBATANISHO "H"

MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU 2012/2013

i. Kuba dilisha mabomba ya *asbestos* na kuweka mengine mapya katika maeneo Amani CCM, Viwanda Vidogo Vidogo, Welezo, Mpendae, Sebleni kwa Wazee, Magomeni, Amani Roundabout, Kwamtipura, Mwembe Mchomeke, Kianga, Chunga, Amani, Mbweni, Daraja Bovu, Meya, Kijito Upele, Maruhubi, na Kilimani. Pia imebadilisha mambomba yaliyopasuka na kuweka mengine mapya katika maeneo ya Mkwajuni na Tingatinga, Micheweni na Kwapweza.

ii. Mare kebisho ya umeme katika visima viwili vya Chumbuni, Chunga namba 009, Mwembe Mchomeke

namba 001, Kiboje, Kigunda, Pangeni, Mwembe Mchomeke namba 13, Unguja Ukuu, Nungwi Kae, Kilindi, Kiashange, Kianga, Machui N8, Makoba, SEMUSO, Mgeni Haji, Ukongoroni, Mombasa, Jendele, Tazari, Bweleo, Mwembe Makumbi, Mtende, Baraza la Wawakilishi, Chaani Kubwa, bumbwisudi, Chemchem ya Machui, Uwanja wa Ndege, Hali ya Hewa, Kaburi Kikombe, Kwarara, Kianga N9-2, Dole, Dunga S. S. Mehta, Welezo, Paje Mwanakwerekwe Masumbani, Chukwani, Selem na Mfenesini, Masipa, Michenzani 4, Darajani, Kiungoni, Kijuki, Daya, Kwapweza, Kwa Sharifuali 2, Kwa Sharifuali 3, Tosa 1, Jamvini, Ng'ambwa 1, Kironjo A na Kironjo B.

iii. Ununuzi na ubadilishaji wa pampu na mota zilizoungua katika

visima vya Chunga 009, Mwembe Mchomeke 001, Kitope, Bumbwisudi, Kaburi Kikombe, Dimani, Bweleo, Chwaka, Baraza la Wawakilishi, Miwani, Nungwi/Tazari, Chaani Kubwa, Kibuteni, Kigongoni, Chumbuni 001, Chumbuni 002, Machui, 001, Welezo 002, Umbuji, Uwanja wa Ndege, Kaburi Kikombe U-10, Kaburi Kikombe U-002, Migombani Jeshini, Welezo na Ole Skuli, Kangani 1, Wesha, Sharifuali 2, Sharifuali 3, Kijuki na Michenzani 1.

KIAMBATANISHO "I"

MAENEO YALIOPATIWA ELIMU KWA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA MAJI KWA KIPINDI CHA JULAI 2012 – MACHI 2013

S/N	ENEO	S/N	ENEO
1.	Bambi,	26.	Kitope
2.	Bumbwini,	27.	Kizimkazi
3.	Bwejuu,	28	Mahonda
4.	Chaani Kubwa,	29	Makoba
5.	Chaani	30	Mangapw

	Masingini,		
6.	Dunga Bweni,	31	Marumbi
7.	Dunga Kiembeni	32	Mfenesini
8.	Donge Mbiji,	33	Misufini
9.	Donge Mtambile,	34	Mkwajuni
10.	Donge Pangamauwa	35	Mpapa
11.	Fujoni,	36	Mtende Makunduc
12.	Gamba,	37	Muanda
13.	Jambiani	38	Muungoni
14.	Jendele	39	Muyuni
15.	Kandwi	40	Moga
16.	Kama	41	Ndijani
17.	Kae Pwani	42	Nungwi
18.	Kaebona	43	Paje
19.	Kiboje	44	Pwani Mchangan
20.	Kibuteni	45	Tindini
21.	Kidimni	46	Ubago
22.	Kilindi	47	Ungujauk
23.	Kilimani		
24.	Kilombero		
25.	Kitogani		

KIAMBATANISHO "J"

MAENEO YATAKAYOFAIDIKA NA MRADI WA UCHIMBAJI WA VISIMA 50

S/N	Project/scheme
A.	**UNGUJA:**
	MKOA WA MJINI MAGHAR
1	Welezo Wateworks
2	Kinuni Waterworks
3	Dole Waterworks
4	Migombani
5	Kianga
6	Mtoni
7	Chumbuni
8	Masingini
	JUMLA NDOGO (MJIN MAGHARIBI
	MKOA WA KASKAZINI UNGUJA
8	Chwaka
9	Michamvi
10	Makunduchi
11	Jumbi kibonde Mzungu
12	Bambi
13	Jendele-Marumbi-Chwaka
14	Tunguu - Kibele
15	Cheju
16	Mzuri
17	Mtende
18	Mwera - Pongwe
19	Kiboje
20	Fuonikibondeni
21	Makunduchi Desalination

	JUMLA NDOGO (KASKAZ
	MKOA WA KUSINI UNGUJA
22	Kijini
23	Bandamaji
24	Upenja - Kiwengwa
24	Majimekundu
26	Kisongoni
27	Moga
28	Kitope
29	Kidanzini
30	Donge
	JUMLA NDOGO (KUSI
B.	**PEMBA:**
	MKOA WA KUSINI
1	Kilindi
2	Kiwani
3	Ukutini
4	Mahuduthi
	Chonga
	JUMLA NDOGO
	MKOA WA KASKAZINI
	Shumba Viamboni
5	Mgogoni
6	Konde
8	Wingwi
9	Kangagani
	JUMLA NDOGO
	JUMLA KUU

KIAMBATANISHO "K"

TAKWIMU ZA MAFUTA YALIOINGIZWA NCHINI KUANZIA JULAI 2012 HADI MACHI 2013

UNGUJA				
		PETROL	**DIESEL**	**KEROSINE**
JULAI	2012	2,004,315	3,637,307	213,485
AGOSTI	2012	1,588,319	4,144,751	838,781
SEPT	2012	2,999,635	890,991	-
OCT	2012	2,636,613	2,305,792	384,117
NOV	2012	2,475,619	2,079,959	525,080
DISE	2012	4,230,814	1,882,015	74,048
JAN	2013	2,520,967	2,812,906	485,080
FEB	2013	721,961	3,037,929	872,163
MACH	2013	3,530,949	3,260,727	768,831
JUMLA		**22,709,192**	**24,052,377**	**4,161,585**

KIAMBATANISHO "L"

VIJIJI VILIVYOPATIWA HUDUMA YA UMEME KUPITIWA MRADI WA USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

UNGUJA	
VIJIJI	**GHARAMA TSH.**
Bumbwi Sudi Umwagiliaji maji	18,313,690
Bumbwi Sudi	6,000,0
Cheju	12,548,8
Dole Kianga	45,120,3
Fuoni Kidarajani	21,606,0
Kama	74,697,9
Kianga Kiamba Ngoma	16,564,5
Kianga kidarajani	27,337,5
Kibonde Maji (Koani)	117,977,0
Kijichi	
Mtwango - Pongwe	115,477,0
Matemwe Mkunguni	40,304,7
Mkanyageni	98,310,0
Masingini	8,568,25
Tunguu Dispensari	74,284,0
Tunguu Mji mpya	3,770,0
Pangani	16,712,1

JUMLA	**774,706,5**

KIAMBATANISHO "M1"

MUHTASARI WA MAKISIO YA MATUMIZI KWA WAMMN 2013 – 2014

KIFUNGU	MAELEZO	M 201 K KA
03	AFISI KUU PEMBA	1,123,
04	IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI	2,384,
05	IDARA YA UJENZI	584,55
07	MAMLAKA YA MJI MKONGWE	299,29
08	IDARA YA NISHATI NA MADINI	735,80
9	IDARA YA ARDHI NA USAJILI	312,25
10	IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI	355

11	IDARA YA NYUMBA NA MAKAAZI	251,8
12	MAHAKAMA YA ARDHI	190,6
13	IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI	781,5
14	MSAJILI WA ARDHI	190,9
15	IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI	309,5
	JUMLA	**7,51**

KIAMBATANISHO "M2"

MUHTASARI WA MAKISIO YA MAKUSANYO YA MAPATO KWA WAMMN 2013/2014

KIFUNGU	MAELEZO	MAKISIO
03	AFISI KUU PEMBA	106,000,000.00
05	IDARA YA UJENZI	9,700,000.00
07	MAMLAKA YA MJI MKONGWE	24,000,000.00
09	IDARA YA ARDHI NA USAJILI	3,505,000,000.00
10	IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI	70,000,000.00
11	IDARA YA NYUMBA NA MAKAAZI	325,000,000.00

	JUMLA	**4,039,700,000.00**

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Ahsante Mhe. Spika, kwa asubuhi ya leo kuweza kunikiaribisha hapa ili niweze kusoma hotuba ya Makadirio ya Mapato ya Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi ikiwa hii ni mara ya kwanza kwa kusoma hotuba hii nikiwa kama Mwenyekiti wa Kamati hii. Mhe. Spika, Naomba nichukue fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambae ametujaalia kukutana leo katika chombo hiki muhimu cha uwakilishi wa wananchi ili niweze kufika na kujadili mambo mbali mbali muhimu kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, nitakuwa mwngi wa fadhila iwapo sitakushukuru wewe, kwa msaada na maelekeo wako kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ili iweze kufanikisha kazi zake za kila siku.
Mhe. Spika, pia naomba kwa heshima niwashukuru wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao yenye tija na yenye lengo la kuimarisha ufanisi wa utendaji waliyoitoa wakati wa kujadili makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.
Mhe. Spika, naomba niwatambue wajumbe hao kwa kuwataja majina kama ifutavyo:-

1.	Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdullah	Makamo Mwenyekiti

3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Mjumbe
4.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	“
5.	Mhe. Mohammed Haji Khalid	“
6.	Mhe. Salma Mohammed Ali	“
7.	Mhe. Marina Joel Thomas	“

Kamati yetu pia ina Makatibu wawili, ambao ni

1. Ndg. Latifa Saleh Suleiman
2. Ndg. Himid Haji Choko

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kutoa maoni ya Kamati kuhusiana na makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ningependa kutoa mkono wa pole kwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na wafiwa wote wa marehemu waliopata ajali ya kuangukiwa na mnara wa tangi la maji huko Pemba hivi karibuni. Tuwaombee kwa Mwenyezimungu awape subira katika kipindi hiki kigumu na wenzetu hao waliotangulia mbele ya haki wapate makaazi mema peponi - Amin.

Mhe. Spika, kwa ujumla Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, na hatimae kutoa maoni yenye lengo la kuimarisha utendaji wa Wizara hiyo. Tathmini ya jumla ya Kamati hii kuhusiana na makadirio hayo ni kama ifuatavyo:

HALI YA MAKADIRIO YA MAPATO

Mhe. Spika, makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2013/2014 yamepunguwa kwa kiasi kidogo, ukilinganisha na makadirio ya mwaka 2012/2013 ambapo mwaka jana yalikuwa ni shilingi 4,092,000,000 na mwaka huu ni shilingi 4,039,700,000.

Kamati inaamini hili limetokana na ukweli kwamba, lengo la mwaka 2012/2013 halikufikiwa kwa vile vyanzo vingi vya mapato vilivyotegemewa na Wizara hii havikuwa katika hali nzuri. Mfano wa vyanzo hivyo ni kama vile viwanda vya kuzalisha kokoto na viwanda vya useremala (kwa Pemba), mauzo ya nyumba za Serikali na kodi za nyumba zote kwa ujumla.

Hivyo basi, Kamati inashauri Wizara kuviboresha vyanzo hivi vizidi kuzalisha zaidi. Si hivyo tu, lakini pia hali hii imesababishwa na madeni makubwa wanayodaiwa wananchi na taasisi za Serikali ambao wamekodi nyumba za Serikali, ambapo ulipaji wake sio wa kuridhisha.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Wizara kulipatia ufumbuzi suala hili kwa kutafuta njia mbadala zitakazowezesha kuhusisha wahusika kulipa madeni yao ili kuongeza mapato ya Serikali.

HALI YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA

Mhe. Spika, makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, yameonesha ongezeko kidogo ambapo jumla ya bilioni 7,519,000,000 zimekisiwa ikiwa ni kiwango kikubwa ukilinganisha na shilingi bilioni 6,707,000,000 za mwaka wa fedha wa 2012/2013. Kamati inaamini

kwamba ongezeko hili litasaidia sana ufanisi na utendaji wa kazi katika kufikia malengo ambayo Wizara yenyewe imejiwekea.

HALI YA MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO

Mhe. Spika, katika suala zima la makadirio ya matumizi kwa Fedha za Maendeleo kwa mwaka huu wa fedha (2013/2014) kumekuwa na ongezeko kidogo la makadirio hayo kwani kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2013, jumla ya fedha zote zilikuwa ni 46,849,750,000 wakati mwaka huu tunaoenda nao makadirio ni shilingi 69,721,030,000.
Mhe, Spika, kupatikana kwa fedha hizi ni faraja kubwa kwani matumizi mazuri ya fedha hizi yataweza kuleta matumaini mapya kwa ile miradi ambayo kipindi kilichopita haikufanyika kwa ufanisi mkubwa. Ni imani yetu kwamba juhudi za makusudi zitachukuliwa na Wizara katika kuisimamia miradi hiyo ili iendelee kuleta tija kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, dhima ya Wizara hii ni kubwa mno, kwa ustawi wa wananchi wetu. Sote tungependa wananchi wetu waishi kwenye nyumba nzuri na zinazoendelea kutunzwa. Tunatarajia sana nyumba zetu zitaendelea kuwa katika hali nzuri kwa kukarabatiwa mara kwa mara, nalo hili liwape moyo wapangaji wetu, hivyo, tunaiomba Wizara izingatie kwa upana wake nyumba za Kengeja na Mtemani.

SEKTA YA UTAWALA

Mhe. Spika, suala la uendelezaji wa watendaji kwa kuwapatia mafunzo kwenye fani mbali mbali ni muhimu, kwani ndilo linalosaidia kuweza kuwa na wataalamu ambao ndio watakaoleta mabadiliko ya kweli katika kuleta maendeleo ya Wizara na Taifa kwa ujumla.

Hivyo, Kamati yangu inaitaka Wizara kulipa msukumo wa kipekee jambo hili.

SEKTA YA ARDHI

Mhe. Spika, ni imani ya kila mwanadamu kwamba, ardhi ni rasilimali muhimu katika maisha yetu. Tunaitegemea sana kwa kilimo na ujenzi. Ni ukweli kwamba eneo la ardhi tulilonayo ni dogo kuliko mahitaji yetu. Hivyo ni vyema Serikali kuwa na mipango na mikakati mahususi ya kuitunza na kuitumia kwa tahadhari kubwa ili wananchi wote waweze kufaidika na rasilimali hii ndogo tuliyonayo.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imechukua hatua mbali mbali katika kuona kwamba kuna mgawanyo mzuri wa ardhi, ikiwa ni pamoja na kuipima, kuifanyia usajili, kupanga miji na vijiji na kuihifadhi miji ya kihistoria. Yote haya yanafanyika ili kuitunza na kuihifadhi vyema rasilimali hii. Hatimae kumeanzishwa pia na Mahakama ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata haki yake ya matumizi ya ardhi.

Hata hivyo, Mhe. Spika, Mahakama **hizi** zinakabiliwa na changamoto nyingi zinazosababisha kushindwa kufanya kazi ipasavyo, kuna upungufu wa Mahakimu , hali inayopelekea Hakimu mmoja kufikia kupangiwa kesi 700 jambo ambalo katika hali ya kawaida haliwezekani. Hivyo, Kamati inaziomba

Mamlaka zinazohusika kuongeza Mahakimu kadri inavyowezekana ili kuongeza ufanisi katika utatuzi wa migogoro ya ardhi hapa nchini.

Migogoro ya Ardhi

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba migogoro ya ardhi Zanzibar inazidi kuongezeka, licha ya kuwepo mamlaka mbali mbali zinazosimamia hali hii. Uuzaji viwanja mara mbili, watu kuuza maeneo ambayo sio yao, mipaka isiyozingatia uhalali wake iliyowekwa na wamiliki wa maeneo bila kufuata taratibu, uelewa mdogo wa wananchi juu ya taratibu zinazopaswa kufuatwa wakati wa kuuziana viwanja zote hizo ni miongoni mwa sababu zinazochangia migogoro hiyo.

Kwa niaba ya Kamati, tunaiomba Serikali kuliangalia sana tatizo hili kwa kulipatia ufumbuzi kwani utaratibu wa sasa wa wale waliosababisha matatizo ndio wayatatue jambo hili litachukua muda na migogoro ya ardhi hatimae itazua maafa makubwa. Kamati pia inapendekeza kwa Serikali kuyapima maeneo yote ambayo bado hayajajengwa ili kuweka mipaka rasmi, hatua iliyo wazi na ambayo inaweza kueleweka.

Maeneo ya Uwekezaji

Mhe. Spika, kumekuwa na tabia ya baadhi ya wawekezaji kuomba maeneo kwa lengo la kuwekeza, au hata wengine kujichukulia maeneo bila ya kufuata taratibu zilizowekwa. Hata hivyo, maeneo hayo hukaa nayo kwa muda mrefu bila ya kuyaendeleza kwa shughuli yoyote.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaiomba na kuitaka Wizara kuhakikisha kwamba wanawatambua wawekezaji hao na kuwachukulia hatua za kisheria, kwani kuyazuia maeneo hayo bila ya kuyaendeleza na kuikosesha mapato Serikali yetu.
Mhe. Spika, tunapenda pia hatua hizo ziende sambamba na marekebisho ya sheria ya marekebisho ya Umiliki wa Ardhi (*Land Tenure Act*) nam 12, ya 1992 ili kuweza kuendana na mabadiliko ya mahitaji ya ardhi kwa sasa.

Ujenzi holela
Mhe.Spika Kamati inasikitishwa na hali ya mji wa Zanzibar ulivyo kwa sasa, ambapo watu wanajenga bila ya kufuata taratibu za kisheria katika maeneo mbali mbali ya mji wa Zanzibar.

Hali ilivyo hivi sasa ni kwamba, hata jitihada za kufikisha huduma muhimu katika maeneo mbali mbali wanayoishi watu hazitawezekana kutokana na ujenzi huo usiozingatia mahitaji hayo muhimu kama vile njia na huduma nyenginezo.
Mhe. Spika, Kamati inaamini kwamba hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwa maeneo mengi ambayo hayakupimwa na hivyo kusababisha wananchi kuuziana viwanja kiholela. Hivyo basi, Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara ilitafutie ufumbuzi tatizo hili kwa kuwa na mpango wa muda mrefu wa kuendeleza Mji wetu ili kuepusha ujenzi holela.

Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mpango wa muda mrefu wa kuigawa ardhi ya Zanzibar katika maeneo tofauti kwa mujibu wa mahitaji ya taifa, kwa mfano kuwa na maeneo maalum kwa ajili ya makaazi

ya watu, mukiwa na maeneo ya mapumziko, viwanja vya michezo, maeneo ya kufanyia ibada, huduma za jamii za afya na elimu, maeneo maalum ya viwanda, uwekezaji na maeneo kwa ajili ya kilimo.

SEKTA YA MAKAAZI

Mhe. Spika, sekta hii ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuwaletea wananchi maendeleo. Hii ni kwa sababu, katika jamii yetu makaazi mazuri ni kigezo kimoja wapo cha utu wa mtu na hadhi yake. Hivyo basi kila mwananchi angependa kuwa na makaazi bora na mazuri yenye hadhi ya kibinadamu.

Mhe .Spika, kwa kulielewa hili, Rais wetu wa awamu ya kwanza marehemu Mzee Abeid Amani Karume alifanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba hata wale wananchi wenye kipato cha chini nao wanapata makaazi yaliyo bora. Katika kulitimiza hili, nyumba nyingi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba zilijengwa mijini na vijijini na kupewa wananchi.

Mhe. Spika, inasikitisha kuona jitihada zote za Serikali ya awamu ya kwanza za kuwapatia wananchi makaazi bora hazikuendelezwa ipasavyo. Hii ina maana kwamba hakukuwa na ushughulikiaji na utunzaji mzuri wa kuzibakisha kwenye hadhi yake nyumba hizo.

Mhe Spika, tunapenda kuishauri Serikali kupitia Wizara hii, ijitahidi katika kuhakikisha kwamba nyumba hizi zinatunzwa na ikiwezekana kujengwa na nyengine mpya ili kuwapunguzia mzigo wa maisha wananchi wa Zanzibar.

Nyumba ya Maendeleo - Kengeja

Mhe. Spika, Kamati yangu ilipata fursa ya kwenda kuiona nyumba ya Maendeleo ya Kengeja, na kujionea hali halisi ilivyo. Kwa kweli nyumba haifai kuishi binadamu kutokana na ubovu, uchakavu na uchafu uliomo katika nyumba hiyo.

Mhe. Spika, katika bajeti hii ya mwaka 2013/2014, mradi wa kuifanyia matengenezo nyumba hiyo umetengewa shilingi milioni 200 ambazo zinatarajiwa kutumika kwa kuiezeka ili isiendelee kuathirika kwa maji ya mvua.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati, tunapenda kuchukua fursa hii kuishauri Serikali kuitizama kwa umakini mkubwa nyumba hiyo kwa sababu inahitaji matengenezo makubwa na ya haraka sana.

Uanzishwaji wa Shirika la Nyumba

Mhe. Spika, tunapenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kwa kuja na wazo zuri la kuanzisha Shirika la nyumba ambalo litasaidia katika kujenga, kutunza na kuzisimamia nyumba za Maendeleo. Ni matumaini ya wananchi walio wengi kwamba, Shirika hili litakuja kumaliza kilio cha wananchi cha kutokuwa na nyumba bora na za bei nafuu. Vile vile tunaamini Shirika hili litaiongezea Serikali mapato na litatoa ajira kwa vijana wa Taifa letu**.**

Mhe. Spika, Kamati inaiomba Wizara kumalizia hatua zilizobakia ili kulianzisha Shirika hili, rasmi.

Udhibiti wa Kodi za Nyumba.

Mhe. Spika, ni hali ya kusikitisha kuona kwamba kodi inayokusanywa kutoka katika nyumba za Serikali ni ndogo kutokana na kuwepo wananchi wanaokataa kulipa kodi hii kwa vizingizio vya kwamba nyumba hizo walipewa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Kamati inaamini kwamba Wizara inalishughulikia hili na itakuja na majibu ya kuridhisha katika Baraza lako hili tukufu. Majibu ambayo yatabainisha ukweli ulivyo, nani anastahiki na asiyestahiki kulipa, na kwa nini. Huu ni wajibu wa moja kwa moja kwa kila anayepanga nyumba hizo ni lazima alipe kodi.

Uhifadhi wa Nyumba za Mji Mkongwe

Mhe. Spika, kumejitokeza wimbi la watu kuzigeuza nyumba za Mji Mkongwe kuwa mahoteli, hali inayohatarisha kupotea kwa mandhari ya mji huo na cha kusikitisha zaidi ni kwamba Mamlaka inayosimamia utalii inatoa vibali hivyo bila ya kujali athari hiyo.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kulidhibiti hili ili kuweza kuuwacha mji huo katika hali yake ya asili jambo ambalo ndio kivutio kikubwa kwa watalii.

SEKTA YA MAJI

Mhe. Spika, sote tunafahamu kwamba maji ni uhai, hivyo ni muhimu katika shughuli zote za mwanadamu. Hivyo, Kamati yangu inaipongeza Mamlaka ya Maji (*ZAWA)* kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana kwa uhakika mijini na vijijini.

Chimbuko la Tatizo la Maji Mjini

Matumizi ya maji katika Mji wa Zanzibar yanatokana na vianzio vikuu viwili vilivyopo Mwanyanya na Mtopepo, maji yake hutiririka kutoka chemchem hizi na kuingia katika matangi ya Saateni kwa kuyatia dawa na kuyapeleka kwa wananchi kwa matumizi yao.

Ikumbukwe kwamba chemchem hizi mbili ni za zamani sana ambazo zilihifadhiwa tokea enzi za serikali ya ukoloni hadi sasa ikiwa maeneo makuu ya makinga maji *(Catchment areas*) nchini, chemchem hizi zilikuwa zikifanya kazi vizuri kwa kutosheleza wakaazi wa mjini kutokana na uzalishaji wake mzuri na mahitaji madogo ya wakaazi wa Mjini kwa wakati ule. Tatizo kubwa la upatikanaji wa huduma ya maji Mjini, umesababishwa zaidi na mabadiliko ya tabia nchi yaliyotokana na uvamizi mkubwa wa wananchi katika maeneo ya mavuno haya ya maji, sambamba na ongezeko kubwa la mahitaji linalotokana na idadi kubwa ya wakaazi wa maeneo ya Mjini, harakati za kibiashara na kiuchumi pamoja na wageni wanaoingia na kutoka kwa shughuli mbali mbali ukilinganishwa na uzalishaji mdogo. Aidha, ujenzi wa nyumba usiofuata utaratibu ni miongoni mwa mambo yanayochangia kwa kiasi kikubwa kupunguza uzalishaji wa maji ambayo ni matatizo ya upatikanaji wa huduma hii muhimu.

Hatua za Kukabiliana na Mapungufu ya Maji Mjini

Hata hivyo tunaipongeza sana serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Maji kwa kubuni mradi maalum wa uchimbaji visima tisa (9) vipya Mjini ambapo kwa sasa jumla ya visima vitano(5) vimeshachibwa, viwili Saateni na vitatu Chumbuni kwa kulifanya eneo hilo kuwa ni vianzio vya maji vitakavyopunguza au kuondosha kabisa mapungufu ya uzalishaji katika chemchem za Mwanyanya na Mtoni, hali ambayo imepelekea hali ya maji kuimarika kwa kiasi kikubwa kama inavyoonekana katika maeneo ya Malindi, Forodhani, Shangani, Michenzani, Miembeni, Kijangwani, Kikwajuni, Makadara na maeneo mengine ya jirani.

Mhe. Spika, Kamati yangu inapenda kutoa tahadhari kwa Wizara kuhusu kuvihifadhi kwa kuviwekea uzio vyanzo vya maji ili kuepusha uharibifu na uvamizi wa maeneo hayo. Lakini pia Wizara ihakikishe maeneo yote yenye vianzio vya maji yanapatiwa hati miliki kwa lengo la kuvihifadhi.

Jambo jengine, Mhe. Spika, tunawaomba wananchi ambao wanapata huduma ya maji basi wawe wanalipa ili kuendeleza huduma hiyo iendelee kwao lakini pia iwafikie wengine.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada hizo za Mamlaka kutoa huduma ya maji, bado kuna kilio kwa wananchi walio wengi kutokana na upungufu wa maji hasa katika maeneo ya mjini. Hivyo, Kamati inazidi kuisisitiza Mamlaka kuongeza juhudi kwa ajili ya kuwafikishia wananchi huduma hii muhimu.

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Spika, Kamati yangu inalipongeza Shirika la Umeme kwa kukamilisha mradi wa njia ya pili ya umeme Unguja ambao ulizunduliwa rasmi tarehe 10 April, 2013 na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein. Mradi huu kwa kiasi kikubwa umepunguza tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara hapa Unguja na kumaliza tatizo la mgao wa umeme uliodumu kwa muda mrefu nchini kwetu.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme linakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo endapo zitatatuliwa, Shirika hilo linaweza kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na madeni ya wateja ambapo mpaka kufikia mwezi wa Febuari 2013 Shirika lilikuwa likidai jumla ya shilingi 22,933,063,610.27 kwa taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar , taasisi za Serikali ya Muungano na kwa wateja binafsi.

Mhe. Spika, ili kuondokana na tatizo hili tunawaomba wateja wote kulipia umeme tena kwa wakati. Kamati pia inalitaka shirika kuharakisha kazi za ufungaji wa mita za TUKUZA kwa awamu na hatimae kwa wateja wote pamoja na kuhakikisha kazi hiyo inakamilika mwaka huu wa fedha wa 2013/2014 angalau kwa kiwango kikubwa. Hatua hii itasaidia kupata fedha zinazodaiwa kwa wateja wa shirika.

Mhe. Spika, Kamati pia inalipongeza Shirika la Umeme Ofisi ya Pemba kwa kuiondoa *transfomer* ya Sokoni Chake-Chake kama ilivyoagizwa na Kamati, kwani ilikuwa ni tatizo kubwa kwa usalama wa wafanya biashara na wananchi wa sehemu hiyo

Mhe. Spika, Mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikitoa maoni ya Kamati ya Mawasilano na Ujenzi kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Aidha napenda kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako kuichangia na hatimae kuipitisha.

Mhe. Spika, Kamati inaliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 7,519,000,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 69,721,030,000 kwa kazi za maendeleo. Kamati inaamini kwamba kupatikana kwa fedha hizo Wizara itaweza kutekeleza kazi, majukumu na malengo waliyojipangia kwa kipindi cha mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni, naunga mkono hoja hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru sana Ramadhani hii ya leo na mimi kuweza kuchangia. Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa tisa katika Idara ya Ardhi na Usajili.

Mhe. Spika, Idara ya Ardhi na Usajili hapa ndio penyewe na hapa mara nyingi sana ndio hutokea matatizo ya hapa na pale. Lakini vile vile Mhe. Spika, tumeoneshwa hapa jinsi gani Idara hii ilivyokuwa inakusanya vianzio vya viwanja na kukodishwa vya ardhi ambayo kwa jumla kama hiyo inavyokadiriwa kukusanya

hadi kufikia miezi kama hiyo. Niipongeze sana kwa jitihada hizo na kuonesha umahiri wake katika utekelezaji. Lakini vile vile nimemwambie Mhe. Waziri kuwa kuna watu ambao huwa wana mchezo mara kwa mara katika kuomba muda wa kuongeza ile wanaita *extension* ya mambo ya kodi hiyo, naomba mara hii Mhe. Waziri usikubali tena kwa sababu hawa watu wanakuwa wanacheza-cheza mara kwa mara ili tusiweze kupata makodi.

Mhe. Spika, katika kuendelea kuichangia Wizara hii, tahadhari ambazo za mhusika niseme ama ni Mkurugenzi wa Idara hii. Mara nyingi sana Idara hizi ndio zinazosababisha migogoro ya ardhi katika wananchi wetu na kupitia hata wakubwa wenyewe nao hutumia sana njia hizi au sehemu hii ili kuweza kumpa kazi kubwa Mhe. Waziri, ili aonekane kuwa ana mapungufu fulani katika utendaji kumbe taratibu zinapoanzia ni sehemu kama hizi.

Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kuwa hawa viongozi ambao wanaopenda sana kupora hizi ardhi za wananchi na kuziuza, sijui Mhe. Waziri kutakuwa na utaratibu gani ambao au hatua dhidi yake ameweza kuzichukulia hatua kwa watu wa aina kama hii, hilo nimuombe kidogo aweze kunipa *challenge* hiyo ya kumuuliza suala hili. Lakini vile vile niweze kumwambia Mhe. Waziri na kumsifu hapa kuwa nimshukuru sana na wale ambao viongozi waliorejesha ardhi niwashukuru sana wametekeleza ile amri ambayo tulikuwa tukisema Wajumbe wa Baraza hili wa *back benchers* wamerudisha lakini kwa hatua ambayo sio kubwa sana lakini hatua nzuri inaridhisha, hata imempa wakati mzuri Mhe. Waziri kuweza kufuta na amefuta katika ujasiri ambao ni mgumu sana, kwa sababu leo kumuona kiongozi ambaye anamjua na akaweza kumfuata bila ya kumtizama usoni, hiyo nayo nampa hongera sana na ajitahidi kama

alivyotueleza katika kipindi kilichopita alisema tumuachie na tutaona matunda yake, matunda tumeyaona kwa kweli.

Mhe. Spika, vile vile ninamuomba sana hapa aendelee kuwapa wale wahusika au wenye sheria ambao walionyang'anywa kwa mujibu wa taratibu ni kinyume na sheria, naomba sana awaite, awaelekeze na awape ili waweze kufuata taratibu za utekelezaji. Lakini vile vile Mhe. Waziri, tahadhari nyengine ya mhusika Mkurugenzi hapa kulikuwepo na kiwanja ambacho kiliwahi kufutwa na yule ambaye alifutiwa alifanya ubadhirifu wa kufoji hati mpaka saini ambao ni kosa la jinai, saini ya Wakili, namuomba sana huyo mtu aachane naye wala asimsogelee kabisa atamuweka pabaya, kwa sababu yule mtu alifoji majina ya watu, saini za watu, alifoji hata yule wakili ambaye kwa upande aliyekuwa akiwasimamia alifoji saini zake. Naomba sana hili namtahadharisha sina haja ya kumtaja yeye mwenyewe atakuwa kishamjua, naomba sana aelekee kule kunako sheria asione tabu kuelekea kwenye sheria na akadhalilisha watu waliokuwa hawana sheria. Naomba sana hilo na naamini utatimiza wajibu ambao unatakiwa.

Mhe. Spika, sasa niende katika Mahakama ya Ardhi ukurasa wa 15. Mahakama ya Ardhi nilipokuwa wakati ule ni mwenyekiti kulikuwa na malalamiko mengi sana na sasa hivi nashukuru sana kuwa wameongezwa Mahakimu wengine, naamini sasa hivi matatizo yatapunguka na tutaenda vizuri. Lakini kilio kikubwa ni ma-*assessor* wanachelewa kupata posho lao na posho lenyewe ni dogo, naomba sana Mhe. Waziri hawa ni wazee wetu wanatoka sehemu za mbali, wanafika mjini wanajigharamia, tuwahurumieni jamani, ifike kwa *time* zile posho lao wapewe na hilo posho lenyewe jamani dogo, hebu tuwaongezeeni. Mimi naamini Mhe.Waziri utafanya lile jambo ambalo kwa busara zaidi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa pana *challenge* kubwa katika Mahakama hii kwa sababu Mahakama zetu hizi zina mapungufu ya kupata nyumba ambazo za kuendesha Mahakama yenyewe, lakini naamini hiyo kwa wewe ninavyokufahamu ulivyokuwa katika Utawala Bora wakati ule ulijaribu Mahakama nyingi kuzitengeneza na kuweza kwenda kwa wakati na zimekuwa nzuri sana, na hili naamini Mhe. Waziri utatafuta sehemu ambazo zinahusika ili kuweza kutatua masuala haya.

Mhe. Spika, niingie ukurasa wa 16 katika sehemu ya upimaji. Sehemu ya upimaji nayo nashukuru sana na namshukuru sana Mkurugenzi kwa utendaji wake amekuwa sasa hivi si rahisi kukubalia kama hajaona *physically* kabisa, hilo ni moja ambalo ni zuri na inavyotakiwa viongozi wote lazima asikubali moja kwa moja bila ya kuweza kufuatilia, kama wewe anavyokufuata nyayo zako Mhe. Waziri, Mkurugenzi huyu naye anapita nyayo ile ile, kuwa lazima kwanza aangalie au lazima kwanza amwite yule mtu muhusika ili aweze kufanikisha suala lile. Hivyo natoa pongezi tukubaliane vizuri katika uimarishaji na afuate nyayo aanzie kwa Sheha muhusika na baadae akaangalie sehemu nyengine, na si vibaya kuishirikisha na Halmashauri ili akaone kuwa hapa hapana matatizo hata aweze kuja kupima, namshukuru kwa hilo na aweze kufanya wajibu wake.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 21 Idara ya Mipango na Miji. Hapa kidogo nina kilio kikubwa sana, wana-*delay time* hawa kwa sababu unakuta mpaka mtu anafika kujenga halafu na wao ndio wanakwenda, kwa kweli hili suala Idara hii bado lingali linakwenda *slow* sana, kwa sababu siku hizi kiutaratibu huwezi ukapima mpaka waje wao, sasa wao wanawachelewesha hawa watu wa Idara ya Upimaji na hivi vitu tumesema viende sambamba, Idara ya Upimaji na Idara Mipango Miji waende sambamba ili kuondoa

matatizo haya ya msongamano ya watu kujenga ovyo ovyo na watu kuvamiana katika maeneo ambayo mtu kujenga katika eneo lililokuwa halihusiki kabisa, wakati huo kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti, kuna sehemu nyengine za michezo *open space* utakuta mtu anajenga, lakini sasa yeye anachelewa utakuta watu washajenga. Mhe. Spika, hapa nina masikitiko makubwa sana.

Mhe. Spika, sasa niingie katika Idara ya Majenzi. Idara hii ya Majenzi hapa kuna masikitiko makubwa sana namuomba sana Mhe. Waziri atanisikiliza kwa uzuri zaidi. Idara hii ya Majenzi ilikumbwa na matatizo, ilikumbwa na matatizo ya upotevu wa fedha kiasi cha shilingi 51,000,000/= kama sijakosea kwa sababu sijakuwa na *data* maalum lakini pale kilichojitokeza. Mhe. Spika, kama hajui Mhe. Waziri kama hajui, lakini ningeomba sana kuwa au kuna matatizo kati ya mapungufu ya kukabidhiana hizi Wizara na nafikiria kuna mambo mengine kuna *data* zinafichwa. Kwa mfano Mhe. Spika, kama juzi lilitokea tatizo la vyombo hapa kupotea vya *cancer* Mhe. Waziri, akasema sio yeye wala si wakati wake yeye, lakini utakuta mtu kama yule ndio sasa hivi anaongoza Wizara. Sasa hapa kidogo mimi hupata mashaka kuwa pengine Mhe. Waziri, hilo halijui na kama analijua basi namuomba leo alitekeleze na atizame.

Mhe. Spika, kuna watu ambao wameshutumiwa katika tatizo hili, kuna mwengine ambaye ni *total* kabisa kwa mujibu wa sheria ameingia, hata kipofu hata asiyeona basi akioneshwa zile njia ataona na ataweza kusaidia. Mhe. Spika, amekwenda mtu kupewa kesi ambayo iliyokuwa yeye haikumhusu kabisa wakati kipindi hicho alipewa ruhusa ya kuendelea masomo huko Bara. Sasa huyu mtu ana watoto, wana wazee maskini ya Mungu, kwa kweli bado hajatendewa haki, kwa mujibu wa sheria mtu mwisho miezi sita ili atekelezewe wajibu kwa vyombo vya sheria, lakini huyu mpaka leo hii miezi 11 hii kesi haijenda

Mahakamani wala haijenda, yeye yumo tu na amesimamishwa na Katiba iliyeyopita. Kwa kweli hapa ukiangalia hasa wataalamu kama sisi utaona lazima kuna kitu ambacho kimefichwa fichwa, wanaonewa wanyonge, jamani mnyonge na yeye ana haki, isifike pahala tukaoneana.

Hili Mhe. Spika, sikubaliani nalo katika unyanyasaji wa wanyonge katu kabisa. Mtu huyu amesimamishwa kazi, ameambiwa amefanya hilo kosa wakati sio yeye, kuna mtu ambaye amefanya kitendo hicho tena kafanya kitendo hicho cha kisayansi na kiteknolojia na ujuzi kabisa, lakini hakupelekwa kwenye vyombo vya sheria, yeye huyu maskini ya Mungu, Mhasibu alikuwa hayupo amekwenda kusoma na yeye kapigwa changa la macho kabisa, sijui wametia njia gani za kuweza kumtia hatiani.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri hapa kuna *documents fake* zipo ambaye huyo mtu aliyezifanya kuna *cheque fake*, kuna *statement bank fake*, ambazo zote hizi hapa zipo na mpaka leo huyu mtu bado hajafikishwa kwenye vyombo vya sheria, namuomba sana Mhe. Waziri sitaki kumzuilia fungu hapa kwa sababu naamini yeye ni mtu ambaye ni mkweli na mtekelezaji, namuomba sana na Katibu leo akirudi tu hili suala walitafutie ufumbuzi kwa mujibu wa sheria, kwa sababu Tume ya Utumishi hayupo maskini ya Mungu. yeye yupo kwenye *dilemma* tu anaelea, kule ukenda Wizara ya Fedha hajulikani wao wamemdhibiti tu wamemtia kwenye koti.

Naomba hili suala lishughulikiwe sitaki kupiga buti kwa hili nipate jibu zuri huyu mtu aweze kurudishwa kazini *immediate* kabisa kwa mujibu wa taratibu, kama kuna makosa wapelekeni kwenye vyombo vya sheria hakuna tatizo, sheria zipo wazi, Mahakama zipo, wapelekeni huko kunakohusika, lakini tusimuonee

mtu mmoja tu kwa kumficha, halafu zaidi ambapo kuwa humu mna mwanamama ambaye ndiye aliyesaini kama ana-*acting* lakini hakusimamishwa. Sasa sijui nani tuseme, yeye ndiye aliyesaini kama Mhasibu Mkuu *acting* Mhasibu Mkuu, lakini hakusimamishwa kenda kasimamishwa mwenzangu mimi tu maskini ya Mungu tusiyejuana na watu.

Mhe. Spika, sasa niende katika Mji Mkongwe. Mji Mkongwe kwanza nimsifu sana Mkurugenzi wake ni mahiri ni mtu ambaye anafuata sheria ambazo zile za uwekezaji wa *UNESCO* anafuata utaratibu. Kwa hapa mimi nampongeza sana na yeye mara nyingi sana ndiye anapata tabu kujibu hoja kwa hawa wafadhili wetu. Kwa hivyo naomba sana Serikali imuangalie naye kwa jicho la kuiutendaji kabisa.

Mhe. Spika, nimalizie na Mamlaka ya Maji. Mamlaka ya Maji ninaomba sana kwa kweli hali halisi tunaijua, hali ya ukame wa maji tunaelewa hivyo lakini bado kuna fungu ambalo linaweza likafanikisha zaidi ili kuleta mambo yawe mazuri hasa katika fungu la kuleta maji ni hili la shs.50,000,000/=. Ninaomba sana hilo tulipitishe na tuwape ili waendelee katika mradi huo kutuletea kwa wingi sana. Mkurugenzi kajitahidi na Wakurugenzi wenzake katika kubuni mbinu za kuongeza visima. Lakini niwashukuru sana hawa wawekezaji wetu wa Japan, nawashukuru sana kwa utekelezaji wake vile wanavyotusaidia sisi hapa Zanzibar na kutujengea matanki mengi na visima sita. Lakini kama tunavyojua ardhi ni ardhi, na sisi tunaitumia vibaya tunajenga ovyo, tunakata miti lakini lazima viwango vya maji vinakuwa vinapungua. Ninawaomba sana hawa ndugu zetu Wajapan wazidi kuendelea kutusaidia wasisikie tabu yoyote na sisi tuko pamoja nao Waheshimiwa tunawapongeza na pongezi zaidi zimfikie mwenyewe Balozi wa Japan kwa

kazi nzuri ambazo aliyoianzishia hapa Zanzibar kutuonesha njia za kupata maji safi na wale wale waliokuwa hawajapata tunawaomba sana wawe wastahamilivu.

Mhe. Spika, niendelee kuwasifu sana hawa kwa mradi huu wa *ACRA*. Mradi huu wa uwekezaji katika masuala ya vijiji unakwenda vizuri ni matatizo ya hapa na pale tu, unajua zile *line* nyengine za kizamani, lakini ninaomba kuwa wajitahidi.

Mwisho ni Shirika la *ZECO*. Nimshukuru sana ndugu yangu Meneja pamoja na watendaji wenzake na hasa katika utendaji wao mzuri kukamilisha miradi yote bila ya kuambiwa wizi, wamelifikisha pahali pazuri na juzi hakuna asiyeona shirika limezindua miradi yote hiyo miwili na tunakwenda vizuri, kwa sababu hapa mtihani mkubwa sana katika ulaji wa fedha na wameweza kuusimamia vizuri kwenye Wizara yao pamoja na Katibu wao ambao wao ni watekelezaji wa ile sera yenyewe na yale mafungu yenyewe ya fedha zinazoingia kwa wafadhili wetu, tumefika pahali pazuri sana. Lakini pongezi nyengine kutupelekea umeme kwenye vijiji na kuwakopesha wanyonge. Hilo si jambo la kawaida ni jambo ambalo la kufurahisha kabisa kwa sababu wanyonge sasa hivi vijijini wanapata neema ya umeme kwa njia ya mkopo. Hiyo namuomba sana aendeleze jitihada zote za kuweza kuwasaidia hawa wanyonge lakini kwa *time* inapofika.

Vile vile Mhe. Spika, kuna tatizo la *transformer*, hili naomba sana kuwa hizi *transformer* sasa hivi tunaomba sana kwa haraka sana azilete ili kufanikisha kwa wale ambao *transformer* zao zimeharibika kwa kupitia wanyama kama komba na wengine. Mhe. Spika, hapa sitakuwa na mengi zaidi nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa kusimamia katika mradi wa *ZECO* pamoja na Katibu na Naibu wake Katibu ili kuona

kuona wale wafadhili wanatupenda sana wanatuongezea mafedha ili ukisimamia vizuri hakuna ubadhirifu basi basi wale wenyewe wafadhili wanatuletea kwa wingi kabisa.

Mhe. Spika, namshukuru sana Meneja wa ZECO kwa jitihada zake aendelee hivyo hivyo pamoja na Mkurugenzi wa Maji. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad:Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi ya kuchangia machache katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2013/14.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa uwasilishaji mzuri wa Mhe. Waziri, katika usomaji wa kitabu hiki kidogo ambacho kimesheheni majadweli yenye kutoa taarifa kamili. Lakini nataka nianze kwa kuanza na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo ya kitabu hiki na ndio hali halisi ilivyo ni kuwa Wizara zote tulizonazo za Ofisi Kuu Pemba, na Ofisi Kuu huwa zina majukumu ya kusimamia shughuli zote za Wizara kule Pemba. Sasa katika kitabu chake Mhe. Waziri ameomba tuidhinishe jumla ya shilingi za Kitanzania 77,240,030,000/= kwa kazi za kawaida na kwa kazi za maendeleo na kati ya hizo shs.69,721,030,000/= ni kwa shughuli za maendeleo. Sasa ukiangalia Ofisi Kuu Pemba ambapo kama nilivyotangulia kusema ni kuwa ina jukumu la kusimamia shughuli zote za Wizara na kutekeleza malengo yaliyopangwa na taasisi zetu kwa upande wa Pemba, Ofisi Kuu Pemba imeidhinishiwa jumla au imeombewa kiasi cha Tanzania shilingi 1,123,007,000/= kwa kazi za kawaida na hakuna hata senti moja ya shughuli za maendeleo.

Mhe. Spika, sasa Ofisi Kuu ya Pemba inafanya kazi za Wizara kule Pemba na Pemba ni kubwa, na Pemba kuna shughuli kama zinazofanywa katika upande wa pili Unguja. Tunalolishuhudia ni kuwa unapokwenda Wizarani na kufuatilia shughuli hizi za maendeleo ikiwa ni pamoja na maji, umeme na kadhalika. Nashukuru kwanza watendaji wa wizara kule Pemba wako tayari wakati wowote kutoa msaada, lakini kwa bahati mbaya hata yale mafuta ya kuingiza kwenye gari kufuatilia tukio hawana. Kwa hivyo, hubidi sisi wenyewe tuchangie mafuta ili kufuatiliwa shughuli zetu.

Mimi nauliza kulikuwa na sababu gani hasa hii Ofisi Kuu kule Pemba isipangiwe fedha za maendeleo na ikafanya kazi zake kwa ufanisi zaidi wakati kuna kazi nyingi sana tu za kufanya. Hii kukaa ikawa kazi yao ni kupima tu na kuleta makisio inatuonesha huruma sana, kumbe ziko fedha nyingi za maendeleo zinaombwa kwa shughuli za wizara hii. Kwa hivyo, hii nataka nipate maelezo ya kina vyenginevyo sitokubali kirahisi.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, niende katika Mradi wa Usambazaji wa Umeme Zanzibar, hii tutaipata kuanzia ukurasa wa 57. Mhe. Spika, ukurasa wa 57 unazungumzia kuhusu mradi wa ujenzi wa njia ya pili ya umeme Unguja ambao nashukuru *Alhamdulillah* umekamilika, unazungumzia habari ya uimarishaji njia na ujenzi wa vituo vipya vya umeme vitatu, vile vile napongeza sana.

Lakini ukija katika usambazaji wa umeme vijijini ukurasa wa 58 kifungu 148 kinasema kuwa, “Shirika lilipanga kutumia shilingi 1.2 bilioni kwa kazi za kusambaza umeme mijini na vijijini na kati ya fedha hizo

shilingi 775,000,000 ni kutoka katika Mfuko wa Shirika la Umeme na shilingi 425,000,000 ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Halafu Mhe. Spika, chini yake ukienda imeandikwa, "Hadi kufikia Machi 2013, jumla ya shilingi 1,457,282,281.00 zimetumika kwa ununuzi wa nguzo, *wire*, *transformer* na vifaa vya umeme kwa kazi za kusambaza umeme katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba kama inavyoonekana katika kiambatanisho "L".

Nazungumza hivi kwa sababu katika bajeti hii ambayo ndio inamalizika hapa mimi nilizungumza sana kuhusu mahitaji ya umeme katika jimbo langu, nilipoangalia hiki kiambatanisho "L" ukurasa wa 99 hakuna hata kijiji kimoja katika Jimbo la Mtambwe kilichopatiwa umeme. Kwa bahati mbaya kifungu 149 kinamalizia kwa kusema kuwa 'shiri linaendelea na kazi za ujenzi wa *line* za kusambaza umeme kwenye vijiji vya Mtwango – Pogwe, Kibonde Maji pamoja na Kitundu – Mkanyageni'. Vile vile hamna.

Mhe. Spika, tukiendelea na kitabu ukurasa wa 59 hapa kutakuwa na malengo kwa mwaka 2013/2014 ikiwa moja ni mradi wa uimarishaji wa miundombinu ya umeme kwa msaada wa Norway pamoja na mradi wa usambazaji umeme vijijini. Lakini ukienda katika kifungu chengine wizara imetaja jumla ya vijiji ambavyo vilitiwa umeme lakini na Mtambwe Kaskazini imeambiwa kuwa haimo. Sasa wakati Mhe. Spika, vijiji vyetu na sisi tunahitaji huo umeme na kila mtu anajua umuhimu wa umeme na anaona kuwa ulipozimwa umeme miezi mitatu tu hapa adha tuliyoipata. Mimi nashangaa ikiwa kwa mwaka mzima wakati

niliahidiwa kuwa nitasambaziwa na mimi ummeme na vijiji vyengine tayari alikwishakwenda kwa wizara Pemba na walikwisha tupimia na kutwambia gharama zilioko, hakuna hata kijiji kimoja.

Mhe. Spika, hivi sasa nazungumza nikikuanzia Shehia na utaona huruma kwa namna gani wizara haikulipa uzito Jimbo la Mtambwe katika kuwasambazia umeme kama ifuatavyo:-

Kwa mfano, Shehia ya Mtwambwe Kaskazini, kuna kijiji cha Mtambwe mkuu ni kikubwa tu, tena chenye historia hakina umeme. Kuna kijiji cha Nyali, Chekea, Chanjaani hakuna umeme ambapo Chanjaani tumeambiwa mpaka tuwe na shilingi 23 milioni ndio tutaweza kupatiwa huo umeme huko Pemba.

Halafu ukija Mtambwe Kusini kuna Kivumoni, Tondooni, Mkanjuni, Mitambuuni na Kinazini hakuna umeme. Inasikitisha.

Mhe. Spika, tukija katika Shehia nyengine mfano kama Shehia ya Kisiwani kuna Tondooni, Mashuga na vijiji vidogo kama vile Malindini na Mleteni vyote havina umeme. Katika Shehia ya Piki tulijitahidi angalau tupeleke umeme pale Matuuni mpaka kukanunuliwa nguzo na ziko zinaharibika hivi sasa. Wizara inashindwa kutupelekea umeme. Pia kuna kijiji cha Shengejuu umeme umepita lakini haukupelekwa.

Sasa Mhe. Spika, ikiwa hali ni hii na tukiona wenzetu wanafanyiwa huwa inatusikitisha sana, namuomba Mhe. Waziri anipe msimamo hasa kuhusu mipango yake ya safari hii, vipi na mimi ataweza kunipatia umeme ili wananchi wangu waweze kufaidika na huduma hiyo muhimu.

Tukitoka hapo Mheshimiwa sasa tuingie kwenye huduma ya maji. Huduma ya maji kama ilivyo umeme ni muhimu sana na mimi nakubaliana na maelezo yaliyomo katika kitabu kuwa bila ya maji hakuna uhai na bila ya maji safi na salama hakuna afya njema. Mhe. Spika, tukifungua ukurasa wa 37 wa kitabu chetu hiki cha bajeti hapa ipo *program* ya maji na ukiangalia ukurasa wa 38 una maeneo yaliyopatiwa huduma ya usambazaji maji vijijini.

Mhe. Spika, hii tunayomaliza ni bajeti ya tatu kila siku ninaambiwa kuwa Mtambwe Kaskazini tutapeleka maji na mpaka leo hayajapelekwa. Katika jadweli humu simo lakini angalau namshukuru Mhe. Waziri safari hii ni tofauti na bajeti zake zilizopita. Kwa makusudi kaeleza katika kifungu cha 101 kuwa miradi mengine iliyopangwa kutekelezwa ambayo haikuweza kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 ni vijiji vingi pamoja na Mtambwe Kaskazini. Angalau kaainisha kwamba havikutekelezwa.

Tukiendelea na kitabu hiki ukurasa wa 45 kifungu 115 kinaeleza miradi mingi tu ambayo itafanywa ya maji, lakini mwisho huku kuna sentensi inasema, miradi mengine ambayo imepangwa kutekelezwa kupitia *program* hii ni Mtende, Muyuni na kadhalika na Mtambwe Kaskazini imo. Sasa imepangwa namna gani, ni uchimbaji wa visima, usambazaji wa mabomba au vipi kwa sababu huku juu ndio maelezo yalivyoeleza.

Lakini naomba nimwambie Mhe. Waziri kuwa kama nilivyoeleza kwenye umeme na vile vile katika jimbo langu kuna matatizo makubwa ya maji, kuna vijiji bado mpaka sasa hivi havijapata maji. Kama

nilivyokwenda kwenye umeme naomba Mhe. Spika, uniruhusu na huku nikutajie vijiji hivyo shehia kwa shehia kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nitaanza Shehia ya Mtambwe Kaskazini, Chekea, Kidundo pamoja na Chanjaani vote hivi havina huduma ya maji. Shehia ya Mtambwe Kusini kuna vijiji kama Makongeni pale pala skuli pana na kituo cha afya, Mitambuni, Kinazini kote huko hakuna maji.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri tumejitahidi kusambaza maji kwa nguvu zetu na kutafuta wafadhili, lakini vile mahitajio akipata mmoja itakuwa ni fitna kwa wengine kila mtu huwa naye anataka na sisi uwezo huo hatuna. Namuomba Mhe. Waziri anipe uhakika hasa katika hivyo vijiji vyengine vitakavyoshughulikiwa usambazaji wa maji safi hivi vina mpango gani wa uhakika ili watu wajue kuwa watapata au itakuwa kama wanavyoahidiwa kila siku. Hiyo ni ya maji.

Jengine Mhe. Spika, ninalopenda kuzungumza ni kuhusu huu umeme tulionao. Namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sasa hivi Unguja na Pemba tuna umeme wa kutosha na umeme huu unatoka Bara. Uzoefu wangu nilionao ni kuwa umeme huu ni ghali sana kweli kweli na tulikuwa na madeni makubwa kweli ya umeme pamoja na kuwa kulipiwa kwetu na serikali ilikuwa haikutoa fidia kwa wananchi lakini bado tulikuwa na deni kubwa la umeme. Wakati ule ilikuwa ni kwa kisiwa cha Unguja tu na sasa hivi tayari kushaongezeka na Pemba umeme huu huu kutoka huko Bara. Naomba Mhe. Waziri anipe takwimu sahihi hasa kweli tunao umeme tunashangiria, lakini wananchi wanalipia kiasi gani na serikali inafidia kiasi na

kwa jumla kwa makisio tu ya wastani kwa mwaka serikali inawajibika kulipa kiasi gani kufidia wananchi katika umeme huu ghali.

Halafu zaidi ya mipango iliyoko katika utafiti nikitaka nijue kuna mpango gani hasa mahususi uliowekwa ili Zanzibar tuwe na umeme wetu wenyewe wa kujitegemea.

Mhe. Spika, umeme huu unaotoka Bara ni umeme tunaoletewa tunalipia na kadhalika, lakini si wetu. Kwa hivyo, ili tuweze kuendelea hasa serikali ina mpango gani wa kuona kuwa Zanzibar nayo inajiendesha kwa umeme wake wenyewe wakati tumeambiwa kuwa kuna uwezekano hapa wa kupata umeme kwa kutumia maji, upepo, nishati ya jua na kadhalika.

Jengine Mhe. Spika, ambalo naomba kuzungumza ni kuhusu suala zima ambalo lilikuwa likienea katika vitabu, suala la mafuta na gesi asilia. Katika kitabu kilichopita nilizungumza vizuri sana tu, katika kitabu cha Makamu wa Pili wa Rais imezungumzwa kuwa limo katika mjadala. Mimi namuomba Mhe. Waziri anieleze, kulinyamazia kimya suala hili kutoliingiza katika kitabu wakati sisi tulipitisha katika Baraza hili la Wawakilishi kuwa mafuta na gesi asilia si mambo ya Muungano wala hakutia lolote humu ni kuwa kisharidhika na hali hii tuliyonayo au suala hili lishatupilia mbali kwa sababu kuna mabadiliko ya Katiba. Naomba na hili nalo nipewe jibu.

Halafu jengine katika kitabu ni kuwa Mheshimiwa kaeleza vizuri sana namna anavyojitahidi ili kuweka himaya ya Mji Mkongwe kutokana na hali kama ilivyo. Lakini mimi nauliza lile jengo kubwa la kisasa

linalojengwa pale palipokuwa na nyumba tuliyoiita Mambo Msiige, kweli linakwenda sambamba na uhuishaji wa Mji Mkongwe kutokana na uhalisia wake au kwa sababu nasikia ni hoteli na pale pana ufukwe mzuri sana tu, limewekwa kwa makusudi ili kuona kuwa utamaduni wa Wazanzibari sasa hivi utakuwa namna kadhaa katika siku za mbele zijazo. Naomba hili nipate majibu tena majibu ya kuridhisha.

La mwisho Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa juhudi yake. Nimeona katika Shehia ya Kisiwani kuna mradi mkubwa wa maji, nasikia kunataka kutengenezwa matangi mawili makubwa ili maji yasambazwe lakini haijulikani lini, naomba atoe maelezo ili wananchi wasikie na wajue kinachoendelea. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi nitoe mchango wangu katika Hotuba hii ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri mtu mzima mwenzangu kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake na pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote kwa jumla kwa kuleta hotuba ambayo kwa kweli imekidhi haja.

Mimi Mhe. Spika, ingelikuwa sina hoja za wananchi wangu walizonituma ningeunga mkono hoja tu moja kwa moja, lakini nimeona nisimame nieleze hoja za wananchi wangu walizonipa na nipate jawabu. Sina haja ya kupiga buti lakini nadhani nitapewa jawabu nzuri ili niweze kukamilisha yale malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia katika maeneo matano. Eneo la kwanza umeme vijijini ipo katika ukurasa wa 58 kifungu 148. Nimpongeze Mhe. Waziri na nimshukuru kwamba na mimi katika mradi huu nimebahatika vijiji viwili kupata umeme huo. Kijiji cha kwanza ni cha Kama kimegharimu shilingi milioni 74.6 na cha pili Mkanyageni kimegharimu shilingi 98.3 milioni. Nashukuru sana na upande wa Kama tayari huduma zimeanza nadhani na Mkanyageni karibu utamalizika mradi.

Lakini ninachoomba kama walivyozungumza wenzangu kwamba bado gharama za umeme kwa mwananchi wa kijijini ni ghali sana, kwa sababu kama mwananchi atakuwa ana nguzo moja tu ya kununua pamoja na mita kwanza nguzo wanauza shilingi laki moja na nusu, mita laki moja na nusu, hujapata *wire*, hujatafuta kikombe hujafanya lolote. Sasa umeme wa nguzo moja hata mtu apate kutumia ndani unagharimu kwenye shilingi laki tano au sita, ningeliomba na mimi wananchi wanaokuja na pesa za kuanzia wapokelewe na nyengine walipe kidogo kidogo kwa lengo la kuweza kufaidika na hii huduma ya umeme, vyenginevyo umeme utakuwepo lakini wananchi watashindwa kuutumia na *ZECO* itapata hasara. Sasa naomba wizara pamoja na watendaji watafute mikataba mwepesi ili wananchi waweze kulipa pesa kidogo kidogo na kuweza kutumia huu umeme.

Lakini pamoja na hayo, kuna matatizo ya hizi *transformer* wakati mwengine zinaungua na unapita muda mrefu sana hazijafanyiwa marekebisho. Kwa mfano, hivi sasa kuna *transformer* yetu *Mwakaje Branch* pale sasa hivi ni mwezi wa tatu bado haijatengenea na kwa bahati mbaya umeingia mwezi wa Ramadhani, watu wanatumia umeme sana wapate maji baridi. Kwa hivyo Mwakaje maji baridi hayapatikani watu wanakuja Mfenesini, waende Bububu kuchukua barafu ni usumbufu. Sasa kama pahala pa kuazima kunapatikana

Mhe. Waziri ningeomba akatafuta kuazima angalau tukavuka huu mwezi wa Ramadhani ili mtu ikifika jioni apate kupoza roho kidogo.

Pili, vile vile kuna *transformer* watu wana mashamba yao hununua wakaweka kwenye mashamba yao lakini ikatumiwa na kijiji, na hizo pia zinaharibika na iko moja upande wa Dimani huku wanaita Muhimbili ipo muda mrefu hivi sasa ni mwezi wa tatu na wana kijiji wanakosa umeme. Kwa hivyo, ningeliomba na hao watu ambao wanaleta *transformer* kusaidia shirika je, ikiharibika dhamana anakuwa nani? Kama ni ya shirika basi na hii ifanyiwe kazi na kama hawapaelewi basi mimi nitawapeleka kwa sababu hilo shamba linanihusu. Kwa hivyo, naomba na hili Mhe. Spika, nipate jibu wanaotengeneza ni nani.

Sehemu ya pili niingie kwenye sehemu ya ardhi ukurasa wa 9 kifungu nambari 24. Hapa kidogo ndio agizo moja nililopewa na wananchi wangu, hili nilikuwa nilizungumze juzi kwenye Wizara ya Katiba na Sheria, lakini ardhi na hii sehemu ninayotaka kuizungumza wanagusana gusana. Kwa hivyo, ningeshauri kwa kuwa juzi nimekosa leo nimpe kazi yeye anisaidie ili tuweze kupata nafuu.

Mfenesini mashine ya maji pana shamba la wakfu, lakini hapo mwanzo halikuwa wakfu lilikuwa ni shamba la serikali tangu mwaka 1964 na watu wamejenga, pana familia sasa hivi si chini ya sitini. Lakini wakfu huo umetokea Maruhubi baada ya kutakiwa eneo la viwanda palikuwa na wakfu ukaondoshwa pale ukaletwa Mfenesini. Tatizo lililotokezea kwamba mwezi uliopita wa sita au watano walikuja watu wa wakfu wakazungumza na wananchi pale na walikubaliana kwamba kwa kuwa watu wamekaa na

wamekutwa basi watoe mchango mdogo ili wakfu uweze kutekeleza hao waliotoa wakfu waweze kupata faida yao.

Lakini baada ya kukaa mwezi mmoja mwezi wa pili imekuja barua wahame kwa muda wa siku tisini, ina maana mazungumzo ya mwanzo yale hayakukubalika. Sasa watu tangu kupewa barua hiyo hadi hivi leo mwezi wa pili hawana raha ya maisha, kwa sababu mtu ukiambiwa uhame kwa siku tisini nyumba umejenga miaka kumi mpaka kumi na tano ndio umeiweza kuijenga je, huko anakokwenda atatumia nguvu gani za kujengea.

Sasa wizara nimezungumza na Waziri na Katibu Mtendaji wa Wakfu lakini bado ufumbuzi hatujaupata. Hivyo naomba na yeye kama anahusika na ardhi na lile shamba lilikuwa la serikali, wakfu ule wa kuhamishwa tungeliomba watafute eneo la wazi uhamishwe tena wakfu ili wananchi wapate raha za kuishi, la si hivyo basi kama kuna rai yoyote ya kuweza kupata muafaka basi ningeliomba tukashirikiana kwa pamoja ili tatizo hili likaondoka. Kwa hivyo, hili limekuwa kero watu wanaishi kwa wasi wasi wa kuhamishwa na uwezo wa kujenga nyumba nyengine hawana. Sasa namuomba Mhe. Waziri mtu mzima mwenzangu anisaidie na nadhani atakapokuja kufanya majumuisho atanijibu ili angalau wananchi wapate matumaini ya kuweza kuendelea kuishi.

Mhe. Spika, walipanda miti yao ya michungwa, mifenesi lakini yote sasa hivi wanachukua wenyewe wakfu, hatuoni tatizo hilo. Kwa sababu matunda ni kitu cha kupita tu, lakini maisha ya kuishi pale pamoja

na wajukuu na watoto ni mambo muhimu zaidi, michungwa watapanda sehemu nyengine watapata rizki zao.

Suala la pili kwenye mashamba tuna tatizo kubwa la Selem pamoja na sehemu moja wanaita Nguruweni. Selem kipindi cha miaka ya 80 serikali ilikuja kuomba wananchi kwamba inataka kuweka mradi wa minazi mbegu fupi, inazaa nazi nyingi na kwa muda mfupi. Wananchi wakaridhia wakaachia mashamba yao na mradi huo ukafanywa. Lakini bahati mbaya sana hatukupata tija kwenye mradi ule na ukafa. Lakusikitisha kwamba mradi baada ya kufa wananchi hawakuitwa tena wakashauriwa tufanye nini isipokuwa mashamba waligawana baadhi ya viongozi na mengine bado mpaka leo yanagaiwa.

Sasa tukizungumza katika maeneo mengi sana lakini tunashukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwenye mwezi wa tano alikuja Mfenesini na huko Nguruweni akasema basi yale maeneo yaliyobakia yapimwe angalau na wananchi wapate japo pa kulima, kwa sababu hakuna maeneo makubwa yaliyobakia. Maeneo yakapimwa lakini kuanzia mwezi huo mpaka leo unafika mwezi wa tano mpaka wa sita hapajagaiwa kitu kwa wananchi na bado viongozi baadhi yao wanajipitisha wanachukua maeneo yale yale yaliyopimwa.

Mhe. Spika, sasa nimuombe Mhe. Waziri kwa heshima zote alifuatilie tupate jibu rasmi hapa kwamba wananchi hizo heka zilizopimwa nusu nusu za kulima watapewa lini wakati Mkuu wa Serikali kishasema toka mwezi wa tano hapajafanywa kitu, lakini wenyewe wanajipenyeza wanachukua pamoja na Nguruweni. Sasa hili Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri akija anitafutie jawabu ili wenyewe wananchi wasikie nao wajue lini watapata maeneo yao ya kulima.

Niende kwenye sehemu ya tatu Mhe. Spika, kuhusu suala la maji. Tunashukuru kwamba serikali ilituandalia mradi unaitwa *ACRA* na uligharimu pesa nyingi sana, bajeti iliyopita ulikuwemo lakini bajeti hii sikuona kuzungumzwa nimeambiwa tu kuna mradi wa kutoka Mfenesini kwenda Bumbwini haujakamilika. Mimi nafahamu kulikuwa na mradi wa *ACRA* unatumia majimbo matatu, Jimbo la Kitope, Bumbwini na Mfenesini. Bahati nzuri visima vyote viwili vipo Mfenesini pamoja na tangi, tukahamasishwa tutafute vijana katika kila Shehia wasomeshwe utaratibu wa kutengeneza kwenye maeneo madogo madogo yanayoharibika pamoja na mifereji ikiharibika na kukusanya mapato kwa mifereji ya nje.

Kazi hiyo imefanywa Mhe. Spika, vijana wameelimishwa lakini cha kusikitisha kwamba mradi sasa hivi umedorora kabisa, tangi linavuja na halijatimiza mwaka. Kisima kimoja tunaambiwa kimekauka kimebakia kimoja, sasa kikipigwa siku moja upande wa Mbuzini – Mfenesini wakae siku tatu ndio irudie tena siku ya pili inakwenda Bumbwini na upande wa Mahonda ume-*block* pale Mfenesini. Kwa sababu watu wa njia walipochimba misingi mabomba yote ya nchi sita yako nje, kuanzia Polisi mpaka sokoni, lakini ukienda Mahonda maeneo mengi yale mabomba yamefukuliwa.

Sasa sijui wizara mbili wakati mnafanya kazi za maendeleo hamshauriani, wewe umefanya kazi ya mradi wa maji mwenzako anakuja anafanya misingi anayafukua, sasa tunashangaa kwamba serikali moja lakini kila mtu na mipango yake. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hilo suala lipo peupe halitaki tochi leo ukipita kwendea Mfenesini utakuta hiyo mipira iko nje. Sasa kwa kuogopa nguvu kazi ya maji linaweza likafukuka labda likapasuka ndio wame-*block*, sasa maji Mahonda hayendi, tunapata Mwakaje, Kama,

Mfenesini, Uzini lakini kwa mgao kila baada ya siku tatu. Sasa ningelimuomba Mheshimiwa kwa kuwa wenzetu walitumia pesa nyingi sana pamoja na serikali yetu waende wakaangalie tangi lililojengwa uharibifu wake na hayo mabomba ili yachimbwe tena yafukiwe. Kwa sababu mradi ule uligharimu pesa nyingi sana na vijana wengi walikuwa wanaajiriwa kila bomba moja lile la futi 12 au 13 anachimba msingi na kulizika kwa shilingi elfu tatu.

Mhe. Spika, fikiri mradi huo umekwenda mpaka Mahonda, Bumbwini, umezunguka mzunguko wote wa Mbuzini kiasi gani cha fedha kimetumika, lakini mabomba sasa hivi yako nje. Sasa naomba na hilo Mhe. Waziri alifanyie kazi ili zile pesa za wenzetu ziweze kuthaminika pamoja na za serikali, lakini na wale vijana waliofunzwa sasa hivi hawana kazi yoyote. Sasa nadhani na wale watizamwe kama kuna maelekezo mengine wapewe ili ile gharama ya kuwasomesa wale pia iweze kufanyiwa kazi na serikali.

Jengine tuna kisima chetu cha muda mrefu tangu ukoloni pale pale Kivuma ambacho pia tunatumia kama hiki cha *ACRA* kikifanya matatizo tunatumia kile. Kwa kweli kimevamiwa sana na majumba wa wananchi wanaokaaa pale kwa sababu hakina uzio na tushaomba muda mrefu tufanyiwe uzio lakini bado hakijafanyiwa. Kwa hivyo, naomba na hili kama serikali itakuwa na uwezo basi tufanyiwe uzio ili tuweze kunusuru pengine matokeo mabaya kuja kutokea sehemu ile. Kisima cha muda mrefu tangu mwaka 1964 lakini kinatufaa na kina maji mengi, hivyo watufanyie uzio pale ili wananchi wasiweze kukaribia na tuweze kutumia maji katika hali iliyokuwa nzuri.

Sehemu yangu ya mwisho Mhe. Spika, nije kwenye nyumba za maendeleo za Michenzani na Kilimani. Muasisi wa nchi yetu Mzee Abeid Amani Karume alijenga nyumba zile kwa minajili ya kuwapa wananchi maisha bora na kidogo na sisi mtu akija petu ajue kwamba pana mji wa maendeleo. Lakini kwa bahati mbaya sasa hivi ukipita ukiangalia hiyo Kilimani pamoja na Michenzani utasikitika sana, labda hili jumba jipya lililomalizwa juzi, lakini majumba yote yamechakaa mno utadhani hayakai watu. Kibaya zaidi ni kwamba watu wameshakuwa wanaishi wengi sana katika nyumba moja, utakuta pengine ikifika wiki tu karo zimefurika, maji ya Michenzani utayakuta yanaingia kwenye ziwa lile la bwawani. Sasa utakuta hata upitaji wa pale barabarani watu wanapita na magari, wanapita kwa miguu wanarushiwa maji yale machafu kwa kweli haipendezi.

Mimi ningelishauri suala moja kama wizara itasaidia hilo nadhani tatizo lile litaondoka. Kwa kuwa nyumba zina watu wengi na haiwezi kukaa miezi miwili mitatu bila ya makaro kufurika, basi angalau kila wiki magari ya kufyonza uchafu yangepita yakawa yanapunguza maji ndani ya makaro. Kila wiki yanapunguza haiwezi kufika muda yakaweza kutapika yale maji, nadhani wangefanya hivyo, bora wanunue magari kama mawili yaweze kusafisha kwa sababu hata tuseme yachimbwe makaro mengine itakuwa hapana pa kuchimbwa, watu washajenga na maji yale yanaleta karaha, mtu anakuja kwenye mji mpya anakuta tope kama zile kwa kweli si jambo zuri.

Halafu la pili tuwashawishi wananchi wanaoishi mle basi angalau kupaka rangi zile nyumba, kuna sehemu nyengine za zege zishabanduka nondo ziko nje. Sasa ningeomba na hilo basi angalau watafute mfuko wa saruji wachapie chapie ili lile lengo la ule mji wetu bado na hadhi ya Mheshimiwa wetu Muasisi iweze

kuonekana, lakini mwenyewe kaondoka mambo huku yanaharibika wakati tumesema watu wakiondoka tutafuata yaliyokuwa mazuri tuyaendeleze mabaya tuyaache. Sasa haya ni mazuri, kwa hivyo tuyafuate ili tuweze kupata nyumba zetu zipendeze na mtu ajue kwamba huu ni mji mpya na Mji Mkongwe unajulikana.

La kumalizia Mhe. Spika, kwa sababu muda ni mdogo nije kwenye Mji Mkongwe na mimi nitie baraka kidogo tu. Mji Mkongwe ni mji wa urithi wa kimataifa na wenzeti dunia nzima wanautambua, hivyo na wanakuja kuuangalia na kuna faida tunapata kutokana na kuwa mji wa hifadhi. Lakini bahati mbaya sasa hivi hawa wawekezaji wote ndio wameuvamia mji ule. Sasa hivi pana hoteli si chini ya kumi wizara wakihama zinafanywa hoteli, nyumba mtu anabembelezwa analetwa ng'ambu wanafanya hoteli, sasa itakwenda mwisho itakuwa si Mji Mkongwe utakuwa ni Mji wa mahoteli. Hiyo itakuwa haina raha kwa sababu dunia nzima na nchi zote miji yao kama hii wanaienzi, watajenga maghorofa hata mia kwenda juu, lakini Mji Mkongwe utaachwa kama historia.

Sasa na mimi ningeshauri mahoteli sasa hivi yende Nungwi, Matemwe bado nafasi zipo, Pwanimchangani, Mfenesini, Kama, lakini Mji Mkongwe uachwe kama Mji Mkongwe ambapo kila anayekuja ajue kuwa huu ni mji wa urithi na Mji Mkonwe wa zamani kwa sehemu yetu hii ya Zanzibar. Vyenginevyo Mhe. Spika, ile hadhi tutaiondoa na tutatoka kwenye ile sifa iliyo katika dunia kwa sababu nyumba zile zimejengwa kwa jiwe na watu kama ukuta wa Ngomekongwe ukienda huwezi kuamini kuwa mtu kainua jiwe la kujenga ukuta ule. Lakini sasa hivi utakuta vurugu tupu magari mazito yanapita yanapasua nyumba. Sasa ningeshauri kwamba wanaohusika pamoja na wizara hili suala walisimamie ili hadhi ya mji wetu upate kuendelea kwa vizazi vya sasa hivi na vizazi vinavyokuja baadae waweze kuona.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi na nimuombe mtu mzima mwenzangu Mhe. Waziri haya mambo yangu matatu aje kunipa jibu ili niweze kupitisha uzuri bajeti yake. Mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusu hoja ilioko mbele yetu.
Awali ya yote Mhe. Spika, kabla ya kwenda kwenye hoja nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii.

Pili nikuombe wewe na Wajumbe wako niwatakie Ramadhani Kareem na niwaombeni tuwe makini sana katika kipindi hichi cha siku hizi 30 katika kutumikia hii amri ya Mwenyezi Mungu.

Aidha kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi napenda nichukue nafasi hii kwa Wazanzibari wote kuwatakia Ramadhani Kareem. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, nende kwenye hoja.

Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa 54 mpaka 59 hapa Mhe. Waziri kazungumzia suala zima la Shirika la Umeme. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na *ZECO* kwa jumla kwa kuweza kusambaza huduma hii takribani katika sehemu kubwa za visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ni kazi kubwa waliyofanya na kwa sababu wenzetu Waingereza wana msemo wanaosema, "Usiache kutoa pongezi

kwa yule anayefanya vizuri". Sasa kwa mantiki hiyo napenda nilipongeze sana shirika hili pamoja na wizara kwa kufanyakazi nzuri katika kututumikia sisi walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Spika, kwa kweli hakuna jambo lililokuwa halina hasara zake, pamoja na faida kubwa tuliopata kwenye shirika hili, lakini kuna matatizo mengi ambayo yamewakumba walipa kodi wa kawaida. Mhe. Spika, katika usambazaji wa umeme huu, shirika katika kuweka mundombinu yake huwa linakata mazao, linavunja nyumba za walipa kodi wa nchi pamoja na kuondosha vitu vyao mbali mbali, lakini katika hili inaonekana mara nyingi serikali haiko makini katika kuona hawa wananchi katika kusambaza huduma hii wanapata athari gani.

Kwa mfano Mhe. Spika, Shirika la Umeme kwa kushirikiana na hii Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, hivi karibuni tu walifanya kazi ya kupeleka umeme katika Kware ilioko Makaani Vitongoji, kutoka Vitongoji Darajani mpaka kufikia Makaani Kwareni. Walikata mazao mengi sana ya wananchi, miembe, migomba, michungwa na kadhalika, ni mazao ambayo yanawasaidia wananchi katika kusaidia kupunguza kasi ya umaskini na kujiongezea kipato. Lakini wizara hii ilifanya kazi hiyo bila kwanza kukutana na wale waathirika, tathmini iliyofanywa hawakushirikishwa wenye mashamba na mazao. Walikwenda tu wataalamu wa shirika na wakafanya tathimini, lakini karibu huu ni mwezi wa sita mpaka sasa hivi malipo hawajalipwa na hao wenyewe hawajui kama watalipwa au laa.

Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nikiuliza swali hapa nikaambiwa kwamba ningoje ipite bajeti hii, ikishapita bajeti hii tutakaa mimi na wewe na Mhe. Waziri wa Mawasiliano ili tulitafutie suluhu. Bajeti yako Mhe.

Waziri itapita lakini na wananchi wanaendelea kuteketea kwa mashaka kwa sababu muembe mmoja aina ya boribo kubwa kwa kila msimu yaani mkulima wa kawaida anakodisha karibu shilingi laki moja na nusu. Sasa wewe umeukata bila kumfanyia tathmini yule, hii ni dhuluma na mimi nadhani katika hili lazima uwe makini kwa sababu kiongozi ni Naibu wa Mwenyezi Mungu katika uso wa ulimwengu na uadilifu wako unaangaliwa Mhe. Spika.

Sasa leo unafanya mambo bila ya kuwashirikisha wenyewe na hadi leo hawajui kama watalipwa au laa. Katika hili mimi naomba ukija kufanya majumuisho Mhe. Waziri uhakikishe unanipa maelezo au unatoa ufafanuzi ni lini wananchi wale watalipwa au bajeti kiasi gani mlitenga kwa ajili ya wale walioharibiwa mashamba yao pamoja na mazao yao. Bila hivyo basi mimi nadhani pamoja na Ramadhani tulionayo basi itabidi Mhe. Waziri nizuie shilingi katika bajeti hii kama hukunipa maelezo ambayo hayatakidhi haja.

Mhe. Spika, kabla sijaondoka hapo ni kwamba shirika hili ni miongoni mwa shirika ambalo yaliundiwa Kamati Teule kuchunguzwa. Sasa Mhe. Spika, hili shirika hadi leo utekelezaji wa ile ripoti bado. Mimi nilikuwa nataka aje anieleze vipi utekelezaji wa ile ripoti ambayo ilitolewa hapa umefikia wapi au ndio umetiwa kapuni, na kama imetiwa kapuni ina maana sisi tujue vya kufanya kwa sababu tulitoa fedha tukawapa wale wakachunguze. Leo ripoti mmeikalia kitako tu hayo si matumizi mazuri ya pesa za walipa kodi wa nchi hii na kwa vyo vyote vile itabidi taratibu zitumike ili kuona kwamba tunafanyakazi ya matumizi mazuri ya walipa kodi wetu.

Mhe. Spika, sasa niende katika Idara ya Nishati na Madini. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza tena wizara yako Mhe. Waziri kwa kuweza kupeleka vijana wetu 3 nchini Uingereza kwa ajili ya masomo ya *Petroleum Engineering,* hili nakupongeza sana. Halafu napenda nimshukuru kijana mmoja ambaye mmemuajiri juzi tu yeye mwenyewe kenda kujisomesha amejitolea masomo hayo hayo ya *Petroleum Engineering*. Nampongeza huyo kijana na nawapongeza nyinyi kwa kumuajiri.
Mhe. Spika, tushukuru kwamba Mwenyezi Mungu ulemavu kauleta kwetu sisi binadamu pamoja na viumbe vyengine. Laiti ingekuwa Serikali pia zimeumbiwa kuwa lemavu basi Serikali yetu hii ingekuwa lemavu. Mhe. Spika, inasikitisha sana na inatia aibu kwamba suala la nishati na madini katika nchi hii bado ni tatizo suala ambalo lipo katika nchi hii kuna kila dalili kwamba kuna mafuta katika nchi hii, hadi leo hii tunazungumza tu wenzetu wameona gesi hapo Mtwara juzi tu wamegundua gesi wameshachimba.

Sisi tumepata uhuru mapema kuliko baadhi ya nchi zile za *EU*. Tumepata uhuru mwanzo hapa, wao walikuwepo hapa ndugu zetu tukapata uhuru tukakaa nao hapa wao wakachelewa kupata uhuru wao, walipopata wakaenda kwao sasa hivi ni matajiri kutokana na mafuta. Sisi hadi leo hii kwa kweli inasikitisha sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuna dalili hapa kwamba Zanzibar kwa kiasi kubwa yako mafuta mengi na gesi Mtwara inachimbwa na juzi tu wamegundua, nini kimezorotesha na wakati Baraza limeshasema nishati na mafuta ni ya Zanzibar inasikitisha. Wakati mutiribu mmoja alikuwa anaitwa Bint Kibakora aliimba nyimbo yake inaitwa Chaso. Katika nyimbo yake hii alisema kuwa ni aibu mtu kulala na njaa na kitu anacho ni Chaso

hiyo! Leo sisi mpaka sasa hivi tunazungumzia kununua mafuta nje wa nchi wakati mafuta tunayo basi ni kulala na njaa wakati tunacho.

Nadhani Serikali ikija hapa itueleze sasa, ni kitu gani kimekwamishwa hadi leo hii au ndio miongoni wa Serikali yenye ulemavu sisi tumelemaa kwamba kila kitu hatuwezi na ulemavu uko kwa binadamu tu na vitu vyengine pia hupata, kumbe hii Serikali yetu pia ni lemavu. Mhe. Spika, mmetumia muda mwingi kuwasomesha wataalamu wetu, tumetumia fedha za walipa kodi wa nchi hii kuwasomesha na wengine sasa hivi sijui kwa kusaidiwa na *Ras al Khaimah* sijui wako Uingereza wanasoma kupitia hizi hizi kodi zetu. Nataka mtwambie lini yatachimbwa mafuta katika nchi hii, sio mtupige maneno tu humu tuambiwe lini mafuta yatachimbwa?

Mhe. Spika, niende katika suala zima la nyumba na maendeleo ya makaazi. Ilizungumziwa sana katika ukurasa wa 29 Mhe. Waziri, sasa mimi nadhani kwanza nichukue fursa hii pamoja na kwamba miaka mingi imepita tumshukuru sana huyu muasisi wa nchi hii Marehemu Mzee Abeid Aman Karume. Kwa kweli amewajengea misingi ya vipi wananchi anaweza kunufaika na nchi yake kwa kuwapatia makaazi yale ya kisasa wale wananchi ambao hawana uwezo.

Lakini misingi hii tangu alipofariki huyu mzee inasikitisha sana tunashindwa kuendeleza hii misingi, ukiacha lile *flat* lililojengwa juzi juzi na Awamu ya Sita ya Mzee huyu Aman Abeid Aman, Karume mtoto huyu ambaye yeye ndiye aliyejenga lile. Sasa nyinyi jamani mnashindwa kuendeleza tangu mapinduzi alipoondoka Marehemu Mzee Karume mpaka leo kajenga mwanawe moja tu, nyinyi mna tatizo gani hebu

tuelezeni kwamba Karume baba kajenga *flats* zile zote alipokuja mwanawe angalau katujengea moja. nyinyi je, hili ni tatizo.

Mimi nadhani Serikali inatakiwa iwe wabunifu hebu jamani endelezeni haya mambo aliyoyaanzisha Marehemu Mzee Karume. hivi sasa yale yalioko yanaanguka angalieni ni aibu Kengaja ukienda halikaliki tena, Chake Chake ukienda ni tatizo. Nyumba zimejengwa nyinyi mnaziacha zianguke tu hivi hivi, kama hamna uwezo basi tuachieni sisi watu wa huku pembeni tuje huko na nyinyi mrudi nyuma mje kuona kama hatukuyatengeneza yale na kuja mengine mapya, kama hamna uwezo tuachieni sisi muda mfupi tu tutaweka sawa.

Mimi nadhani Mhe. Waziri utakapokuja hapa uje unieleze kwa nini serikali imeshindwa kujenga zile *flats* zilioko Kengeja ambazo zinaanza kubomoka na tumelipa fedha za walipa kodi wa nchi hii, unieleze hili kwa nini. Mimi nataka kusema kitu kimoja Mhe. Spika, kwamba *flats* zile zimejengwa chini ya usimamizi wa Mzee Karume na akiwa na *engineers* waliobobea kabisa. Leo inasikitisha kwamba Mhe. Waziri upo na Katibu wako Mkuu mnafanya hii *reconstruction* katika yale majengo mtu anakuja kujenga anavyotaka yeye, mtayaangusha yale majengo, sasa kwa nini mnawaruhusu watu wanafanya vile. Majengo yale yataanguka sababu ya kutokusimamiwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, mimi nadhani Mhe. Waziri Wazanzibari watalia na wewe kwa sababu kuna wengine wanaweka ma-*grill*, wengine wanaweka makuta. Yale majengo tumeyajenga kwa viwango vyetu sasa ndio

mkaona tangu mwaka huo mpaka leo hii hakuna nyumba iliyokuwa na ufa, haya mnayojenga nyinyi kila siku yanapasuka humu ndani, lile mmeliona limepasuka.

Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri kuna zile nyumba ambazo tulizojenga za *blocks* kwa matofali ya udongo vijijini, zile nyumba vipi bado za Serikali au umewashawauzia wale ambao mumewakodisha. Kama za Serikali mbona hamzifanyii matenegenezo au hawalipi kodi hawa. Sasa katika hii Mhe. Waziri utakapokuja uje unifahamishe mambo yafuatayo. Ni nyumba ngapi za Serikali ambazo zinalipiwa kodi na ni ngapi ambazo waliopewa tu watu baada ya kuvunjiwa nyumba zao, ni ngapi na zipi zinalipiwa kodi uje unieleze. Maana najua kuna watu wamevunjiwa majengo yao pale sisi tuliwapa tu kipindi kile cha miaka ya 1970 tukawaambia kwa sababu tumewavunjia sawa chukueni. Lakini kuna wengine wajanja wapo hawataki kulipa kodi tu wana visingizio kwamba wamepewa na Mzee Karume wengine hatukuwapa. Sasa walipe kodi, tuwaone wajitambulishe yupi anastahiki alipe na yupi hastahiki asilipe. Hilo jengine.

Mhe. Spika, nije kwenye mambo ya Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi. Kuna bwana mmoja hapa aliwatumikia wananchi na amelitumikia Baraza hili kwa miaka mingi sana na akapata ugonjwa ndani ya kulitumikia Baraza hili. Serikali imempa *plot* ya Darajani kwa ajili ya kujenga *Petrol station* pale. Ni mzalendo wa nchi hii na kaitumikia Serikali hii. Lakini sasa anaambiwa kuna *transformer* asijenge hapo pana matatizo. Lakini kuna maduka pale kwa nini asiambiwe na yeye ajenge duka anyang'anywe, hii ni aibu sana na kafuata taratibu na alikuwa ni Mwakilishi humu ameshawahi kuwa Naibu Spika wa Baraza hili. Mimi nadhani asiachiwe akauza mitake ile moto moto. Kwa hili aruhusiwe, tumsaidieni yule mtu

kaumia sana na ameshamaliza taratibu zote hizi zinazotakiwa. Nadhani katika hili tusiwe wabaya, wakija wageni tu tunawapa kumbe sisi wenyewe tukawa tunadhalilika, huyu mtu ni mzalendo.

Mimi naamini huyu angekuwa Mtaliana pengine ingekuwa tayari ameshaanza kuekeza mambo anayoyataka. Mimi nadhani kama kakamilisha taratibu basi *inshaallah* Mhe. Waziri naamini umesikia na Baraza la Mawaziri hilo hapo linasikia kilio hichi asiachiwe akauza moto moto pale Mikunguni mpeni na yeye aweze kufanya shughuli zake pale.

Jengine Mhe. Spika, Idara ya Mipango Miji. Mhe. Waziri mimi nadhani hawa ndio wenye mamlaka ya kutupangia na kutupambia miji yetu mnalo jukumu hilo. Na hivi sasa Waheshimiwa napenda tu nielezee kwamba kuna tatizo, kuna tatizo kubwa sana hivi la uvamizi wa maeneo, kuna maeneo yanavamiwa na watu lakini kuna maeneo yanavamiwa na maji ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii.

Sasa mimi nilikuwa naomba Mhe. Waziri kama hujawahi kwenda pale *SUZA Campus* ya Nkurumah wende maji yamevamia sana pale, wewe unataka kujenga *retain* kwa sababu watalii wanakuja pale wasije kupata mawimbi ya maji. Lakini nataka uone vile vile katika *Campus* ya Nkurumah maji sasa yameshafika kuuchukuwa ule msikiti. Mimi nadhani katika hili Mhe. Waziri ulione na usitegemee tu mwahala mwa biashara lakini hata mwahala mwa taaluma kwa mfano *SUZA* panahitaji napo kuwepo kwa *retain wall*.
Mhe. Spika, vile vile inasikitisha kwamba katika ofisi yako inatoa hatimiliki kienyeji enyeji tu hivi kwa watu akishakuja mtu maarufu anapewa tu hatimiliki huku ukiwanyima wenye haki ya msingi katika eneo lile.

Mhe. Spika, juzi niliuliza swali katika Wizara ya Elimu kwamba mbona Skuli ya Ndagoni imo katika mashamba ya watu yamechukuliwa tu. Nikaambiwa kuwa wameshapewa hatimiliki, nani katoa wakati wale pale wenye shamba lile wenyewe wanahatimiliki wapo na wanayo hatimiliki. Kwa nini Wizara ya Elimu isiende ikazungumza nao hii ni dhulma.

Nilipouliza juzi kwa mwalimu kule Pemba nikaambiwa kwamba wale waarabu waachiwe shamba lile alaa, kwani mwarabu si mtu hana haki mwarabu katika nchi hii. Mimi ninachosema Mhe. Waziri uende Skuli ya Ndagoni kuna tatizo kweli lile shamba wale vijana wamerithi upande mmoja ni waarabu lakini upande mmoja vile vile ni watu wa hapa, inasikitisha msitowe majibu tu mnawavunja moyo, msitoe jawabu tu hata humu ndani hakuna hata mmoja aliyekuwa hajamgusa mwarabu kwa njia moja au nyengine. Haya kama mwarabu mbaya basi wafukuzeni humu majumbani. Sisi tunajua tunao waarabu ndani sasa tuwafukuze hao.

Mimi nadhani tusiendelee kuchukua kodi kwa waarabu tu lakini hata na haki zao tuzitunze. Hawa vijana kuna Suleiman Ayoub Suleiman na ndugu zake mmewanyanganya shamba na mkawapa hatimiliki, basi nikwambieni huyu Suleiman Ayoub ni mwarabu lakini ni Sheha wa shehia ya Vitongoji, mimi namtetea mpiga kura wangu japo hajanipa kura mimi namtetea ni Sheha huyu leo anawasaidie nyie CCM jamani msifanye hivyo ni tatizo kiongozi ni Naibu wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu msitubague kwa sababu ya misingi ya rangi hata siku moja.

Mhe. Spika, katika hili naomba uniruhusu nimnukuu Ahmad bin Deedat na yeye kafanya *foundation* kwenye Quraan. Anasema naomba kunukuu Mhe. Spika.
The Prophet Mohammad said "ooh, people verily at your Lord is one and you father is one, We are all belonging to Adam and Adam made up of clay, there isn't superiority for an Arab over non Arab, no superior for non Arab over an Arab, no superior fo white coloured over black skinned, no superior for black skinned over white coloured. The most important of you, is the one who is most prayer. Mwisho wa kunukuu Mhe Spika.
Kwa lugha yetu ya Kiswahili naomba kidogo niweke: Bwana Ahmad Deedat wakati anamnukuu Mtume (SAW) alisema kwamba:

> "Enyi watu kumbukeni kwamba bwana wenu ni mmoja na baba yenu ni mmoja nyote mnetokana na Adam ambae Adam ameumbwa kwa udongo hakuna nguvu kwa mwarabu kwa asiyekuwa mwarabu hakuna nguvu kwa asiyekuwa mwarabu mbele ya mwarabu, hakuna nguvu kwa mweupe mbele ya mweusi, hakuna nguvu kwa mweusi mbele ya mweupe, mbora wenu ni yule anamcha Mwenyezi Mungu sana".

Mhe. Waziri nakuomba sana hawa watu kama umewapa ile Skuli ya Ndagani imo ndani ya shamba ya Suleiman Ayoub Suleiman na ndugu zake ni Wazanzibari sote tumetokana na Adamu. Kwa hivyo, naomba haki yao ilindwe.

Nimalizie kwa *ZAWA*.

Mhe. Spika: Muda umemalizika. Kwa hiyo funga hotuba yako.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, namalizia kwenye *ZAWA*. Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwamba *ZAWA* kwamba hawa wanatupelekea maji vijijini. Lakini sasa hawa *ZAWA* wana matatizo na kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi katika ilivyo sasa maji yatakuwa hayatoshelezi milele na milele katika nchi hii kwa sababu Serikali yetu ni lemavu.

Mhe. Spika, niliuliza *possibility* ya kupata maji ya bahari nikaambiwa kuwa haiwezekani. Sasa mimi nashauri Serikali kwamba tuwekeni mitambo ya kutibia maji. Haya maji taka yaingie kwenye mitambo halafu yaweze kutumika tena Mhe. Waziri.
Mwisho nimalizie, katika wizara ambayo haiwezi kudhibiti maji taka ni hii wizara yetu hii, haiwezi kabisa. Mji Mkongwe Mhe. Waziri haupitiki ukipita maji yameshafufurika mara yakurukie katika nguo yako ya kusalia haiswaliki tena matatizo tu. Sasa mimi naishauri Serikali iyatibu yale maji kwanza ijenge miumndombinu mizuri ya maji taka, sio wayaachie yanatuharibia nguo ikawa hatuwezi kusali. Ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe bado tuna kikwazo kikubwa cha muda. Muda kwa kweli uko finyu mno, inabidi tujitahidi sana hizi shughuli zetu ziende kwa mujibu wa ratiba tulivyoweka.

Sasa tujitahidi kuliona hilo na umuhimu wa Wajumbe walio wengi kupata kuchangia ili kumsaidia Mhe. Waziri ili kuona kwamba hatimae wizara hii inafanyakazi kuwahudumia wananchi. Ni wizara ambayo

mambo yake yote yanawagusa wananchi kwa karibu mno. Kuna wachangiaji hadi sasa 31 tuliopata kuwasikiliza ni wachangiaji watatu.
Tatizo limeanza pale tuliposhindwa kupitisha Bajeti ya Ustawi wa Jamii jana. Angalau leo ingekuwa tuko nusu hapa, kesho Ijumaa bajeti ilipaswa imalizike kwa mujibu wa ratiba. Kwa idadi hii na kwa kuwa pamoja na kwamba tunaondoka saa 6 haturudi tena kwa mwezi wa Ramadhani kwa mujibu wa kanuni. Lakini tuone uzito huo ulivyo na jinsi ya shughuli zetu ambavyo inabidi ziende .

Kwa hiyo, tukubaliane kwamba shughuli zetu tujaribu kufupisha muda, ili tupate wachangiaji wengi tuepuke kurudia rudia sana hatimae angalau tusiende zaidi nje ya muda ambao tumejipangia ukapitiliza, ili shughuli zetu tuweze kumudu kuziendesha vizuri. Nataka niseme hayo ili kesho tujue namna gani tumejipanga.

Waheshimiwa Wajumbe sasa muda umefika tukapumzike na nichukuwe nafasi hii basi kuakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 12/07/2013 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 8:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 12/07/2013 saa 3:00 asubuhi)